# KWA NINI
## MIMI NI MSHIRIKA WA KANISA LA KRISTO



Na

LEROY BROWNLOW

# KWA NINI MIMI NI MSHIRIKA WA KANISA LA KRISTO

Na LEROY BROWNLOW

Uchapishaji: Niim Computers & Graphics (T)
Dar es Salaam - Tanzania

Mpangilio, usanifu, na uundaji wa chati: Adam Nathanael Evans

TANZANIA.

Watafsiri: Aritamba Bisansaba, James Mwamongi

Kimetafsiriwa 2015-2016

Wahariri
(2015-2017)
Bright Mwakaboko, Maurice Gasper Wisibo
(2020-2021):
Peter Kamatula , Bernard Kulanga, Israel Mhenga,
Baraka Asukileh, Adam Nathanael Evans

## HAKIUZWI

LEROY BROWNLOW,

Mchapishaji wa awali kwa Kiingereza.

3716 Avenue L Fort Worth 5, Texas

Kwa Kijana Wangu Paul Clyde Brownlow

Hakimiliki, 1945 Na LEROY BROWNLOW

Imetafsiriwa kutoka toleo la Saba.

Toleo la kwanza, Uchapishaji wa kwanza 2022.

ISBN #: 978-9912-40-082-5

Kwa masiliano zaidi au kupata taarifa za makusanyiko mbali mbali ambapo Wakristo wanakusanyika kuabudu, wasiliana

Arusha
076-747-5945
078-348-5751
075-491-7481
cmwanga3@gmail.com
Isaackusupa9@mail.com

Chimala
075-307-8704
Mfaumeremmy1@gmail.com

Mbeya
076-703-0084
godkipaka@mail.com

Morogoro
076-311-5079
065-864-8377
Mhengaisrael77@mail.com

Mwanza
075-467-0264
071-567-0264
kanisalakristokisiri@gmail.com

Dar es Salaam
075-263-4082
mbezicoc@gmail.com

Dodoma
078-476-9055
katitomnasi@gmail.com

Tunduma
075-380-2712

Iringa
065-849-3861
Christopherkapila269@mail.com

Njombe
062-086-3190
Myumbilwaa@gmail.com

Shukrani za kipekee kwa Shule ya Biblia ya video ya kimataifa (WVBS) kwa kutupatia ridhaa kuchapisha majedwali ya katika kitabu hiki.

https://video.wvbs.org/

https://www.youtube.com/user/worldvbs

https://video.wvbs.org/video/directors-invitation-to-prospective-students-wvbs-online-school/

https://gbntv.org/

# YALIYOMO

## SABABU YA


DIBAJI................................... .xiii

1 Kwa sababu lilianzishwa na Mjenzi wa kimaandiko - Kristo ... 1

2 Kwa sababu limejengwa juu ya msingi wa kimaandiko............ ... 9

3 Kwa sababu lilianzishwa katika eneo la kimaandiko - Yerusalemu ......................... . 17

4 Kwa sababu lilianzishwa katika nyakati za kimaandiko – Siku ya Pentekoste baada ya ufufuo wa Kristo ............................ . 31

**5** Kwa sababu Kristo ni mwanzilishi wa kanisa moja tu – kanisa lake . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 37

**6** Kwa sababu ni la kimaandiko kwa jina . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 53

**7** Kwa sababu muundo wake ni wa kimaandiko . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 73

**8** Kwa sababu lina Biblia pekee kama kiongozi cha imani, ungamo na mwongozo wake. . . . . 93

**9** Kwa sababu lina amini Biblia yote ni neno la Mungu lililovuviwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 107

**10** Kwa sababu linaamini kuwa Biblia ni kitabu kinachopaswa kutumiwa kwa usahihi ............ 125

**11** Kwa sababu sio la kimadhehebu . 149

**12** Kwa sababu ni la kimaandiko katika kufanya kazi ya kimisionari ............................ 167

**13** Kwa sababu linafundisha kwamba ufalme umekwisha anzishwa tayari na Kristo sasa ndiye mtawala ....................... 177

**14** Kwa sababu linatoa majibu ya kimaandiko kwa swali - nifanye nini ili niweze kuokolewa? ....... 195

**15** Kwa sababu linafundisha kwamba mtu anaokolewa kwa imani lakini sio kwa imani pekee .................................... 209

**16** Kwa sababu linafundisha kuwa mwanadamu ameokolewa kwa damu ya Kristo ...................... 223

**17** Kwa sababu linafundisha kwamba badiliko la moyo ni muhimu kwa wokovu wa mwanadamu .......................... 237

**18** Kwa sababu ya mafundisho na taratibu zake kuhusiana na maombi ................................ 251

**19** Kwa sababu linafundisha na kusimamia ubatizo wa kwenye Biblia .................................. 267

**20** Kwa sababu linafundisha kwamba mtoto wa Mungu anaweza kufanya dhambi na hivyo akapotea milele ............. 287

**21** Kwa sababu linafundisha kwamba watoto wachanga wanazaliwa wakiwa safi na bila hatia badala ya kupotea kabisa .................................. 309

**22** Kwa sababu linafundisha kwamba udhihirishaji wa kimiujiza wa Roho Mtakatifu umesitishwa .......................... 321

**23** Kwa sababu ya mafundisho yake ya kimaandiko na ushikaji wa meza ya Bwana ..................... 339

**24** Kwa sababu lina muziki wa kimaandiko wakati wa ibada ... 355

**25** Kwa sababu wokovu upo katika kanisa la Kristo ...................... 375

**K1** Kiambatanisho na Nyongeza 1.... 389

**K2** Viambatanisho, vielelezo, na chati .................................... 391

# DIBAJI

"*Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu*" (1 Petro 3:15).

Mwandishi aaminiye himizo hili, na kwa maombi ya wengi katika sehemu mbalimbali, ambao walishawahi kumsikia akihubiri mfululizo wa masomo katika mada hii–anawasilisha mbele za umma juzuu ya sababu za kimaandiko za kuwa mshirika wa kanisa la Kristo.

Wengi wa watu wapo jinsi walivyo kidini kwa sababu za kibinadamu kuliko za kimaandiko. Kwa mfano: "Ni kanisa maarufu"; "Ni kanisa rafiki"; "Mama yangu alikuwa mshirika wa kanisa hilo"; "Walinipata nikiwa bado mtoto mchanga kwa kizazi badala ya uzao": "Nilioa/kuolewa katika kanisa hili"; "Wana jengo zuri sana mjini." Sababu kama hizo hazina maana machoni pa Mungu na ni maneno matupu kwa watu wanaotamani kuongozwa na "hivi ndivyo asema Bwana."

Mwandishi wa kitabu hiki katika ujana wake hakuwa mshirika wa kanisa la Kristo.

Jitihada zimefanywa katika juzuu hii ili kuweka vitu ambavyo vitakuwa ni rasilimali kwa watoto wa Mungu katika kujiandaa kutoa jibu kwa kila mtu atakayewauliza sababu

kuhusiana na tumaini lililomo ndani yao, ni zana ambazo zinaweza kutumiwa nyumbani ili kuwafundisha watoto, kwa maana kila kizazi kinapaswa kufundishwa; kitabu ambacho kinaweza kutumika katika uinjilisti binafsi; juzuu ambayo itakuwa msaada kwa wale wanaofanya majadiliano katikati ya juma; na mfululizo wa masomo yaliyotengenezwa kwa ajili ya kazi ya darasa la Biblia.

Kiasi cha masomo kwa kila kipindi cha darasa hakikuwekwa, kwa sababu walimu tofauti wanakamilisha masomo hayo hayo katika muda tofauti. Kwa kuzingatia hili, sura zimegawanywa katika sehemu na mada mbalimbali, na kufanya kuwa rahisi kwa kila darasa kukamilisha masomo katika kasi itakayoonekana ni vema.

Mwandishi hasemi kuwa yeye ndiye chanzo cha kila mawazo au mjadala katika kitabu hiki. Ametoa kutoka katika vyanzo tofauti tofauti wakati wa maisha yake ya Kikristo: madarasa ya chuo, mihadhara, mafundisho, midahalo, mazungumzo, nakala za kidini na vitabu vingi. Ni vigumu kwake kutoa heshima kwa yule inayomstahili, lakini pale ambapo nukuu ya moja kwa moja inatumika, jina la mwandishi hutajwa pamoja na kitabu au nakala.

Kanisa ni "*...nguzo na msingi wa kweli*" (1 Timotheo 3:15). Neno la Mungu ni kweli (Yohana 17:17). Kwa hiyo, ni wajibu wa kanisa kufundisha na kufuata kila lililo kweli katika neno la Mungu,

ambayo mafundisho yake yanalenga mamlaka ya kibiblia pekee. Kuliko mafundisho yanayotokana na dini za kimwili zifanyavyo. Tunaposema kanisa la Kristo linafundisha au kufuata ukweli, inaeleweka kwamba kanisa katika mamlaka ya Biblia, linabeba ujumbe mtakatifu kama "...*nguzo na msingi wa kweli.*"

Limekuwa ni tamanio la moyo la mwandishi kuwasilisha sababu hizi kwa namna rahisi na lugha rahisi kadri iwezekanavyo, akiamini kwamba kweli hizi zinaweza kueleweka kirahisi na madaraja yote ya wanadamu. Vielelezo vinafanya kitabu chetu na masomo kuwa rahisi kwa wote; na vingetolewa vingi zaidi endapo nafasi ingeruhusu.

Nukuu zote za Maandiko zimetoka katika Biblia ya "Kiswahili Union Version", vinginevyo iwe imeelezwa tofauti.


Tumaini sasa limekuja kwamba kitabu hiki cha sababu za kuwa mshirika wa kanisa la Kristo kitakuwa mwanga kwa wale waliopo kwenye giza; chanzo cha msaada kwa wale wanaotafuta msaada wa Biblia; na chanzo cha utukufu kwa yeye ambaye atashughulika na kila kitabu kulingana na faida zake.

LEROY BROWNLOW

Fort Worth, Texas, USA



Ukumbusho: Shukrani kwa Makanisa ya Kristo Marekani kwa kufanya uchapishaji uwezekane. Kitabu hiki hakijaandikwa kwa kuibadili Biblia. Hiki kitabu ni kwa msaada wako tu.



# KWA NINI MIMI NI MSHIRIKA WA KANISA LA KRISTO

# 1

## SABABU YA KWANZA



## SABABU YA KWANZA

# Kwa sababu lilianzishwa na mjenzi wa kimaandiko – Kristo

**1. Hakuna kanisa liwezalo kuwa la kimaandiko mpaka litokane na mjenzi atokanaye na maandiko.**

UKWELI kwamba uwepo wa taasisi ya kidini ni ushahidi kwamba kuna mtu aliianzisha. Ulimwengu wa leo kuna mlundikano wa makanisa, yakitofautiana katika asili, mafundisho na desturi; kwa hiyo, kila moja lilianzishwa na Mungu au binadamu. Ama kimaandiko au si kimaandiko. Hivyo, ni muhimu kujua kama mwanzilishi wa kanisa, alifanya hivyo kimaandiko au si kimaandiko. Kama kanisa lilianzishwa si katika misingi ya maandiko, basi kanisa hilo si la kimaandiko: ni kazi ya binadamu na si ya Kristo.

**2. Kristo alianzisha kanisa la kimaandiko.**

A. Kuthibitisha kauli hiyo hapo juu

tunanukuu maneno ya Kristo, ambayo aliahidi kujenga kanisa: "*...na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu;...*" (Mathayo 16:18). Kwa hiyo, ni hakika kwamba hakuna kanisa linaloweza kuwa kanisa la kimaandiko isipokuwa lililoanzishwa na Kristo. Kama kanisa lilianzishwa na Henry VIII, John Calvin, John Wesley, Joseph Smith, Jr., au binadamu mwingine awaye yeyote, kanisa hilo bila shaka ni la kibinadamu.

B. Yesu, katika kutimiliza ahadi yake ya kujenga kanisa lake, alimpa Petro mamlaka ya kusema (au kuwasilisha) vigezo vya kuongezwa humo: "*Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni*" (Mathayo 16:19). Hakuna mwanadamu aliyewahi kuwa na mamlaka ya maandiko

hili kama alivyofanya Yesu, kwa kuwa hakuna mwanadamu mwenye mamlaka kimaandiko ya kuanzisha kanisa. Hili linaweza kusemwa tu na mwenye mamlaka yote ya mbinguni na duniani, mwanzilishi wa kanisa la kimaandiko.

### 3. Kanisa halikuanzishwa na Yohana Mbatizaji.

A. Wanadini wengi hudhani kwamba kanisa lilianzishwa na Yohana Mbatizaji. Lakini ukweli ni kwamba lilianzishwa na Kristo ni ushahidi dhahiri kuwa halikuanzishwa na Yohana Mbatizaji au binadamu mwingine yeyote.

B. Yohana alikuwa ameshafariki wakati Yesu anaahidi kulijenga kanisa. Katika Mathayo 14:10 tunasoma juu ya kuuwawa kwa Yohana: (Herode - mstari 6) "*akatuma mtu, akamkata kichwa Yohana mle gerezani.*" Weka akilini kwamba Yohana alikuwa ameshakufa tunapo kwenda sura mbili mbele na kuja katika ahadi ya Kristo katika Mathayo 16:18. "*Nitalijenga kanisa langu*". "*Nitalijenga*" ni wakati ujao. Yohana alikua ameshakufa na

uanzishwaji wa kanisa ulikua wakati ujao. Yohana Mbatizaji alikuwa mtu mkuu na alifanya kazi ya kimaandiko, yaani yeye alikuwa mtangulizi ambaye alimtangulia Bwana kuwaandaa watu kumpokea (Isaya 40:3; Malaki 3:1; Luka 1:17). Yohana alifanya hivyo, lakini yeye hakuanzisha kanisa ulisomalo ndani ya Biblia (kanisa la Biblia) wala kanisa lingine lolote lijulikanalo kwa wanadamu.

C. Haiwezi kuthibitishwa kuwa Yesu, katika kuahidi kujenga kanisa lake, alikuwa anaahidi kujenga mwendelezo wa yale ambayo Yohana alikuwa ameanzisha. Hoja hiyo haijasimama, kwa sababu rahisi kwamba Yesu aliahidi kujenga kanisa lake kuanzia katika msingi: "*.... juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu ...*" Mathayo 16:18.

D. Yohana Mbatizaji kamwe hakuwahi kuwa mshirika wa kanisa, au raia wa ufalme wa mbinguni. Yesu alisema, "*Amin, nawaambieni, Hajaondokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji; walakini aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni*

*mkuu kuliko yeye*" (Mathayo 11:11). Yawezekanaje kwa Yohana kuwa mmoja wa mkuu aliyezaliwa na uzao wa mwanamke, lakini aliye mdogo kabisa (mwenye umhimu mdogo) katika ufalme au kanisa kuwa bora zaidi yake? Mfano huu utaweza kufafanua hili: katika shule ya msingi hakuna zaidi ya Bill, lakini aliye mdogo katika shule ya sekondari ni mkubwa zaidi kuliko yeye: hii ni kweli kwa sababu Bill hayupo katika shule ya sekondari. Hivyo Yohana Mbatizaji hakuwa katika kanisa au ufalme wa mbinguni.

**4. Mimea mingine itang'olewa.**

Kanisa la Kristo lilianzishwa na Kristo na milango ya kuzimu *(hádēs)* haitalishinda; lakini mimea mingine itang'olewa. Onyo liko wazi sana na adhabu ni kubwa mno kwa mimi kuwa mshirika wa kanisa ambalo halijapandwa na Baba. Yesu, akizungumzia dini zilizojengwa juu ya tamaduni na mapokeo ya wazee, akasema, "*...Kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni litang'olewa*" (Mathayo 15:13). Hiyo ilikuwa wakati wa sheria ya Musa. Mungu alipanda dini ya Kiyahudi, na mimea mingine

iling'olewa. Kama Mungu atang'oa mimea mingine katika mfumo wa ibada, Je, hatafanya hivyo chini ya mfumo wa Kikristo? Ni lazima tukubali kwamba kiwango hakijapunguzwa; Kwa hiyo, onyo hilo linaweza kutumika katika mfumo wa Ukristo wa sasa. Na tuzingatie onyo lililotolewa na Bwana.

# UCHUNGUZI NA HITIMISHO

## KWA NINI MIMI NI MSHIRIKA WA KANISA LA KRISTO

# 2

## SABABU YA PILI



## SABABU YA PILI

# Kwa sababu limejengwa juu ya msingi wa kimaandiko

### 1. Umuhimu wa msingi mzuri

Ni ukweli ulio wazi kwamba hakuna jengo au taasisi inayoweza kuwa na nguvu zaidi kuliko msingi wake. Nguvu ya chochote hutegemea moja kwa moja msingi wake. Hakuna nyumba iliyojengwa nje ya uwiano wa msingi wake inayoweza kusimama kwa muda mrefu. Kanisa nalo ni sawa halina utofauti, utulivu wake na faida hutegemea msingi wake.

A. Kanisa la kimaandiko lazima liwe na msingi wa kimaandiko; vinginevyo halitakuwa la kimaandiko. Hivyo hakuna mtu anayeweza kudai kuwa mshirika katika kanisa la kimaandiko isipokuwa kwa kuwa mshirika wa kanisa lililojengwa juu ya msingi wa kimaandiko.

### 2. Upi ni mwamba au msingi

A. Kutambua utambulisho wa mwamba,

yatupasa kwanza kutambua ukiri ambao mwamba unalirejelea. Petro alimkiri Kristo: "*Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai*" (Mathayo 16:16). Yesu akamwambia Petro mara moja: "*Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro...*" Kisha, Kristo aliahidi kujenga kanisa lake juu ya mwamba huu. Mwamba, kwa hiyo, ni lazima kukiri kwa Kristo mbele ya Petro au kukiri kwa Petro mbele ya Kristo. Wengi wamekuwa wakiamini kwamba mwamba una uhusiano na Petro, kwa vile neno "*Petro*" maana yake mwamba au jiwe. Lakini lugha ya asili hairuhusu tafsiri hii kwa sababu maneno mawili tofauti hutumika: "*Wewe*

1 Kitabu Rejea: (Help Word Studies / Inasaidia Kujifunza Maneno):

"#4074 Pétros (Nomino ya kiume) yaani jiwe, jiwe dogo, linaloweza kupatikana hata pembenzoni mwa njia.

*ndiwe Petro* [*Petros*[1]], *na juu ya mwamba* [*Petra*[2]] *huu nitalijenga kanisa langu...*" (Mathayo 16:18). Hivyo Yesu hakuwa na ahadi ya kujenga kanisa lake juu ya Petro (*Petros*[1] - jiwe dogo) lakini juu ya jabali (*Petra*[2] - mlima uliyofanywa kwa mawe ambao hauwezi kuondolewa) badala yake ni katika: Ukuu na utukufu wa kweli ambao ni Kristo Mwana wa Mungu. Hivyo, kanisa la Bwana halijawahi kujengwa juu ya mwili dhaifu wa kibinadamu, lakini juu ya uungu na hali ya Kristo kuwa mwana wa Mungu.

#4074 (Pétros) ("jiwe dogo") hivyo ni tofauti na #4073 (pétra) ("jabali") <Abbott-Smith> (mlima uliyofanywa kwa mawe ambao hauwezi kuondolewa)

1 "#4074 (Pétros) ni jiwe" - "#4074 (Pétros) mara zote humaanisha jiwe.....ambalo mtu huweza kulirusha kwa mkono.
Wavuti: http://biblehub.com/greek/4074.htm

2 "#4073 (pétra) ni jabali" (TDNT, 3, 100). "#4073 (pé-tra), ni
mwamba au jabali uliyojitokeza" (S. Zodhiates, Dict)."
Wavuti: http://biblehub.com/greek/4073.htm

**Angalia kiambatanisho nyuma ya kitabu kwa maelezo zaidi.**

B. Vifungu vingine hutoa fasiri hii:

(1) "*Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani Yesu Kristo*" (1 Wakorintho 3:11).

(2) "*Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni*" (Waefeso 2:20).

(3) *"kwa ajili ya hayo Bwana, MUNGU, asema hivi, Tazama, naweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara..."* (Isaya 28:16). "*Jiwe walilolikataa waashi Limekuwa jiwe kuu la pembeni*" (Zaburi 118:22). Yesu akatimiliza unabii huu juu yake mwenyewe. *"Yesu akawaambia, Hamkupata kusoma katika maandiko, Jiwe walilolikataa waashi, Hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni; Neno hili limetoka kwa Bwana, Nalo ni ajabu machoni petu?"* (Mathayo 21:42). Petro pia alisema unabii huu ulikuwa unazungumzia kuhusu Yesu Kristo; *"Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa*

*na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni"* (Matendo 4:11). Ushahidi huu unastaajabisha!

**3. Msingi huu utasimama**

A. Msingi mtukufu kwamba Kristo Mwana wa Mungu umesimama na utaendelea kusimama. Fitina pamoja na mashambulizi ya upinzani hayajaweza kuudhoofisha. Makafiri, wapingaji wa uwepo wa Mungu, wageuza dini, na wenye wasiwasi hulalama na kupiga makelele, lakini Kristo bado ni Mwana wa Mungu aliye hai. Mwamba huu unaweza kulinganishwa na fuawe kongwe lililopigwa nyundo nyingi. Msingi huu unasimama salama na imara leo hata milele.




B. Inasemekana kwamba katika karne ya 18, Voltaire, mwanafalsafa Mfaransa (1694-1778) anayejulikana kwa kupinga Ukristo na Biblia, kwa majivuno alitangaza kwamba

hakutakuwa na nakala ya Biblia baada ya miaka 100 kupita (akimaanisha kuwa hakutakuwa na Biblia duniani ifikapo karne ya 19)[1]. Kitabu hiki kilichapwa mnamo karne ya 21 na Biblia ipo hapa hata leo. Imeshatimia zaidi ya miaka mia moja tangu unabii wake wa kufuru ulipotolewa na hakuna dalili za kutimilika sasa kuliko ilivyokuwa wakati huo. Chombo hicho cha habari kilichotumiwa kutoa utabiri huo wa kikafiri sasa kinatumiwa na jumuiya ya Biblia ya Geneva[2]. Ni unabii gani huo!

C. Lakini vipi kuhusu taasisi za watu zilizojengwa juu ya watu? Zimewekwa juu ya mchanga; misingi ni dhaifu na ni lazima wataanguka tu. Kanisa la Kristo laja kwa ushindi, kwa kuwa liko juu ya jiwe lililojaribiwa, msingi wa uhakika.

1 https://bellatorchristi.com/2019/03/18/voltaires-prediction-home-and-the-bible-society-truth-or-myth/

2 The Missionary Register for 1836, William Acworth, "Bible Notices in Switzerland and Italy," (London: L&G Seeley, 1836), 352.




Inatumiwa kwa idhini ya; "World Video Bible School"{WVBS} yaani Shule ya Biblia kwa njia ya filamu ulimwengu. https://video.wvbs.org/

# KWA NINI MIMI NI MSHIRIKA WA KANISA LA KRISTO

# 3

## SABABU YA TATU



## SABABU YA TATU

# Kwa sababu lilianzishwa katika eneo la kimaandiko matakatifu-Yerusalemu

### 1. Kanisa ambalo halijaanzishwa katika eneo la kimaandiko matakatifu sio kanisa la kimaandiko.

SABABU NYINGINE ya kuwa mshirika wa kanisa la Kristo ni kwamba lilianzishwa Yerusalemu, mahali pa kimaandiko. Kama mtu anataka kuwa mshirika wa kanisa fulani lililoanzishwa kwa mara ya kwanza London au New York, Dar es Salaam au Nairobi, hawezi kudai kuwa yeye ni mshirika wa kanisa la Kristo; kwa sababu kanisa la Kristo asili yake sio London au New York, Dar es Salaam au Nairobi. Mtu hawezi kuwa mshirika wa kanisa la kimaandiko isipokuwa kwa kuwa mshirika wa kanisa lililoanzishwa katika mahali pa Maandiko.

### 2. Vifungu kadhaa vinavyoonyesha kuanzishwa kwake

A. Kwanza tusome unabii wa Isaya: "*Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima*

*wa nyumba ya BWANA utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na mataifa yote watauendea makundi makundi. Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani kwa BWANA, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la BWANA katika Yerusalemu*" (Isaya 2:2-3). Kutokana na unabii huu tunajifunza, kwanza, kwamba nyumba ya Bwana ilipaswa kuanzishwa Yerusalemu.

Pili, nyumba ya Bwana itainuliwa na mataifa yote wataiendea ndani yake.

Tatu, wakati wa kutimiza itakuwa katika siku za mwisho. Ni lazima sasa kujifunza maana ya nyumba ya Bwana. Paulo anaongea kuhusu "*... nyumba ya Mungu, iliyo kanisa*

*la Mungu aliye hai ...*" (1 Timotheo 3:15). Hivyo nyumba ya Bwana ni kanisa, na kutoka katika kifungu hiki tunajifunza ni lini na wapi lilipaswa kuanzishwa: –yaani katika siku za mwisho huko Yerusalemu.

B. Katika Mika 4:1–2 tunaona unabii huo katika maneno kama hayo: "*Lakini itakuwa katika siku za mwisho, ya kwamba mlima wa nyumba ya BWANA utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na watu wa mataifa watauendea makundi makundi. Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani kwa BWANA, na nyumbani kwa Mungu wa Yakobo; naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake; kwa maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la BWANA litatoka Yerusalemu.*"

C. Zekaria pia alitabiri kwamba nyumba ya Bwana au kanisa yapaswa kuanzishwa Yerusalemu: "*Kwa sababu hiyo BWANA asema hivi, Ninaurudia Yerusalemu kwa rehema nyingi; nyumba yangu itajengwa ndani yake, asema BWANA wa majeshi, na kamba itanyoshwa juu*

*ya Yerusalemu* " (Zekaria 1:16). Hivyo mara nyingine tena Roho Mtakatifu anafundisha kwamba kanisa asili yake ni Yerusalemu.

D. Katika kuanzisha utume wa duniani kote, Yesu alifundisha kwamba Yerusalemu ilikuwa mahali pa kuanzia: "*Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya. Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu*" (Luka 24:46-49). Yafaa kukumbuka:

(1) Ilimbidi Kristo kuteswa na kufufuka kutoka katika wafu kabla ya toba na ondoleo la dhambi kuhubiriwa kwa jina lake.

(2) Kutangazwa kwa ujumbe huu kulipaswa kuanzia Yerusalemu.

(3) Walikuwa wakae Yerusalemu mpaka walipopewa nguvu kutoka juu.

Yesu hapo awali aliwaahidi mitume nguvu hii ambayo wangeipokea kutoka juu. Yawekwa dhahiri katika Yohana 14:26; 15:26-27; 16:7-8 kwamba Msaidizi, Roho Mtakatifu, asingekuja mpaka Yesu aondoke, na kwamba wakati Roho Mtakatifu ajapo angeweza kufanya mambo kadhaa – yaani: Kufundisha mitume vitu vyote, kuwakumbusha juu ya kile Yesu alichosema na kuuweka hatiani (kukemea) ulimwengu wa dhambi. Hii ni nguvu ambayo mitume waliamuliwa kuisubiri huko Yerusalemu.

**3. Kutimilika kwa vifungu hivyo**

A. Roho Mtakatifu hakupaswa kuja mpaka Yesu aondoke, *"Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa nyinyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu*" (Yohana 16:7). Mitume walimwona akipaa na kutoweka machoni pao, "*Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao*" (Matendo 1:9).

B. Mitume waliamuriwa kusubiri Yerusalemu (Luka 24:49). Baada ya mitume kumwangalia Bwana wao akipaa wakarudi Yerusalemu (Matendo 1:12), mahali maalumu palipochaguliwa; na walikaa huko.

C. Mitume walivishwa nguvu kutoka juu (Luka 24:49). Katika Matendo 2:1-4) tunasoma kutimilika kwa ahadi hii: "*Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.*" Roho Mtakatifu alipaswa kuja na tunaona kwamba alishuka huko Yerusalemu siku ya Pentekoste.

D. Neno la Bwana lilisonga mbele nje ya Yerusalemu katika siku za mwisho (Isaya 2:2-3; Mika 4:1-2). Tunaona kutimilika kwa unabii huu Matendo 2:14-42, ambapo kuchochea mahubiri

kunahubiriwa Yerusalemu. Hii ilitokea katika siku za mwisho; kwa Petro akanukuu unabii wa Yoeli (Yoeli 2:28-32) kama ushahidi wa yaliyotokea katika siku za mwisho. Kwa hiyo, hii ilikuwa sehemu sahihi na wakati sahihi.

E. Toba na ondoleo la dhambi lapaswa kuhubiriwa kwa jina la Bwana, kuanzia Yerusalemu (Luka 24:47). Petro atangaza ujumbe huo, akisema, "*Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu...*" (Matendo 2:38).

F. Nyumba ya Bwana (kanisa) kuanzishwa huko Yerusalemu siku za mwisho (Isaya 2:2-3; Mika 4:1-2; Zekaria 1:16). Hapo ndiyo mahali na wakati lilipoanzishwa. Wale waliosikia Injili siku ya Pentekoste katika Yerusalemu, ambao waliamini, walitubu na kubatizwa nao waliongezwa kwalo; "*Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu*" (Matendo 2:41). Katika mstari wa arobaini na saba wa sura hiyo tunasoma kwamba Bwana aliwazidisha katika kanisa. Hii ilitokea katika siku za mwisho

kwa Petro kunukuu unabii wa Yoeli katika ushahidi kwamba mambo yale yalipaswa kutokea katika siku za mwisho (Matendo 2:17-21). Kabla ya Matendo 2, kanisa linazungumzwa kama kitu kijacho wakati ujao. Hapa katika Matendo 2, kanisa linazungumzwa kama kitu kilichopo tayari na sio kitu kinachotarajiwa kuja wakati ujao. (Ona mfano kuhusu Pentekoste katika kurasa za 34-35). Hivyo, kulingana na unabii na utimilifu wake, kanisa la Kristo asili yake ni Yerusalemu. Hili ndilo kanisa ambalo mimi ni mshirika.

4. **Upandikizaji wa kanisa hilo katika jamii yoyote au nyakati zozote unategemea upandaji wa mbegu hizo hizo badala ya kufanya mwendelezo wa kanisa.**
   A. Hakuna tija katika mwendelezo wa mfululizo wa kanisa. Hata kama mtu anaweza kufuatilia taasisi, mwaka hadi mwaka, tokea kuanzishwa kwake, bado hapati uhakika wa kuwapo katika taasisi ile ile iliyokuwepo mwanzo. Kwa miaka kadhaa kusanyiko lingeweza kuondoka (au kuasi) hivi kwamba lisiweze kuwa kanisa la kweli. Paulo

alisema kwamba uasi, au kuanguka mbali, kutakuja. Hebu soma vifungu vichache, tafadhali:

(i) "*Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao*" (Matendo 20:29-30).

(ii) "*Basi, ndugu, tunakusihini, kwa habari ya kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo, na kukusanyika kwetu mbele zake, kwamba msifadhaishwe upesi hata kuiacha nia yenu, wala msisitushwe, kwa roho, wala kwa neno, wala kwa waraka unaodhaniwa kuwa ni wetu, kana kwamba siku ya Bwana imekwisha kuwapo. Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe*

*kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu*" (2 Wathesalonike 2:1-4).

(iii) "*Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe; wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula, ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli*" (1 Timotheo 4:1-3).

Nukuu za hapo juu zinaonyesha wazi kwamba kanisa la kikengeufu lingeinuka nje ya kanisa la kweli; Kwa hiyo, kanisa lolote ambalo lingewezekana kuchanganuliwa mlolongo wa mwendelezo kwa asili mpaka Yerusalemu na Pentekoste lingewezekana likawa kanisa lililokengeuka. Kama mtu angeweza kurejea mwanzo ingewezekana kuwa kanisa la kweli. Lakini pia, kama

mtu angeweza kurejea mwanzoni wangeweza kuwa kanisa lililokengeuka kwa sababu yote yanaweza kurejea mwanzo. Hii ni kwa sababu kanisa lililokengeuka limetoka kwenye kanisa la kweli, hivyo basi kurejea mwanzo si njia mahususi ya kuthibitisha kwamba kweli ninyi ndilo kanisa la kwenye Biblia.

B. Ni bora kuwa na hamu ya kuona kama tunapanda mbegu moja sawa na mbegu za mitume. Tunaambiwa katika mfano wa mpanzi, neno la Mungu ni mbegu ya ufalme huo (Luka 8:11). Kama tukipanda mbegu moja sawa na mitume, kanisa pia litachanua sawa nao; "*Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna*" (Wagalatia 6:7).

Kila mbegu huzaa kwa aina yake. Ukipanda shayiri na utavuna shayiri; ukipanda ngano na utavuna ngano; ukipanda mbegu halisi ya ufalme (kanisa) utavuna kanisa la kweli. Wakati mbegu ya ufalme ilipopandwa zamani katika karne ya kwanza haikuzaa mazao ya majina yanayobeba

mwelekeo wa imani ya kikundi fulani au wanadamu. Wala mbegu ya ufalme haitazalisha mazao kama hayo leo. Kwa hiyo ni lazima tukubali kwamba mazao kama hayo yapo leo kwa sababu baadhi ya mbegu nyingine zaidi ya mbegu ya ufalme zimepandwa. Neno la Mungu, mbegu ya ufalme, inazaa Mkristo tu; mazao mengine yote wamekuwa yakizalishwa na mbegu nyingine.

C. Nasi sasa tunatoa mifano: Kama mahindi yote yaotayo ulimwenguni yakaharibiwa, bado tutaendelea kuwa na mahindi ikiwa tu tutaendelea kuwa na mbegu ya mahindi. Mbegu hii inaweza kupandwa (hata kwa muda mrefu baadaye na huenda hata katika sehemu tofauti) na utapata mazao sawa kabisa na ya awali. Kwa namna hiyo niruhusu niseme kwamba kama mikusanyiko yote ya kuongezeka kwa kanisa la kweli itakuwa imeharibiwa na uasi au mateso na kupotea kwa miaka elfu moja, kanisa la Kristo halita haribiwa kwa kuwa neno la Mungu, mbegu ya ufalme hubaki. Kwa kuipanda mbegu ile ile mahali popote

tunanaweza kupanda kusanyiko la wanafunzi sawa kabisa katika namna zote na lile la awali.

"*Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe*" (Marko 13:31).

Kanisa hili la Kristo lililoanzia Yerusalemu, linaweza kuanzishwa katika mji wowote au jamii yoyote kwa kuhubiri Injili kama ile ile ya mitume. Miaka michache baada ya kanisa la Bwana kuanza kwa asili yake huko Yerusalemu, Paulo akaenda Korintho na kulipanda huko. Alisema, "*Mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu*" (1 Wakorintho 3:6). Taasisi iliyopandwa katika Korintho inaweza kupandwa katika sehemu yoyote dunia wakati wowote, ilimradi mtu anaifanya kwa makini na kupanda mbegu moja ile ya mitume. Hapa ndipo nia yetu kuu inapolalia.

# 4

## SABABU YA NNE



## SABABU YA NNE

# Kwa sababu lilianzishwa katika nyakati za kimaandiko – Pentekoste baada ya ufufuo wa Kristo

### 1. UTANGULIZI

Wakati wa uanzishwaji wa kanisa umeonyeshwa kwa kifupi na kwa ufasaha katika kuonyesha wapi kanisa lilianzishwa. Kwa ukweli huo, sitakupeleka kwenye majadiliano marefu, kuthibitisha kuwa taasisi hii iliundwa wakati wa siku ya Pentekoste; Hili jedwali litatusaidia kubaini ukweli; Safu ya maandiko ndani yake bila shaka inathibitisha kuwa Pentekoste ndio ulikuwa wakati.

Kanisa lolote ambalo halijajengwa wakati wa Pentekoste sio kanisa la kweli. Hii ni moja ya vipimo ambavyo huamua kama kanisa ni kanisa la kweli au kanisa bandia. Katika kuangalia kanisa la kimaandiko, angalia alama; limeanzishwa na Kristo; limejengwa juu ya Kristo; limeanzia Yerusalemu; siku

ya Pentekoste; kanisa lolote ambalo halijabeba alama hizi sio kanisa ambalo Kristo aliahidi kulijenga. Linaweza kuwa na watu wengi ndani yake na kufundisha mambo mengi bora, lakini si kanisa la Mungu aliye hai; ni kanisa la binadamu lililowekwa juu ya matakwa ya binadamu wasiopenda kuchunguza na kuamini bila ushuhuda wa kutosha, kutoka katika Maandiko.

**1** 3,000 walizidishwa siku ile.
**Matendo 2:41**

**2** Ni katika siku za mwisho.
**Matendo 2:17-21**

**3** Ni katika Yerusalemu.
**Luka 24:46-49; Matendo 1:12; 2:1-6**

**4** Ni katika siku za wafalme hao.

**5** Ni katika siku za baadhi ya wanafunzi.
**Matendo 1:15 - Matendo 2:9**

**6** Nguvu ilishuka.
**Matendo 2:1-4**

**7** Ilianza pale Roho Mtakatifu alipowashukia Mitume.
**Matendo 11:15**
Roho Mtakatifu alishuka siku ya Pentekoste.

**8** Unabii wa Agano la Kale uliutizamia wakati ujao kwa ajili ya utimilifu wa kuja kwa ufalme/kanisa. Kitabu cha Matendo cha Agano Jipya kinaandika utimilifu wa unabii na uanzishwaji wa kanisa mnamo siku ya Pentekoste kutokana na kusulibishwa kwake. Maandiko ya Agano Jipya pia huzungumza juu ya kanisa kana kwamba limekwisha kuanzishwa katika siku ya Pentekoste baada ya kifo cha Yesu msalabani.

**Isaya 2:24**
Siku za mwisho katika Yerusalemu.
01

**Mika 4:12**
Siku za mwisho katika Yerusalemu.
02

**Danieli 2:44**
Katika siku za Wafalme hao.
03

**Mathayo 3:1-2**
Unakaribia.
04

**Marko 1:15**
Unakaribia.
05

**Mathayo 6:9-10**
Walitakiwa kuomba juu ya ujio wake.
06

**Mathayo 16:18**
Ataujenga.
07

**Marko 9:1**
Utakuja wakati baadhi ya wanafunzi watakuwa hai.
08

**Mathayo 18:3**
Wanafunzi hawakuuingia
09

**Luka 10:9**
Umewakaribia
10

**Luka 22:18**
Utakapokuja
11

# PENTEKOSTE

**Matendo 2:47**
Akalizidisha
01

**Wakolosai 1:13-14**
Waana wa Ufalme
02

## Ni kwa namna gani kundi lenu la kidini linafanania na kanisa ulisomalo katika Biblia?

**ANDIKA TAARIFA ZA KUNDI LA KIDINI ULILOPO**

(Jaza jibu katika miduara ifuatayo na ulinganishe na majibu yako)

### MJENZI

**KRISTO**
**MATHAYO 16:18**

### MSINGI

**YESU**
**MWANA WA MUNGU**
**YOHANA 3:16**

### MAHALI

**YERUSALEMU**
**LUKA 24:47**

### MUDA

**PENTEKOSTE**
**BAADA YA**
**KRISTO KUFUFUKA**
**MATENDO 2**

# 5

## SABABU YA TANO



## SABABU YA TANO

# Kwa sababu Kristo ni mwanzilishi wa kanisa moja tu – kanisa lake

### 1. USHAHIDI NA UTHIBITISHO

Yeye ambaye ana mamlaka yote mbinguni na duniani alisema, "*...juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu...*" (Mathayo 16:18). Yesu hakusema kwamba angeweza kujenga kanisa, makanisa yake au moja ya makanisa yake. Hivyo hayo ni mangapi Yesu aliahidi kujenga? Alisema, "*nitalijenga kanisa langu*". Hebu zingatia: K-A-N-I-S-A - Hiyo ndiyo idadi ambayo Yesu aliahidi kujenga. Kila mtu ambaye anajua chochote kuhusu lugha ya Kiswahili anaweza kusema kama hapo ni umoja au wingi. Ni vigumu kwa watu wengi wazuri, katika mtazamo wa hali ya sasa, kuamini juu ya umoja wa kanisa, lakini, msururu wa makanisa tuliyo nayo hauna uwezo wa kubadilisha maneno ya Kristo. Yeye asema, "*maneno yangu hayatapita kamwe*"

(Mathayo 24:35)

A. Paulo anafundisha kwamba kuna mwili mmoja: "*Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu*" (Waefeso 4:4). "*Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja; Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake*" (Warumi 12:4–5). "*Lakini sasa viungo ni vingi, ila mwili ni mmoja*" (1 Wakorintho 12:20). Paulo, kama tunavyoona, amefundisha muda baada ya muda umoja wa mwili. Je, mwili maana yake kanisa? Tutaona; "*akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote*"

(Waefeso 1:22-23). Katika fungu hili, Paulo anatuambia kwamba kanisa ni mwili. Katika Wakolosai 1:18 anafundisha kwamba mwili ni kanisa. Kwa hiyo, kanisa ni mwili na mwili ni kanisa. Kuna mwili mmoja tu; hivyo kuna kanisa moja tu. Tazama jinsi ambavyo hayo yanakubaliana na ahadi, "...*nitalijenga kanisa langu...*" (Mathayo 16:18).

B. Umoja wa kanisa pia unaonekana katika takwimu za shamba la mizabibu, na Mungu mkulima wake; "*Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima*" (Yohana 15:1). Hatuoni taswira ya mashamba ya mizabibu



tofautitofauti kila moja likikinzana na lingine, yote yakilimwa na mkulima mmoja. Tunaona muunganiko wa shamba moja la mzabibu, matawi yote yakiwa pamoja na kuishi katika Kristo (Mzabibu), lenye kutunzwa na mkulima mmoja (Baba Mungu). Kuna mamia ya mizabibu (mashamba) ya kidini katika dunia ya leo, kila moja akidai Mungu kuwa mkulima wake. Hiki ndicho tunakiona kwa kuinua macho yetu na kuiangalia dunia, bali hatuoni hilo tukiinua macho na kuitazama Biblia. Kwa hiyo, tunaona mzabibu (shamba) moja na mkulima mmoja.

C. Wazo hili la kanisa pia limeoneshwa zaidi katika sura ya mzabibu na matawi: Kristo ni mzabibu wa kweli na kila mtu aliyekombolewa ni tawi katika mzabibu;

> "*Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha, ili lizidi kuzaa. Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia. Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama*

*vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote. Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea*" (Yohana 15:1-6).

Hapa hatuoni Kristo kama wingi wa mizabibu na matawi mengi katika kila mzabibu, kila mzabibu na matawi yake kukua kwa njia yenye mgogoro katika ukuaji wa na mizabibi mingine; Hapana! Wala hatulioni hilo kabisa. Tunaona mzabibu mmoja mkubwa na mzuri, Kristo, Mwana wa Mungu, na kila aliyeokolewa ni tawi ndani yake, ameokolewa naye na kuzaa matunda kwa heshima na utukufu wake. Jinsi gani picha ya kidunia na ile ya Biblia zinapingana.

Wapo watu katika majaribio na vitendo vyenye kukosa tumaini vyenye kutaka kuhalalisha dini wamejaribu kutuambia

kwamba mzabibu ni kanisa la awali na kweli na matawi ni madhehebu mbalimbali katika dunia. Huo ndo utetezi wao namba moja kuhusu madhehebu. Fikra kidogo tu zitaweza kuonyesha kwamba hilo haliwezi kuwa kweli kwa sababu kadhaa:

(1) Kristo alikuwa akiongea na wanafunzi wake badala ya makanisa aliposema, "*Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi...*" (Yohana 15:5). Ni kutumia tofauti ujumbe wake kwa kutumia taarifa hiyo kuwakilisha makanisa wakati yeye alielekeza kwa watu.

(2) Kristo alisema, "*Kaeni ndani yangu...*" mzabibu wa kweli. Kama wewe hukaa katika tawi, basi upo katika hatia ya kukosa. Kristo hakusema, "Kaeni katika tawi"; alisema, "*Kaeni ndani yangu...*" (mzabibu).

(3) Anasema waziwazi kwamba tawi ni mtu: "*Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi ...*" "*Mtu*" ni "*tawi*".

(4) Haiwezi kuwa kweli kwa sababu

# “Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo?” 1 Cor. 1:13




“... kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.
1 Kor. 1:10

“Maana hapo mtu mmoja asemapo, Mimi ni wa Paulo; na mwingine, Mimi ni wa Apolo, je! Ninyi si wanadamu? Basi Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Ni wahudumu ambao kwao mliamini...”
1 Kor. 3:4-5

“Mimi ni mzabibu,
**ninyi** ni matawi...”
Yohana 15:5




“ Mkizishika amri zangu mtakaa katika pendo langu...”
Yohana 15:10

“**Mtu** asipokaa ndani yangu, **hutupwa** nje kama tawi na kunyauka...”
Yohana 15:6


hutia dosari katika mfano wa uwianisho. Ni upotoshaji na ujinga kufikiri kwamba juu ya mzabibu wa kweli zitazaliwa zabibu, tikiti maji, tango, maboga, nk. Watu wenye fikra hawawezi kamwe kukubali kitu kionekane chenye mantiki katika ulimwengu wa kiroho, wakati hata katika ulimwengu wa kawaida kinaonekana wazi wazi ni upuuzi; hata hivyo hakuna upuuzi kuzidi upuuzi wa madai ya mwanatheolojia asiye na Maandiko kuthibitisha fundisho lake.

D. Umoja wa kanisa pia unawasilishwa katika sura ya nyumba au familia: "*... nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai...*" (1 Timotheo 3:15). Nyumba ya Mungu ina maana familia ya Mungu. Kwa mfano, tunaposoma kuhusu kuongolewa kwa mlinzi wa gereza na nyumba yake tunajua kwamba ilikuwa ni mlinzi wa gereza pamoja na familia yake (Matendo 16:23-40). Pia, nyumba ya Mungu ni familia ya Mungu; na familia ya Mungu ni kanisa la Mungu. Tunaona katika Biblia picha ya wazi kwa familia ya

Mungu kama Baba, Kristo kaka na wote waliookolewa kama "*... watoto wa Mungu; na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo...*" (Warumi 8:16-17). Wala hatuoni katika Biblia taswira ya mamia ya familia mbalimbali, kila moja au zaidi au kupingana na nyingine zote, kila moja kwa serikali yake tofauti na nyingine, kila moja imevaa jina lake yenyewe, na kila moja ikidai Baba mmoja na kaka mkubwa mmoja, na kila mtoto katika kila familia akidai kuwa mrithi. Hii itakuwa kama ndoa batili. Mtu na hapaswi kwa neno au kwa tendo kuleta picha ya namna hiyo mbele za Mungu. Picha ya Mungu ni moja ya umoja wa familia kubwa na Mungu kama Baba na Kristo kama Kaka mkubwa, na wanafamilia wote wakifanya kazi kwa pamoja kwa manufaa ya familia.

E. Wazo hili la umoja kwa mara nyingine tena limeonekana katika taswira ya kundi moja na mchungaji mmoja: "*... kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja*" (Yohana 10:16). Ni lazima kuangalia katika dunia badala ya

Biblia kuona makundi mengi, kila moja likidai kuwa na mchungaji mmoja. Mungu hana picha hii katika neno lake ya mamia ya makundi, kila mmoja kwa aina yake ya pekee ya kondoo, na kila moja au zaidi likipingana na mengine yote. Mungu anasema: "... *kundi moja na mchungaji mmoja.*" Akili zote, utajiri wote, na heshima zote za ulimwengu vyote haviwezi kubadili neno lake. Sasa hakuna makundi zaidi ya idadi ya wachungaji. Mchungaji yupi unayemfuata? Katika swali hili kuna jibu moja pekee: Mchungaji mkuu Yesu Kristo. Wewe ni mshirika wa kundi gani? Katika swali hili kuna jibu moja tu: Kuna kundi moja tu. Kundi la Mungu. Kuna mchungaji mmoja na kundi moja.



F. Fikiria mfano mwingine, tafadhali : wakati huu, mfano wa mwili wa binadamu. Kanisa limeoneshwa katika sura ya mwili wa binadamu pamoja na Kristo kama kichwa na wote

waliokombolewa kama viungo vya mwili , kufanya kazi chini ya udhibiti na mwelekeo wa kichwa (1 Wakorintho 12:12-27; Wakolosai 1:18). Mwili mmoja na kichwa kimoja. Katika ulimwengu wa kidini tunaona mamia ya miili, yote ikidai kuwa na kichwa kimoja, Kristo. Hii ni picha gani? Au mnyama gani? Basi na tunaweza kuliita zimwi? Hakuna jina kwa sababu haijawahi kusikika katika ulimwengu wa kawaida kitu cha namna hiyo.Kina mamia ya miili na kila mwili unapingana na mingine yote, na bado kila mwili uongozwe na akili moja ya kichwa kimoja. Msitishwe, kamwe hamtaona kiumbe wa namna hiyo katika ulimwengu wa kawaida wa wanyama. Lakini unaweza kuona mamia ya miili inayo pingana katika ulimwengu wa kidini, kila mmoja likidai kuwa Kristo ndiye kichwa chao. Hakika, mtu ana macho ambayo hawezi kuona kwayo na masikio, ambayo hawezi kusikia kwayo kwa kulipokea jambo hili bila busara katika ulimwengu wa kidini, huku akijua kwamba halina mantiki hata katika ulimwengu wa kawaida.

G. Muungano na umoja wa watu wa Mungu unafundishwa zaidi katika Sala ya Kristo kwa Baba. Hebu jifunze kwa muda: "*Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma*" (Yohana 17:20–21). Yesu aliomba kwamba wote wanaoamini juu yake waweze kuwa pamoja. Ombi hili ni kutaka kukemea uwingi wa makanisa. Tunajua kwamba Yesu hakuomba kwa ajili ya umoja na kisha kugeuka na kuanzisha makanisa mengi kujenga mgawanyiko. Ubadilishaji huo utakuwa giza na kazi ya unafiki. Kila wakati mtu anaposema kwamba Yesu ni mwanzilishi wa makanisa mengi, mafundisho mbalimbali ya madhehebu na mgawanyiko, humtuhumu Bwana kwa kazi ya unafiki. Ni sawa na kusema kwamba Yesu hakuwa mkweli wala mwaminifu alipomwendea Baba yake kwa sala kwa ajili ya umoja. Ni mashtaka dhidi ya usafi na uadilifu wa Mkombozi wetu. Siwezi kukubaliana na

kuelewa ikiwa ukitolewa mtazamo wa namna hiyo kwa Mwokozi wangu.

Watu wengi wameomba kwaajili ya (wakikubaliana na) mgawanyiko. Au ni mara ngapi tumeona wahubiri wakipiga magoti wakisikika wakimshukuru Mungu kwa kuwepo makanisa mengi ambapo watu watatwaa  moja ya lile walilolichagua. Yesu hakuomba kwa njia hii. Hivyo wengi wamegeukia mbali na roho ya Kristo.

## 2. Wingi wa makanisa


Ndiyo, Biblia inasema "*...Makanisa yote ya Kristo ...*" (Warumi 16:16) na *"...makanisa saba yaliyoko Asia..."* (Ufunuo 1:4). Neno makanisa hapa limetumika kwa maana ya makusanyiko (kusanyiko la pamoja la Wakristo, wale ambao wameitwa kutoka dhambini ili kumtumikia Kristo (Wakolosai 1:13-14). Hata leo neno limetumika hivi. Tunaongelea Kanisa la Kristo katika nchi, lakini yote ni sawa, kwa alama moja ya utambulisho. Tunataja idadi ya makanisa saba au idadi yoyote katika eneo fulani kama vile Roho Mtakatifu alivyozungumzia "makanisa yaliyoko

Asia”.

Hii yatosha kushawishi wenye mashaka wengi kwamba Kristo ni mwanzilishi wa kanisa moja tu. Kwa kuwa hili ni kweli kabisa kwamba Kristo ni mwasisi wakanisa moja tu, hatuna chaguzi katika swala hili na nilazima kuwa washirika wa kanisa la Kristo.

# “...Makanisa yote ya Kristo yawasalimu.”

WARUMI 16:16




**Haya hayakuwa madhehebu tofautitofauti isipokuwa makusanyiko ya Kanisa la Kristo katika miji na maeneo mbalimbali.**

“Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga **kanisa** langu;
wala milango ya kuzimu haitalishinda.
Nami nitakupa wewe funguo za **ufalme** wa mbinguni;
na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni;
na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.”
Mathayo 16:18-19

“akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya **kanisa; ambalo ndilo mwili wake**, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.”
Waefeso 1:22-23

“**Mwili mmoja**, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu.”
Waefeso 4:4

# UCHUNGUZI NA HITIMISHO

# 6

## SABABU YA SITA



## SABABU YA SITA

# Kwa sababu ni la kimaandiko kwa jina

### 1. Je, kuna lolote katika jina

Wazo kwamba hakuna lolote katika jina ni fundisho lililopata umaarufu iwe kimaandiko au kimantiki.

A. Kuna mengi katika jina mpaka Mungu akawapa Adam na Hawa. Naye *"... akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa"* (Mwanzo 5:2 ). Kuna kitu katika jina au la Mungu asingewaita.

B. Kama hakuna chochote katika jina, eleza kwa nini Mungu aligeuza jina la Abramu kuwa *" Ibrahimu"* na Sarai kuwa *"Sara"* (Mwanzo 17:5,15). Kuna mengi katika jina hivyo Mungu

1 Nya. 1:27 "na Abramu, naye ndiye Ibrahimu."

Strong's Concordance inalielezea jina defines *"Abram"* (#H87) kama "baba msifiwa" au "baba mkuu."[1]

Strong's Exhaustive Concordance inalielezea jina *"Ibrahimu"* (#H85) kama "baba wa mataifa"[2]

<u>Mwanzo 17:5-6</u> "wala jina lako hutaitwa tena Abramu, lakini

1 Strong's Hebrew: 87. אַבְרָם (Abram). biblehub.com/hebrew/87.htm.
2 Strong's Hebrew: 85. אַבְרָהָם (Abraham). biblehub.com/hebrew/85.htm.

jina lako litakuwa Ibrahimu, kwani nimekuweka uwe baba wa mataifa mengi. (6) Nitakufanya uwe na uzao mwingi sana, nami nitakufanya kuwa mataifa, na wafalme watatoka kwako."

Warumi 4:11,16,17 (11) "Naye aliipokea dalili hii ya kutahiriwa, muhuri ya ile haki ya imani aliyokuwa nayo kabla hajatahiriwa; apate kuwa **baba yao wote waaminio**, ijapokuwa hawakutahiriwa, ili na wao pia wahesabiwe haki;"

(16) "Kwa hiyo ilitoka katika imani, iwe kwa njia ya neema, ili kwamba ile ahadi iwe imara kwa wazao wote; si kwa wale wa torati tu, ila na kwa wale wa imani ya Ibrahimu; aliye **baba yetu sisi sote;** (17) (kama ilivyoandikwa, Nimekuweka kuwa **baba wa mataifa mengi**); mbele zake yeye aliyemwamini, yaani Mungu, mwenye kuwahuisha wafu, ayatajaye yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako."

Brown-Driver-Briggs inalirejea jina *"Sarai"* (#H8297) kama "...jina la mlima tasa (kame)"[3]

Terry Varner, muhubiri wa Injili, anachangia juu ya kubadilika kwa jina hili na kusema "Inaaminiwa kwamba Sarai lilikuwa ni jina la mlima tasa(mkame), na hili likafungamanishwa pamoja na utasa wake"[4]

Strong Concordance huelezea jina *"Sara"* (#H8283), "ni jina ya kike, kama "Binti mfalme"[5]

Strong Concordance (#H8282), Mzizi wa nomino unaelezea kwamba ni "Binti mfalme, mwanamke mwenye kuheshimika." Strong's Exhaustive Concordance inaelezea "Uanawake wa Sar" inalielielezea hili kama "Mwanamke mweshimiwa"[6]

---

3 Strong's Hebrew: 8297. שָׂרָי (SARAY). biblehub.com/hebrew/8297.htm.

4 A Homiletic Commentary on the Book of Genesis, by Garland Elkins and Thomas B. Warren, Getwell Church of Christ, 1985, p. 206.

5 Strong's Hebrew: 8283. שָׂרָה (SARAH). biblehub.com/hebrew/8283.htm.

6 Strong's Hebrew: 8282. שָׂרַת (SARAH). biblehub.com/hebrew/8282.htm.

"Kwa kweli, *'Sara'* ni mbadala tu wa kuandika *'Sarai'*, lenye maana ya 'Binti mfalme'."[7]

"Makala ya mtandaoni inayohusiana na mada hii inalielezea jina Sara kama 'binti mfalme wa wengi."[8]

Mwanzo 17:15-16 "Mungu akamwambia Ibrahimu, Sarai mkeo, hutamwita jina lake Sarai, kwa kuwa jina lake litakuwa Sara. (16) Nami nitambariki, na tena nitakupa mwana kwake, naam, nitambariki, naye atakuwa mama wa mataifa, na wafalme wa kabila za watu watatoka kwake."

---

7 Grasham, William Wesley. Genesis 1-22. Truth for Today Commentary. Resource Publications, 2014. Pg. 487

8 Various Contributors. "What Is the Significance of Changing the Names of ABRAM to Abraham and SARAI to Sarah?" Christianity Stack Exchange, 1 Aug. 2013, christianity.stackexchange.com/questions/15116/what-is-the-significance-of-changing-the-names-of-abram-to-abraham-and-sarai-to.

alibadilisha majina hayo.

C. Tena, kuna umuhimu sana katika majina hata Mungu alibadilisha jina la Yakobo kuwa *"Israeli"* (Mwanzo 32:27-28). Kwa kusema kwamba hakuna chochote katika jina ni kutafakari juu ya hekima ya Mungu na kumshtaki kwa kufanya matendo ya upumbavu yasio na maana.

D. Paulo alilaani majina ya binadamu na mgawanyiko kwa kuuliza, *"Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo?"* (1 Wakorintho 1:13). Kwa nini basi kulitumia jina la Paulo au jina la mtu mwingine? "*Nashukuru, kwa sababu sikumbatiza mtu kwenu, ila*

*Krispo na Gayo* (1 Wakorintho 1: 14) – si kwamba alipunguza thamani ya ubatizo au kutoa mhimu wake – "*mtu asije akasema kwamba mlibatizwa kwa jina langu*" (1 Wakorintho 1:15). Kama hakuna chochote katika majina kwanini Paulo alikemea majina ya kibinadamu?

E. Jina lina maana sana ndio maana mtu huita mbwa wake "Chui", "Simba", "Shetani" au "Kali"; punda wao "Muasi" au "Msumbufu"; na watoto wao, "Yakobo" na "Yohana." Kama hakuna chochote katika jina, kwa nini tusibadili mfumo na kuwaita watoto "Chui", "Mbwa" au "Shetani" ?

F. Kama bado una shaka kwamba hakuna kitu katika jina, tuseme wewe umwite Raia safi jina kama "Yuda", "Msaliti", "Mhuni" au "mtu mwongo" au mwite raia mwema "mhalifu," na haitakuchukua muda kujifunza kuwa, baada ya yote, kuna kitu katika jina.

## 2. Namna kanisa lilivyoitwa

Kanisa halina jina maalum, lakini linatajwa kwa majina kadhaa muhimu ili kulikumbuka. Linaitwa:

A. *"Kanisa langu"* (Mathayo 16:18). Yesu

alisema hivyo; hivyo ni kanisa la Kristo.

B. *"Kanisa"* (Matendo 8:1). Neno *"kanisa"* linatokana na neno la Kiyunani "ekklesia", kwa maana ya kundi la watu walioitwa kutoka dhambini. Bwana anakundi hilo moja tu, linaitwa; *"kanisa".*

C. *"Kanisa la Mungu"* (1 Wakorintho 1:2). Hii inaonyesha umiliki. Kwa mfano, nyumba ya Mheshimiwa Brown ni nyumba mali ya Bw. Brown.

D. *"Makanisa ya Kristo"* (Warumi 16:16). Mwandishi anazungumza kuhusu makusanyiko mbalimbali. Hili linadhihirisha kuwa ni mali ya Kristo.

E. *"Mwili wa Kristo"* (Waefeso 4:12). Mwili ambao ni mali ya Kristo.

F. *"Kanisa la Mungu aliye hai"* (1 Timotheo 3:15). Inaonesha umiliki.

G. *"Kanisa la mzaliwa wa kwanza"* (Waebrania 12:23). Kanisa la wale ambao walipokea Injili ya Kristo kwanza - mzaliwa wa kwanza, malimbuko.

Washirika wote wa makanisa ya Kristo huzungumzia kanisa kama suala

la ki-maandiko. Vipi kuhusu makundi mengine? Unaweza kuona mwenyewe kwa kuangalia mabango au alama ya nyumba za makutano yao, utaona majina yasiyopatikana katika Biblia. Ni ajabu kwamba watu ambao wanadai kuwa wanadini kuvaa majina au vyeo ambavyo ni vya kigeni katika Biblia. Je, hii sio kutokumheshimu Mungu, Kristo na Biblia?

**3. Namna washirika wake walivyoitwa.**
Tunaona kwamba washirika walivaa majina kadhaa tofauti na muhimu, yaani:

A. *"Wanafunzi"* (Matendo 20:7). Hii ina maana wanafunzi au wafuasi. Ni msamiati wa kawaida lakini unahitaji kupewa sifa yake ili kujua ni wanafunzi wafuasi wa nani; Tunasoma juu ya wanafunzi wa Yohana (Mathayo 9:14), wafuasi wa Mafarisayo (Marko 2:18), na wafuasi wa Musa (Yohana 9:28), kama vile wanafunzi wa Kristo.

B. *"Watakatifu"* (1 Wakorintho 1:2). Waliitwa hivi kwa sababu walikuwa wameokolewa kutoka dhambi za zamani, walikuwa watakatifu katika maisha, na walitakaswa (tengwa) na

Injili ya Kristo.

C. *“Wapenzi wa Mungu”* (Warumi 1:7). Mpendwa wa Mungu.

D. *“Ndugu”* (1 Wakorintho 15:6). Inaonyesha uhusiano wao kwa kila mmoja. Watu wanaweza kuwa ndugu katika mwili, katika klabu, na katika amri hata bila kuwa ndugu katika Kristo lakini wao walikuwa ni ndugu katika Kristo.

E. *“Wana wa Mungu”* (Warumi 8:14). Wao waliitwa hivi katika mtazamo wa uhusiano wao na Mungu.

F. *“Watoto wa Mungu”* (1 Yohana 3:1). Inaonesha uhusiano na Mungu.

G. *“Warithi wa Mungu”* (Warumi 8:17). Hii inaonyesha kwamba watarithi kutoka kwa Mungu.

H. *“Mtukufu kuhani”* au “kuhani” (1 Petro 2:9). Kila Mkristo ni kuhani kwa kuwa “anaweza kutolea dhabihu za kiroho zenye kumpendeza Mungu kwa njia ya Yesu Kristo,” kuhani mkuu (1 Petro 2:5; Waebrania 8:1–2).

I. *“Wakristo”* (Matendo 11:26). Hili ni jina (nomino) la pekee na wala

halihitaji maelezo zaidi kulifafanua. Jina linaonyesha uhusiano wa mtu aliyeokolewa kwa Kristo.

(1) Baadhi wamejaribu kupunguza umuhimu wa jina hili, wakisema kuwa lilitumika katika kudhihaki. Lakini jina hili lilitolewa na mamlaka ya Mungu. Isaya alitabiri: *"Na mataifa wataiona haki yako, na wafalme wote watauona utukufu wako; nawe utaitwa jina jipya, litakalotajwa na kinywa cha BWANA"* (Isaya 62:2). Hawakupaswa kupewa jina jipya mpaka Wamataifa au walipoiona haki ya Mungu. Katika Matendo 10 tunasoma juu ya uongofu wa watu wa mataifa; Kornelio na nyumba yake. Katika sura inayofuata (Matendo 11:26) tunasoma, *"...wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia"* Hili lilikuwa jina jipya na walipewa baada ya watu wa mataifa kuona utukufu wa Mungu. Kama hili si jina jipya ambalo lilipaswa kutolewa na Bwana, basi tuambie ni lipi tafadhali.

(2) Baada ya Paulo kumhubiria Mfalme Agripa mfalme akasema, *"...Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo"* (Matendo 26:28). Hivi ndivyo Paulo alivyojaribu kumfanya kila mtu kufanyika na kuwa "Mkristo". Msomaji, Roho Mtakatifu hataki wewe kuwa kitu kingine chochote!

(3) Petro anasema, *"Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo"* (1 Petro 4:16). Hatuwezi kumtukuza Mungu katika jina hili kwa kuvaa majina ya watu wengine. Hii ni amri chanya na kila anayeiasi ana hatia ya dhambi.

(4) Kuna majina mengine mengi chini ya mbingu na miongoni mwa watu, lakini soma Matendo 4:12: *"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."* Jina gani? Yesu Kristo (Matendo 4:10). Ni onyo kubwa! Je, uko tayari kuliadhimisha?

## 4. Wakristo tu

Nina hakika kwamba tunapaswa kuwa na wazee (neno la Kiyunani *presbuteros*) ambao ni Maaskofu wa kutawala na kusimamia katika makutano, lakini mimi si Mpresbiteri (TPC); Ni kweli kwamba inahitajika kuzamisha kufanya ubatizo, lakini mimi si Mbaptisti; Ni kweli Wakristo wanapaswa kujua kuhusu siku ya Pentekoste lakini mimi si Mpentekoste (Pentecostal Holiness: PHM); Ninajua kuhusu Sabato, lakini mimi si Msabato; Ni kweli kwamba kanisa lapaswa kuwa "mahali pote" (yaani kwa Kiyunani "*katholikos*"), lakini mimi si Mkatoliki. Kwa sababu tu naamini au nafahamu kitu (jambo) ambacho kipo katika Biblia haina maana kwamba nijiite kwa jina lake au kwa kitu hicho. Kama tungejiita kwa majina ya vitu hivyo basi tungeitwa Mpresbiteriani-Mbaptisti-Mpentekoste-Msabato-Mkatoliki-(na kadhalika)-Mkristo. Hayo yote si ya lazima. Tunaona katika Biblia kwamba wafuasi waliitwa Wakristo tu. Mtu anaweza kuuliza, "Je, wewe ni Mkristo?" Baada ya kujibiwa jibu "ndiyo," anaweza kuuliza "Je, wewe ni Mkristo gani?" Mara nyingi hili hujibiwa kutokana na jina la madhehebu yake. Kwa kuwa sote tunafuata Biblia moja. Kwa nini sote tusiwe kitu kimoja? Tunapaswa

kuwa Wakristo tu bila kuongezea kuwa wewe ni Mkristo gani. Ninatakiwa kuifuata Biblia na kuwa Mkristo tu.

**5. Ushuhuda wa Spurgeon na Luther**

A. Sikiliza lugha ya Charles Spurgeon, Mhubiri wa kibaptisti aliyewahi kuishi, mwenye kipaji na kufahamika zaidi: “Nasema juu ya jina Mbaptisti basi na life, lakini jina la Kristo lidumu milele. Nina tumaini na shauku katika siku ambayo hakutakuwa na maisha ya kibaptisti. Natumaini yatapotea hivi karibuni. Natarajia jina Mbaptisti litatoweka hivi karibuni; hivyo basi jina la Kristo lidumu milele” - *Spurgeon Memorial Library, Vol 1, p.168.*

B. Sikilizeni maneno ya Martin Luther, mtu ambaye jina lake latukuzwa na wengi; “Naomba mliache jina langu, na kutojiita Walutheri, bali Wakristo. Luther ni nani? Mafundisho yangu si yangu. Mimi sikusulibiwa kwa ajili ya yeyote. Mtakatifu Paulo asingeweza kuruhusu yeyote kujiita jina kwa kumwenzi Paulo, wala Petro, lakini kwa Kristo. Namna gani inanistahili mimi mwenye huzuni na dhaifu kama mfuko

wa taka au majivu kutoa jina langu kwa wana wa Mungu? Komeni, wapenzi wangu kushikamana na majina haya tofauti ya kivyama; mbali na yote; na tujiite Wakristo tu kwa jina lake Yeye mwenyewe ambaye mafundisho yetu huja kutoka kwake". *– Maisha ya Luther, na Stork, ukurasa. 289.*

Hivyo tunaona kwamba katika kuvaa majina ya binadamu, kumemchukiza si tu Mungu bali pia yule wanayejaribu kumtukuza.

"**Mawazo mwongozo katika hitimisho**" - *(Syllogism)* Ushindani – Ni aina ya hoja ya kimantiki ambayo hutumika kuhitimisha hoja (ni kitendo cha kutoa sababu kutoka kwenye taarifa 'kauli' moja au zaidi ile kufikia hitimisho la kimantiki)

https://en.wikipedia.org/wiki/Deductive_reasoning

https://en.wikipedia.org/wiki/Syllogism

Ni aina ya hoja ambayo hitimisho lake hutoka katika majadiliano ya pande mbili (kauli). Pamoja na kutoa majadiliano ya pande mbili lakini sio katika hitimisho linaloweza kuwa batili (hoja isiyofungamana au isiyo ya kweli).

https://www.lexico.com/definition/syllogism

**6. Mawazo mwongozo katika hitimisho**
Labda itakuwa sahihi na busara kama tutaweka chini baadhi ya mawazo katika mfumo maalumu wa mwongozo na kisha kufanya hitimisho:

**1. Wazo la kwanza:**

1. Biblia inalaani majina ya Kibinadamu (1 Wakorintho 1:12-13).

2. Jina "Walutheri" (KKKT) ni jina la kibinadamu.

3. Kwa hiyo, jina "la Kilutheri" (KKKT) lipo chini ya hatia ya kutumia majina ya kibinadamu.

**2. Wazo la pili:**

1. Biblia hufundisha kwamba majina ya kichama ni ya kidunia (1 Wakorintho 3:3-4).

2. Jina "Wamethodisti" ni jina la kichama.

3. Kwa hiyo jina "Wamethodisti" ni jina la kidunia.

**3. Wazo la tatu**

1. *"Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la*

*Kristo"* (Warumi 10:17).

2. Jina "Moraviani" halipo katika neno la Mungu.

3. Kwa hiyo, jina la "Moraviani" si la imani.

**4. Wazo la nne**

1. Kazi za dini na zifanyike katika jina la Bwana (Wakolosai 3:17).

2. Waefatha hufanya kazi za kidini kwa jina la "Efatha".

3. Kwa hiyo, Waefatha wako katika hatia ya makosa.

**5. Wazo la tano**

1. Watu wameamriwa kumtukuza Mungu katika jina *"Mkristo"* (1 Petro 4:16).

2. Wakatoliki hujaribu kumtukuza Mungu katika jina "Katoliki".

3. Kwa hiyo, Wakatoliki wapo katika uasi kwa amri ya Mungu.

**6. Wazo la sita**

1. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu

walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo (Matendo 4:10,12).

2. Jina “Baptisti” ni jina jingine mbali na la Kristo.

3. Kwa hiyo, hakuna wokovu katika jina “Baptisti”.

Majina katika uwanja huo yanatumika kama mifano lakini kuna majina mengi mengine ambayo yangeweza kuchambuliwa katika mwongozo wa hitimisho kama huo na isingekuwa tofauti. Kama mawazo hayo madogo na makubwa ni kweli - na ni kweli basi hitimisho ni la kweli pia. Tunawasihi watu wote wema wa dunia kukataa majina yote ya kibinadamu, yenye kuleta mgawanyiko na sio ya kimaandiko. Maombi yetu ni kufikia mafanikio; maelfu ya watu sasa wanaachana na yasiyo kimaandiko na kuambatana na Maandiko.

**7. Vyeo**

Muda mrefu umepita tangu Wayahudi kupotosha hotuba zao kwa kutumia *“nusu kwa lugha ya Ashdodi”* (Nehemia 13:23-24). Tuzungumze kwa mfano,

tuna mengi ya mfano wa lugha ya Ashdodi katika dunia ya leo. Majina mengi tu ya kujiinua sasa yakitumika kwa kupingana na mafundisho ya Biblia.

A. "Reverend." Neno Reverend hupatikana mara moja tu katika tafsiri ya Biblia ya Kiingereza likimzungumzia Mungu (Zaburi 111:9) na kamwe halipatikani katika Biblia ya Kiswahili; Ingawa hupatikana mara nyingi zaidi katika lugha ya asili. Lakini halitumiki kama cheo kwa watu. Kwa mtu kutumia hili kama cheo kwake wakati Roho Mtakatifu kamwe hakulitumia neno hili ambayo litawaweka katika hatia ya kupotosha neno. Hakuna palipotajwa katika maandiko; "Reverend Paulo," "Reverend Yakobo" na "Mwenye Haki Reverend Petro." Walijiangalia kama viumbe dhaifu, wanaohitaji msaada wa Mungu; *"... nisione fahari juu ya kitu cho chote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo..."* (Wagalatia 6:14). Baadhi ya wahubiri humtaja "Paulo" bila kutumia cheo, "Yakobo" bila kutumia cheo, "Yohana" bila kutumia cheo, na "Yesu" bila kutumia cheo,

lakini kujiita wenyewe na wengine kama “Reverend”. Hili lingechekesha kama sio kutisha. Hata Yesu, wakati alipoishi katika mwili duniani alikataa jina *“Mwema”* (Mathayo 19:16-17). Paulo alianza baadhi ya barua zake katika maneno haya: *“Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu...”* (Warumi 1:1). Paulo amejitambulisha kama “mtumishi” au “mtumwa” (Wagalatia 1:10). Paulo alimwelezea mtenda kazi mwingine katika ufalme kama “mtumishi” (1 Timotheo 4:6). Paulo pia anamwelezea Timotheo kama “mtumishi” (1 Wathesalonike 3:2). Lakini wahubiri wengi wasioguswa leo hujipachika vyeo vya juu iwezekanavyo, katika kujikweza na kujitukuza. Upinzani wa namna gani huu, majina hayo ya hali ya juu yanatokana na hali ya kutaka kujikweza. Tunakumbushwa na maneno muhimu ya Yesu; *“Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu; na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu”* (Mathayo 20:26-27).

B. “Mchungaji.” Mtumishi au mwinjilisti wa kanisa hawi mchungaji isipokuwa kwa kuchaguliwa na kanisa *“kazi ya askofu”* (1 Timotheo 3:1), mzee, au mwangalizi. Agano Jipya linatoa mwongozo wa wingi wa maaskofu, waangalizi, wazee au wachungaji katika kusanyiko hilo (Matendo 14:23). Wanatakiwa kufanya kazi ya kichungaji katika kulinda kundi. Maneno haya si vyeo, lakini ni majina kama, “mwalimu,” “mkulima” na “seremala”.

C. “Baba.” Neno Hili mara nyingi hutumika kama jina lakidini katika upinzani wa moja kwa moja na mafundisho ya Kristo; *“Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni”* (Mathayo 23:9). Hii ni katika kuzungumzia matumizi ya kidini kuliko mahusiano ya kimwili, kwa sababu mara nyingi Roho Mtakatifu hutumia neno “baba” akizungumza juu ya wazazi wa mtu. Si ajabu kwamba mamilioni hutumia jina hilo kama cheo na kama vile ni vyema wakati ni haramu na imekatazwa na Kristo?

Kanisa la Kristo ni la kimaandiko

kwa jina na hata lugha. Hakuna mtu anayeweza kukana jambo hilo. Ni imani na utendaji wa kanisa la kristo "kuita vitu vya kibiblia majina ya kibiblia." Paulo alimhimiza Timotheo kufanya hivyo, akisema, *"Shika kielelezo cha maneno yenye uzima..."* (2 Timotheo 1:13). Tunapaswa kuepuka tabia maarufu za kutumia vyeo vya kujipandikiza, lakini afadhali kufuata ushauri huu; *"Tafadhali, nisiupendelee uso wa mtu; Wala sitajipendekeza kwa mtu ye yote. Kwani mimi sijui kujipendekeza; Au Muumba wangu angeniondoa kwa upesi"* (Ayubu 32:21-22).

# 7

## SABABU YA SABA



# Kwa sababu muundo wake ni wa kimaandiko

## SABABU YA SABA

# Kwa sababu muundo wake ni wa kimaandiko

### 1. Mifumo ya uongozi wa kiimani

Madhehebu yanatawaliwa na mifumo na serikali zao za kidini. Wamempuuza Mkuu wa kanisa na kuona wana haki ya kuwa na serikali binafsi ya kidini. Hukiri kwa vinywa vyao kwamba Kristo ana "mamlaka yote", lakini mioyo yao ipo mbali na hilo na ni kujiwekea demokrasia yao na aina za serikali. Kwa hiyo, tunasikia mengi kuhusu "Sinodi" "makasisi", "Halmashauri", "makanisa kwa ujumla" na "makongamano". Kutokana na maamuzi ya makundi mbalimbali ya serikali za kidini zitawalazo, wanaunda taratibu za kibinadamu ambazo zinaleta maelekezo ya muundo wa makundi haya ya kidini yaliyoundwa na wanadamu au madhehebu.

A. Bila shaka uwezo huu wa kutunga sheria kamwe hajapewa mtu wala kikundi chochote cha wasio vuviwa. Hakuna kundi la watu lenye mamlaka

MUUNDO

kutoka kwenye Biblia kuamua ni mara ngapi kwa mwaka karamu ya Bwana iliwe,kubadili tendo la ubatizo, kuweka kando ubatizo kama hali ya wokovu, au kufanya mabadiliko yoyote katika utaratibu wa Mungu . Mtu yeyote ambaye hudhani ana mamlaka ya kubadili serikali ya kanisa au sheria iliyotolewa na mitume huasi mbele ya Kristo, kichwa na mamlaka ya juu kabisa. Mapenzi ya Kristo ni sheria na uasi dhidi yake ni uhaini.

B. Kukataa mamlaka kuu ya Kristo hutokana na kukua kwa marekebisho. Badiliko moja husababisha jingine; na hatimaye viongozi wa makundi ya dini huinuka, mabadiliko katika muundo husababisha mabadiliko katika sheria; mabadiliko haya katika sheria humwondoa Kristo kama Mfalme na kutawaza mamlaka ya kibinadamu kiutawala na

kiuongozi.

**2. Ufalme**

A.Kanisa la Kristo ni Ufalme. Yeye ni kichwa na mkuu. *“Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote”* (Wakolosai 1:18). Msikilize Paulo tena: *“akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote”*(Waefeso 1:22-23). Katika tukio la kubadilika (kugeuka kwa sura yake) Mungu alisema, *“…Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye”*(Mathayo 17:5). Muda mfupi kabla Kristo hajapaa kuketi mkono wa kuume wa Mungu, alisema; *“... Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani”*(Mathayo 28:18). Kristo ana mamlaka yote; basi mtu hana kabisa. Kristo si kukomesha *“utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu”* mpaka mwisho utakapofika (1 Wakorintho 15:24).

B. Yesu aliwaahidi mitume kumtuma kwao Roho Mtakatifu, ambaye angewafundisha mambo yote, na kuwakumbusha mambo yote (Yohana 14:26). Mitume walikuwa mashahidi wa Roho Mtakatifu akimshuhudia Kristo (Yohana 15:26-27). Mafundisho na ushahidi wa mitume,utadhihirishwa na kukubalika mbinguni, kwa maana *"Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni"* (Mathayo 16:19). Kristo kamwe hakutoa mamlaka haya isipokuwa kwa mitume. Kwa watu wanaoishi baada ya wakati wa mitume kuwa na mamlaka katika mabaraza, dayosisi, au sinodi ni kumdhihaki Mfalme juu ya kiti chake cha enzi.

## 3. Kujitegemea au utawala binafsi wa kanisa

A. Katika kuzungungumzia utawala binafsi wa kanisa tuna maana ya kujitegemea kwa kanisa mahalia (kusanyiko). Kujitegemea kunaelezwa kama "haki ya kujitawala; hali ya

kujiongoza; kundi huru." Katika karne ya kwanza kila kusanyiko lilikuwa hivyo. Kila kusanyiko lilikuwa huru pasipo kutegemea kusanyiko jingine (Hata hivyo, makusanyiko yote yanapaswa kushirikiana katika Kristo). Hakukuwa na mamlaka ya kusanyiko moja juu ya jingine. Kanisa la karne ya kwanza huko Rumi au Yerusalemu halikuwa na mamlaka juu ya makanisa au makusanyiko mengine. Watu nje ya kusanyiko hilo hawakuwa na haki ya kuwa na mamlaka na nguvu ndani ya kusanyiko jingine. Wazee na mashemasi katika kusanyiko moja hawakuwa na mamlaka ya kutawala juu ya wazee na mashemasi katika kusanyiko jingine. Kila kusanyiko (kanisa) lilikuwa huru, chini ya mafundisho ya Kristo na mitume, kujiendesha, kazi zake, na kusimamia mambo yake lenyewe. Hakukuwa na mfumo wa utawala mkubwa kuliko kanisa mahalia. Makusanyiko yote yalikuwa na kichwa kimoja, msingi mmoja, na utume mmoja, kuhubiri Injili moja; makusanyiko mahalia hufanya mwili mmoja duniani kote. Lakini kila kusanyiko lilikuwa huru katika kazi na

mamlaka yake.

B. "Busara ya Mungu huonekana katika utaratibu wa makusanyiko yake. Kama moja litapotoshwa katika mafundisho au kuathirika na mazoea ya uovu, makusanyiko mengine hayawezi kuharibika. Kama mfarakano utaibuka katika moja, hauwezi kuenea kwa wengine; kama mmoja utapotezwa, wengine hawawezi kuanguka nao. Kama dirisha limeundwa na pingili moja kubwa, kuvunjika kutaliangusha lote, lakini kama dirisha limeundwa kwa pingili tofauti kuvunjika kwa kioo katika pingili moja hakuwezi kulivunja lote. Uhuru wa makanisa ni ulinzi kwa ajili ya kila mmoja." - *H. Leo Boles, Gospel Advocate, Mwinjilisti, Februari 15, 1940.*

C. Hata hivyo muundo huu rahisi umeshindwa kuwaridhisha wengi. Walifanya mabadiliko ya muundo wa kanisa ili kwamba watu mbalimbali wawe na mamlaka makubwa, na uwezo mkubwa kuliko vile Mungu alivyokusudia kuwapa. Katika historia kwa mara ya kwanza tunaona watu wakiondoka katika ukweli kwa kubadili

muundo wa utawala wa kanisa la Kristo.

**4. Wazee**

A. Roho Mtakatifu hufundisha kwamba wazee, maaskofu, waangalizi au wachungaji huwekwa wakfu katika kila kusanyiko la kanisa moja (Tito

**Maneno matatu ya Kiyunani yaliyotafsiriwa katika Kiswahili yanayotupa maneno mbalimbali ya Kiswahili. Haya maneno yanawakilisha nafasi (kazi) moja.**

1. (neno la Kiyunani episkope / *episcopos*)
"Askofu" (1 Timotheo 3:1; Tito 1:7).

"waangalizi" (Matendo 20:28).

2. (neno la Kiyunani *presbuteros/presbuterion*)

"Wazee" (Matendo 20:17; Matendo 14:23; 1 Petro 5:1; Yakobo 5:14; Tito 1:5; 1 Timotheo 5:17; 1 Timotheo 4:14).

3. (neno la Kiyunani *poimen / poimaino*)

"Mchungaji" (Waefeso 4:11; 1 Petro 5:2).

"kulilisha" (Matendo 20:28).

**Tito 1:5, 7 (5)**

"Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee (***presbyterous***) katika kila mji kama vile nilivyokuamuru;" (7) "Maana imempasa askofu (***episkopon***) awe mtu ..."

**Matendo 20:17,28**

(17) "Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee (***presbyterous***) wa kanisa." (28) "Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi (***episkopous***) ndani yake, mpate kulilisha (***poimainein***) kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe."

**1 Petro 5:1-2**

"Nawasihi wazee (***presbyterous***) walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye; lichungeni (***poimanate***) kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia (***episkopountes***), si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo."

1:5). Katika Matendo 20:17 tunasoma kwamba Paulo *"akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa"*, akizungumza na kundi hili Paulo alitangaza kwamba walikuwa "waangalizi" (SUV, Matendo 20:28). Wanaume ambao walifanya kazi hii pia wanatajwa kama wachungaji (Waefeso 4:11). Hivyo katika kila kusanyiko inapaswa kuwa na wazee (wachungaji, maaskofu) wawili au zaidi na sio makusanyiko zaidi ya moja kuwa na mzee mmoja (askofu mmoja). Katika mfumo wa madhehebu watu wamesahau kabisa mfumo huu wa kiroho na kufanya makusanyiko mengi chini ya askofu mmoja.

B. Ni wajibu wa Maaskofu;

(1) *"Jitunzeni"*

(a) *"nafsi zenu"*

(b) *"kundi lote"*

(2) *"mpate kulilisha kanisa lake Mungu"* (Matendo 20:28);

(3) *"kuwasaidia wanyonge"* (Matendo 20:35);

(4) *"akilishika lile neno la imani"* na

(5) *"kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima"* (Tito 1:9);

(6) *"waonyeni wale wasiokaa kwa utaratibu"*;

(7) *"watieni moyo walio dhaifu";*

(8) *"watieni nguvu wanyonge"* (1 Wathesolonike 5:14);

(9) *"lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu"* ;

(10) *"kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao"*;

(11) *"kujifanya vielelezo kwa lile kundi."* (1 Petro 5:2-3);

(12) kutembelea wagonjwa (Yakobo 5:14);

(13) *"maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu"* (Waebrania 13:17).

Majukumu yaliyotajwa hapo juu yamewekwa kwao na Bwana. Kazi hizi zisipofanywa, ushirika huharibiwa,

hakuna elekezo katika Biblia kwamba wazee wana mamlaka ya Mungu kubatilisha au kurekebisha sheria ya Kristo. Wana mamlaka ya kutekeleza sheria ya Kristo tu, na si kwa kutunga sheria kwa serikali na madai yao. Wana heri kusanyiko ambalo wana wazee ambao hutekeleza majukumu yaliyotajwa.

C. Sifa za Askofu ni kama zifuatazo: Basi imempasa askofu awe

(1) *"mtu asiyelaumika,"*

(2) *"mume wa mke mmoja,"*

(3) *"mwenye kiasi na busara,"*

(3) *"mtu wa utaratibu,"*

(4) *"mkaribishaji, ajuaye kufundisha,"*

(5) *"si mtu wa kuzoelea ulevi,"*

(6) *"si mpiga watu; bali awe mpole,"*

(7) *"si mtu wa "kujadiliana", wala asiwe mwenye kupenda fedha,"*

(8) *"mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu, (yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake*

*mwenyewe, atalitunzaje Kanisa la Mungu?)"*

(9) *"Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi,"*

(10) *"Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi,"* (1 Timotheo 3:2-7);

(11) *"ikiwa mtu hakushitakiwa neno,"*

(12) *"Ana watoto waaminio,"*

(13) *"wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii,"*

(14) *"Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno,"*

(15) *"wakili wa MUNGU,"*

(16) *"asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake,"*

(17) *"asiwe mwepesi wa hasira,asiwe mlevi wala mgomvi,"*

(18) *"asiwe mpenda mapato ya aibu, bali awe mkaribishaji,"*

(19) *"mpenda wema, mwenye kiasi,"*

(20) *“mwenye haki,”*

(21) *“mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake;”*

(22) *“akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa,”*

(23) *“apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga.”* (Tito 1:6–9). Ni mara nyingi tu, kazi ya askofu hutolewa kwa watu ambao hawana sifa hizi na ambao hukubali wajibu huu kwa uelewa mdogo wa majukumu yao.

D. Na kusanyiko limeamuriwa;

(1) *“...mwatambue wale wanaojitaabisha kwa ajili yenu, na kuwasimamia nyinyi katika Bwana, na kuwaonyeni;”*
(2) *“mkawastahi sana katika upendo, kwa ajili ya kazi zao. Iweni na amani ninyi kwa ninyi”* (1 Wathesolonike 5:12–13);

(3) *“Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu; hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha”* (I Tim 5:17.);

(4) *“Watiini wenye kuwaongoza, na”*

(5) *“kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua; maana isingewafaa ninyi”* (Waebrania 13:17);

(6) *“Usikubali mashitaka juu ya mzee, ila kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu”* (1 Timotheo 5:19). Ni muhimu kwa ushirika kutimiza majukumu yake juu ya wazee wake kama ilivyo muhimu kwa wazee kutimiza majukumu yao kwa ushirika/makutano.

**5. Mashemasi**

A. Majukumu ya mashemasi hayako wazi sana kama ilivyo kwa wazee, lakini bila shaka ni yale ya usaidizi na utumishi. Katika Matendo 6:1-6 tunasoma watu saba katika kanisa la Yerusalemu waliwekwa maalumu *“kuhudumu mezani.”* Kundi hili halikutambuliwa wazi au kutambulishwa katika Biblia kama mashemasi, lakini kutokana na lugha

ya asili tunajifunza kuwa walifanya kazi ya wahudumu au watumishi , neno *"shemasi"* linatumika kama watumishi au msaidizi katika kanisa. Hivyo wazee ni watawala au waangalizi katika kanisa na mashemasi ni watumishi. Inasemwa kuwa kazi ya wazee ni ya kiroho na kazi ya mashemasi ni ya kimwili, lakini matendo yao hayawezi kubanwa hivyo katika nyanja hizo tu. Hatuwezi kusema kwamba wazee kama watawala katika makutano/ ushirika hawapaswi kuhusika na mambo ya fedha, kwa maana tunasoma katika Matendo 11:29-30 juu ya michango kupelekwa kwa wazee huko Yerusalemu kwa mikono ya Barnaba na Sauli. Wala hatuwezi kusema kwamba kazi ya mashemasi ni ya kimwili tu kwa maana tunasoma juu ya Stefano na Filipo, wawili kati ya wale saba waliochaguliwa Yerusalemu, baadaye walihubiri Habari Njema kwa nguvu sana na ushawishi.

B. Wale ambao wanachaguliwa kufanya kazi hii ni lazima kuwa na sifa zifuatazo:-

(1) *"walioshuhudiwa kuwa wema,"*

(2) *“wenye kujawa na Roho,”*

(3) *“na hekima”* (Matendo 6:3);

(4) *“wawe wastahivu”*;

(5) *“si wenye kauli mbili,”*

(6) *“si watu wa kutumia mvinyo sana,”*

(7) *“si watu wanaotamani fedha ya aibu.”*

(8) *“wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa”*

(9) *“hawana hatia.”*

(10) *“Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahimilivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi,”*

(11) *“waaminifu katika mambo yote.”*


(12) *“Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja,”*

(13) *“wakiwasimamia watoto wao*


*vizuri, na nyumba zao.*” (1 Timotheo 3:8-12).

Muundo wa kanisa ni rahisi mno, lakini

mpango wa Mungu umetumiwa  vibaya sana. Kila jaribio la kuboresha mpango huu limesababisha uasi na mifumo na matendo mbalimbali ya imani ya kimadhehebu.


MUUNDO WA KANISA
YESU KRISTO
Mchungaji Mkuu
(1 Petro 5:4)
Mwangalizi wa nafsi zenu.
(1 Petro 2:25)
Uwingi (mbili au zaidi, Wafilipi 1:1) wa
Wazee
(Matendo 20:17; Tito 1:5; 1 Timotheo 4:14)
Maaskofu / Waangalizi
(1 Timotheo 3; Matendo 20:28)
Wachungaji
(1 Petro 5:2; Waefeso 4:11)
katika kila kanisa
(Matendo 14:23)
katika kila mji
(Tito 1:5)
Mchungaji
Mzee
Askofu
Mwangalizi
Shemasi
(1 Tim. 3:8-13)
Shemasi
Mhubiri
(Marko 16:16)
(2 Timotheo 4:2)
Shemasi
Shemasi
Shemasi
Shemasi
Mwinjilisti
(2 Timotheo 4:5; Waefeso 4:11)
Shemasi
Shemasi
Shemasi
Mhudumu
(Wakolosai 1:23)

# MUUNDO WA KANISA



# 8

## SABABU YA NANE



## SABABU YA NANE

# Kwa sababu lina Biblia pekee kama kiongozi cha imani, ungamo na mwongozo wake.

### 1. Sababu ya imani hii

Siwezi KAMWE kuwa mshirika katika baadhi ya mifumo ya dini ambayo ina imani ya binadamu. Hii ni imani yangu kwa sababu kadhaa, zifuatazo:

A. Katika nyakati za mitume na kwa karne tatu za kwanza Biblia ilikuwa ndio imani pekee. Kwa nini tusitumie imani hiyo hata leo? Sitaki kitabu cha mwongozo cha kidini kinachofanana na Biblia, bali nataka kuwa na Biblia yenyewe. Kwa hili kuwezekana ni lazima kutumia Biblia pekee.

B. Biblia kwa hakika hutupelekea katika kila kazi njema: Tunajua *"Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake*

*mwenyewe"* (2 Petro 1:3); na kwamba *"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; 17ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema"* (2 Timotheo 3:16–17). Roho Mtakatifu anasema kwamba Maandiko yametolewa kutupeleka katika mafundisho, kuonya, kusahihisha, mafundisho katika haki, na kwa kila kazi njema, Ndiyo! Hivyo kwa nini basi kushikilia imani za kibinadamu zenye kutofautiana na sababu za awali za Mungu kutoa Biblia? Biblia ni salama, je vipi kuhusu imani za kibinadamu? Hata wao wanaoamini katika mafundisho ya wanadamu wanakiri kwamba wana mafundisho kadhaa yenye makosa au matatizo. Kwa nini kuwa muumini wa kitu

ambacho kimetokana na binadamu na kina dosari wakati unaweza kuwa muumini wa Maandiko ya Roho yaliyo tokana na Mungu na wala hayana dosari? Hata kama viongozi wa kanisa lazima waandike fundisho la imani ambalo haliongezi au kuondoa lolote katika Biblia, lingekuwa sawa kabisa na ilivyo katika Biblia; kwa nini basi kuwa na mafundisho mawili yenye kufanana kabisa? Kutakuwa hakuna maana yoyote katika hilo. Basi si ni heri kubaki na Biblia moja?

C. Yafuatayo yaweza kutajwa kama ya Biblia pekee. “Kitabu hiki kikongwe kina mawazo ya Mungu, hali ya mtu, njia ya wokovu, adhabu ya dhambi na furaha ya waumini. Ni historia na kweli, mafundisho yake ni matakatifu, maagizo yake ni sheria, na maamuzi yake hayabadiliki.Soma ili kuwa mwenye hekima, kuamini ili kuwa salama, na uishi katika utakatifu. Kina mwanga kukuongoza, chakula kukusaidia na faraja kwa moyo wako. Ni ramani kwa wasafiri, fimbo ya mahujaji (wasafiri), dira ya baharia, upanga kwa askari, na mwongozo kwa

Mkristo. Hapa paradiso hurejeshwa, milango ya mbinguni huwekwa wazi na kuzimu kufungwa. Dhamira kuu ya Biblia ni Kristo, kuundwa kwake ni kwa faida yetu, na shabaha yake ni utukufu wa Mungu. Neno la Mungu litajaza kumbukumbu zetu, litatawala mioyo yetu, na kuyanyosha mapito yetu. Soma kwa uangalifu, mara kwa mara, pamoja na kuomba. Ni mgodi wa mali, paradiso ya utukufu na mto wa furaha. Kimetolewa kwako katika maisha, kitafunguliwa wakati wa hukumu na kukumbukwa milele. Kina husisha mamlaka ya juu, huzawadia kazi njema na kulaani wote wenye kupotosha utakatifu wake" - (Mwandishi hajulikani). Hakuna kitabu cha kidini kilichoandikwa na mwanadamu kinachoweza kufanya madai haya. Vitabu vya kidini vilivyoandikwa na wanadamu havihitajiki.

D. Kanuni za kibinadamu hurekebishwa kila mara kwa sababu ya hitilafu yake. Mwanafunzi wa imani za kibinadamu wala hajui imani na mafundisho yake yatakuwaje baada ya miaka kumi. Kanisa ambalo kwa miaka

lilifundisha kuwa watoto walizaliwa na dhambi za asili lilibadilisha imani yake miaka mitatu au minne iliyopita na kuanza kufundisha kuwa watoto hawazaliwi wakiwa na unyonge,wala udhalimu, wala dhambi. Waamini wa udhalimu huo waliitana na kubalisha udhalimu huo kuufanya sawa. Huo ni mfano mmoja tu. Imani zinaendelea kubadilika na kurekebishwa. Hii pekee huwaweka katika aibu ya udhaifu na kutokuwa kamili.

Wakati imani za kibinadamu zinaendelea kufutwa na kubadilishwa ili kuwa mpya, Biblia imeendelea kuishi na kufanya kazi. Inaishi kwa sababu haihitaji mabadiliko. Injili ya Kristo ni kamili na huzungumziwa kama; *"...sheria kamilifu iliyo ya uhuru..."* (Yakobo 1:25). Ni kamili, na laana ya hukumu i juu ya mtu yeyote au kundi la watu wanaotaka kuipotosha kwa kuihariri na kuongeza au kupunguza neno kutoka humo (Wagalatia 1:6-9): (Ufunuo 22:18-19). Neno la Mungu ni kamilifu na hajawahi kuruhusu mtu kuliingilia kwa kubadilisha. Hata nyuma katika nyakati za Musa Bwana aliagiza

*"Msiliongeze neno niwaamurulo wala msilipunguze..."* (Kumbukumbu La Torati 4:2).

E. Kanuni za kibinadamu haziwezi kutetewa. Zifuatazo ni nukuu kutokana na matendo ya Benjamin Franklin:

"Kwanza, kanuni za imani (kitabu chochote cha kiimani cha mwongozo) zenye kuwa na vitu zaidi ya Biblia hazikubaliki, kwa sababu zimeweka vitu vyake kuliko vilivyo kwenye Biblia.

Pili, kanuni za imani ambazo zina mambo machache kuliko Biblia hazikubaliki, kwa sababu zina machache kuliko yaliyomo katika Biblia.

Tatu, kanuni za imani zilizo tofauti na Biblia hazikubaliki, kwa sababu zinapingana na Biblia.

Nne, kanuni za imani ambazo zipo sawa na Biblia ni bure, kwa sababu tayari tuna Biblia.

Haya yanabeba mawazo yote. Haiwezekani kuongeza mawazo mengine zaidi. Kanuni ya imani ni lazima ama ibebe mafundisho zaidi, pungufu, tofauti, au kama kwenye Biblia kwa sababu tayari kuna Biblia

kamilifu. Wakati mtu anatangaza au kutetea kitabu chake cha kanuni ya imani, hasemi kwamba kitabu chake cha imani kina mafundisho zaidi, pungufu, tofauti, au sawa na Biblia. Kama kanuni ya imani haiwezi kutetewa katika misingi hiyo ni misingi gani basi yaweza kutetewa kwayo? Hakuna namna iwezekanayo kwa hili kutetewa.

F. Waonyeshao utii katika kanuni za imani za kibinadamu hawawezi kuitetea Biblia. Fundisho lao la imani katika kufuata kitabu chao cha kanuni ya imani kama ziada ya Biblia linaondoa nguvu yoyote katika hoja zao dhidi ya ukamilifu na utimilifu wa neno la Mungu. Wanashindwa kuonyesha imani yao kwa matendo yao (Yakobo 2:18). Kwa kweli, kwa matendo yao huonyesha ukosefu wao wa imani ndani yake. Kama mtu haifuati Biblia pekee kama kanuni yake ya imani, hawezi kufanikiwa kuilinda dhidi ya wapagani. Ni vigumu kabisa kwa mhubiri kutetea mafundisho ya Biblia wakati mafundisho yake mwenyewe yametokana na kitabu

kingine tofauti na Biblia. Mafundisho na matendo yake ya imani hayapatani. Hii yaonesha hana imani katika Biblia pekee. Mpagani aweza kusema; "Mhubiri, waweza kutueleza kwa nini una mwongozo mwingine wa kanuni ya imani tofauti na Biblia kama Biblia ni kweli? Kama Biblia ni kweli, kama usemavyo, kuwa inatupatia mafundisho, inatuonya makosa yetu, kutuongoza, na kutuadibisha katika haki, ili tupate kutenda kila tendo jema, hivyo, unawezaje kutetea na kuhalalisha kanuni yako ya imani ya kibinadamu?" Mhubiri huyo ambaye anashikilia kanuni ya imani ya kibinadamu atakuwa mwenye mkanganyiko na aibu.

Kwa zaidi ya miaka mia moja iliyopita, Robert Dale Owen wa Scotland, mkuu wa ukafiri, aliingia Marekani. Yeye alifanya kama Goliath wa Wafilisti katika zama za kale; huyo alipowatukana watu wa Mungu; akawataka wafuasi wa Kristo wapeleke mtu kushiriki naye katika malumbano na kupambana na ukweli wa Biblia. Wahubiri waliofungwa

na kanuni ya imani ya kimadhehebu wakatetemeka kwa changamoto ya sauti yake. Kwa nini? Walijua nafasi yao ilikatisha tamaa katika kujitetea! Walijua Owen angewataka kuhalalisha ukweli wa kanuni zao za imani zozote zisizo kwenye Biblia; kueleza kwa nini walijivika majina yasiyo tajwa katika Biblia na kuweka wazi kwa nini walikuwa wajumbe wa makanisa ya kigeni kwa Biblia. Walitetemeka lakini Daudi akasimama na kukubali changamoto. Hakuwa kitu kingine bali Mkristo, mshirika wa kanisa la Kristo pekee, na hakuwa na kanuni ya imani nyingine ila Biblia. Vita kwa ajili ya ukweli vilifanyika huko Cincinnati (USA), kuanzia Aprili 13, 1829, na vilidumu kwa muda wa siku nane. Bwana Owen, Goliath mwanaharamu kafiri, hakuweza kutumia silaha yake aipendayo: upayukaji wa wale wanaokiri kuamini Biblia na kuwa kinyume chake. Mpinzani wake hakuwa muumini wa madhehebu, wala hakujivika majina yasiyo katika Biblia, wala hakuwa na kununi ya imani ya kibinadamu. Kafiri akaangushwa chini. Ilikuwa ni ushindi mkubwa kwa Biblia

na Wakristo walifurahi. Mtetezi wa imani alikuwa Alexander Campbell. Mtu yeyote angeweza kusimama kinyume na kafiri kama hawangekuwa wameshikilia mafundisho yao ambayo yasingeweza kutetewa. Watu hawawezi kuitetea Biblia wakati wameweka nguvu zao kwenye kanuni za imani zilizoandikwa na watu wasiovuviwa.

G. Kanuni za imanai za kibinadamu huleta migawanyiko. Huwafanya watu wa dini kugawanyika katika vyama na madhehebu. Kila kanuni ya imani hufanya kama ukuta unaofungia ndani wafuasi wake pekee na kuwatenga wengine wote. Hizi kuta lazima kuporomoka na kuanguka kabla ya umoja kuweza kuwa ukweli. Wote lazima kwenda. Kundi moja la madhehebu haliwezi kutarajia madhehebu mengine yote kutupa kando kanuni zao za imani za kibinadamu na kufuata kanuni za imani nyingine za kibinadamu. Kama wataendelea kushikamana na kanuni ya imani ya kibinadamu basi watashikamana na waliyonayo. Ili kuungana ni lazima

kanuni za binadamu kufutwa, vikwazo vya madhehebu vitaanza kudhoofika na watu waliogawanywa watashika njia moja kuelekea umoja.

## 2. Mawazo mwongozo katika hitimisho

Hakuna shaka kwamba mgawanyiko ni dhambi. Sikiliza ujumbe wa Roho Mtakatifu: *"Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja."* (I Wakorintho 1:10). Mgawanyiko ni dhambi, ukiukaji wa amri chanya. Kanuni za imani za kibinadamu huchangia hali hii ya dhambi; Kwa hiyo, kanuni za imani za kibinadamu ni dhambi na wale ambao huzichangia hushiriki katika hatia ya dhambi hiyo.

Labda itakuwa wazi zaidi kama tutaainisha baadhi ya maeneo na kisha kufanya hitimisho.

### 1. Wazo la kwanza ("Mawazo mwongozo katika hitimisho") - *(Syllogism)*:

(1) Mgawanyiko ni dhambi (1 Wakorintho 1:10; Wakorintho 3:3)

(2) Kanuni za imani za kibinadamu ni mgawanyiko (wazo hili linalokubalika kwa uwazi kabisa)

(3) Kwa hiyo, kanuni za imani za kibinadamu ni dhambi

**2. Wazo la pili:**

(1) Ni dhambi kuenenda kwa kiwango tofauti cha kanuni ya mwongozo au sheria tofautitofauti (Wafilipi 3:16)

(2) Kanuni za imani za kibinadamu ni sheria tofauti (wazo hili linalokubalika na wote)

(3) Kwa hiyo, ni dhambi kuenenda chini ya kanuni za imani za kibinadamu.

**3. Wazo la tatu**

(1) Mgawanyiko hupelekea ukafiri/upagani. (Yohana 17:20-21)

(2) Kanuni za imani za kibinadamu hupelekea mgawanyiko (wazo hili linalokubalika na wote)

(3) Kwa hiyo, kanuni za imani za kibinadamu hupelekea ukafiri/upagani.

Njia pekee ya kupinga majumuisho haya ni kwa kukanusha aidha vipengele vidogo au vya msingi. Kama vipengele hivyo ni kweli, basi hitimisho halina shaka-hivyo hitimisho ni hakika.

# 9

## SABABU YA TISA



## SABABU YA TISA

# Kwa sababu linaamini Biblia yote ni neno la Mungu lililovuviwa

### 1. Maoni ya baadhi ya wahubiri

Katika mahubiri juu ya “Mtazamo wa kisasa wa Biblia”, yaliyofanywa na L.R.Wilson, (*Firm Foundation*, April 28, 1942) tunapata yafuatayo: “Ni mwaka jana tu Dr. McCartney, katika hotuba ya ‘Injili tukufu’, katika kipindi kiitwacho “mahubiri leo” alinukuu takwimu (kutoka kwa Betts, katika chapisho la AbingtonPress, chini ya maelezo ya “Imani ya wahubiri 700”) ambayo ilionesha matokeo yafuatayo: asilimia kumi na tatu walikataa maelezo ya Biblia ya uumbaji; asilimia thelathini na tatu hawaamini tena kama kuna shetani; Asilimia 13 walikataa fundisho la Utatu (sifa ya Uungu), asilimia 48 hawakuamini katika uumbaji wa Mungu; asilimia 33 hawaamini kwamba kuna Ibilisi; asilimia 38 hawaamini katika ufunuo kutoka kwa Mungu; asilimia 43 wanakataa uvuvio wa neno kwa neno wa Maandiko; asilimia 38 hawaamini manabii

wa Agano la Kale walikuwa na uwezo wakutabiri matukio ya siku ya usoni; asilimia 55 hawaamini biblia ni huru na haihusiani kabisa hadithi na simulizi za kutunga; asilimia 19 hukataa maelezo kuhusu Mungu kufanyika mwili; asilimia 19 hawaamini kuwa Yesu ni sawa na Mungu; asilimia 24 hukataa upatanisho wa Kristo; asilimia 12 hukataa ufufuo wa Kristo; asilimia 34 hawaamini tena katika adhabu ya baadaye kwa waovu; asilimia 33 hawaamini katika ufufuo wa mwili; asilimia 27 hawaamini kuwa Yesu atakuja tena kuwa hukumu wazima na wafu; asilimia 33 hukataa anguko la mwanadamu lililofundishwa katika kitabu cha Mwanzo; asilimia 51 hawaamini kwamba ubatizo na meza ya Bwana siyo lazima; asilimia 39 wanaona kwamba ni vizuri, kwamba watu wanapaswa kupokewa kanisani bila kujali imani zao juu ya wokovu."

A. Ni jambo la kushangaza kwamba wengi hawaamini Biblia kuwa kiongozi na mamlaka ya neno la Mungu:

hivyo, hawaamini katika kile ambacho Mungu anasema katika masomo mengi.

Wale wasioamini kuwako kwa Mungu wana msimamo zaidi kuliko Mkisasa (Modernist): Mtu ambaye haamini kwamba Mungu yupo haiamini Biblia wakati Mkisasa anaamini chochote apendacho na kukichagua.

**Usasa (Modernism):** Vuguvugu lililojumuisha fikra za kidini za kale pamoja na za kisasa. Mfikiriaji wa mambo ya kidini mwenye mabadiliko ya wastani. Walipendelea zaidi maelezo, uthibithisho, na sayansi kuliko kuamini na imani, ambayo imepelekea wengi kuikubali nadharia ya mageuko (evolution) dhidi ya maelezo yaliyo kwenye kitabu cha Mwanzo. Katika kitabu hiki, mtu aaminiye mawazo haya tutamwita Mkisasa (Modernist).

## 2. Sababu za kuamini Biblia

Zingatia; hizi ni chache kati ya sababu nyingi za kuamini Biblia:

A. Kama Biblia si kweli basi hakuna historia yenye kukubalika na kuaminika. Hakuna historia nyingine

yenye tabia na sifa za kuaminika na kutegemewa. Biblia hubeba kila alama ya ukweli. Katika kumzungumzia Kristo ilisemwa; *"Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tulililoliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya Neno la uzima"* (1 Yohana 1:1). Ushahidi sio tetesi–walimwona, walisikia, na kumgusa Kristo -na inakubalika hata kwa mtazamo na maarifa. Ukweli kwamba walisikia, walimwona na kumgusa Kristo ni mkubwa mno, kukataliwa kwa kudhani kuwa wanaweza kuwa na maono duni, kutohisi au usikivu duni, ni ujinga kuwashitaki kwa kusema uwongo au kuhoji usafi wao. Haikuwaletea faida zozote za kimwili wala kidunia kwa kutoa ushuhuda huu. Kwao tendo hilo lilikuwa ni kuwakana marafiki na familia, kukataa maisha rahisi, kukubali mateso na kifo.  Ni jambo la kiendawazimu kusema kwamba walikubali kufa kwa suala la uongo. Kamwe! hakuna mwanahistoria aliyewahi kutoa ushahidi wenye nguvu kuwazidi wao. Kama Biblia si ya kweli basi hakuna historia inayokidhi

uthibitisho wetu.

Wapi kama sio kutoka mbinguni, kwa miaka mingi tofauti na maeneo tofauti, walipozaliwa watu, wasio na ujuzi ama vipaji vya sanaa kuandika mambo yaliyo shabihiana na kukubaliana Ama kwa nini au vipi watake kutudanganya? Kukubali, maumivu yao, kutoa ushauri wao bila faida kwao na kifo kuwa malipo yao?

B. Biblia ni kitabu cha vitabu sitini na sita kwa idadi lakini vyenye umoja katika maelewano na mawazo, vilivyoandikwa na waandishi arobaini mbalimbali, ilichkua takriban muda wa miaka 1600 (karne 16) kuandikwa, haiwezi kuwa iliandikwa kwa ajali, au bahati mbaya. Hawa watu waliishi katika vipindi tofauti vya historia, wakifanya kazi mbalimbali tofauti, na kujiajiri/kuajiriwa katika sekta tofauti,serikali na maeneo tofauti ya kijiografia. Waliishi katika nyakati tofauti na katika sehemu mbalimbali na waliandika kwa kujitegemea kila mmoja. Hivyo, ni vigumu kwao kuwa na njama ya kuandika udanganyifu. Lakini wakati kazi zao tofauti zinawekwa

pamoja, tunapata umoja mkubwa wa mawazo na mwendelezo kutoka mwanzo hadi mwisho. Hii haiwezi kutokea kwa bahati mbaya! Mpango wake ni lazima ulikuwa kazi ya mwenye nguvu kubwa (ya kimbingu). Kusema Biblia ni kazi ya bahati nasibu, ni sawa na kusema kwamba mamia ya wafanyakazi na wajenzi waliojenga mnara mkubwa wa "Askari" jijini Dar es Salaam, Tanzania, huku kila mmoja akifanya mpango wake bila mchoro mmoja ulioandaliwa mapema, kila mmoja akiwa na vifaa vyake, na kila mmoja jitihada yake binafsi.

C. Watu hawa walitoka sehemu tofauti, na walikuwa na kazi tofauti, na wakiwa na elimu tofauti, wakizumgumza na kuandika kwa nyakati tofauti, wakiwa na uwezo tofauti, wakiwa na mafanikio tofauti, na ujuzi tofauti, wameandika mambo yaliyotukuka na kushabihiana ni ukweli na ushahidi tosha kwamba waliunena ujumbe wa Mungu kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu. *"... bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu"* (2 Petro 1:21). Kwa mfano,

Musa alielimika katika hekima ya Wamisri akawa mchungaji na kiongozi; Joshua, askari na mpelelezi; Ezra, mwandishi mashuhuri na kuhani; Nehemia, mnyweshaji wa mfalme; Daudi, mchungaji, mwanamuziki, shujaa wa vita na mfalme; Sulemani, mwanadamu mwenye hekima zaidi na mfalme mwenye nguvu; Isaya nabii, Ezekiel, Myahudi aliye uhamishoni; Daniel, kiongozi mkubwa huko Babeli; Amos, mchungaji na mkulima; Mathayo, mtoza ushuru; Petro na Yohana, wavuvi, "wasio na elimu."; Luka, daktari; na Paul, mtengeneza mahema na msomi aliyelelewa miguuni pa Gamalieli. Wanaume wasiovuviwa kutoka maeneo, kazi na uelewa tofauti wasingeweza kuandika kitabu ambacho ni mzinga wa utamu wote, ngao ya silaha zote kali, mnara wenye taji la thamani duniani, taa yenye kuleta mwanga kwa wote. Nyumba ya wafalme wote, Jiwe kuu ambalo kwalo Mbingu huketi na kusujudiwa na Dunia kwa utukufu wake. Umoja wa maandiko usingekuwa kazi ya bahati nasibu! Lazima iwe kazi ya Mungu!

D. Kama Biblia si ya kweli basi makosa ni bora zaidi katika ulimwengu kuliko Ukweli. Kama siyo kweli ni uongo. Hata hivyo, Biblia imefanya kazi zaidi ili kuwainua watu na kuibariki dunia kuliko maneno yote ya wapagani, wenye wasiwasi, wachunguzi, wabishi, wakosoaji wa juu na wasioamini. Biblia daima imekuwa shoka la kusafishia njia ya ustaarabu na maendeleo. Daima imekuwa ushawishi wa utakaso wa asili ya binadamu. Watu wenye huruma zaidi, wema na undugu wameiridhia na kupokea kama ukweli. Hivyo, Kama Biblia si ya kweli basi makosa ni bora zaidi katika ulimwengu kuliko Ukweli.

E. Kama Biblia siyo ya kweli, hivyo "asili hutenda kazi bure." Katika dunia miongoni mwa wakazi wa dunia kuna daraja moja la viumbe ambao toka kwao viumbe wengine wote hupata faraja. Binadamu ni jina la kundi hilo. Kama wanadamu wakitoweka milele basi vyote hutoweka. Mazao ya mboga mboga kila mwaka hutoka kwa msimu na kurudi tena. Jamii ya wanyama hula juu yake na kufa. Siku zinasonga na miaka inaenda. Dunia yazunguka

katika mhimili wake inaendelea kulisha walio ndani yake mchana na usiku kumfanikisha kila mmoja. Miaka inaenda. Dunia inajizungusha katika  mhimili wake, hulizunguka jua, huvilisha na kuvizika viumbe vyake; wanadamu na vyakula vyao hutoweka daima.

"Sasa ni nini faida ya shughuli nzima? Kama mtu hataishi tena -kama Biblia si kweli, basi asili ni kazi bure; na kama kuna Muumbaji, basi anafanya kazi bila malengo. Na kufanya kazi bure, ... basi, kama, Biblia si kweli, kama historia inayotoa ya mwanadamu si kweli, kuanguka kwake, ahueni yake, vyote kuwa si kweli-kwa neno moja Injili ni UONGO, na Biblia ni UONGO, hakuna mtu hai anaweza kutoa sababu iliyo bora zaidi kuhusu kuwepo kwa sayari yetu" (Ubatizo wa Kikristo, Campbell). Au kama Biblia sio kweli ni sawa na kusema Hakuna malengo ya kuishi, Dunia ni kazi bure na haina maana na uumbaji wake ni kushindwa.

F. Tabia/Sifa bora ya Biblia, isiyopatikana katika vitabu vingine ni kwamba ina mamlaka na maelezo ya kutegemewa.

"Bwana asema hivi" ni maneno yanayopatikana zaidi ya mara elfu mbili. Inatoka kwa Bwana. Kauli zake zina msingi wa mamlaka kamili ya Mungu, Mwandishi wake. Wakati na waandishi, binadamu huwa na mashaka na bila uhakika, Biblia ni dhahiri na hakika. Pia inaongea juu ya mambo ya baadaye vyema kwa hakika kana kwamba ni siku za nyuma. Hii ni tofauti kati yake na kazi ya binadamu.

G. Biblia ni tofauti na vitabu vya kibinadamu, na haina upendeleo. Mtu ambaye ana pigwa picha kwenye anga za juu sana pia anaelezwa kuwa mtenda dhambi. Kwa mfano: Ilisema kuwa Daudi alikuwa ni mtu wa moyo wa Mungu mwenyewe, lakini yeye pia anaelezwa kuwa mzinzi na muuaji. Binadamu wangetoa wasifu wa upande mmoja tu. Kama ni rafiki, hupunguza dhambi zake na kuzidisha ukuu wa fadhila zake. Kama ni adui, huzidisha mapungufu yake na kupunguza heshima yake. Lakini sifa ya Biblia ni Tofauti kwamba "hakuna kumpendelea mtu". Inasema ukweli mtupu kuhusu kila mtu, ni ya namna tofauti na kazi za

kibinadamu.

H. Ni lazima kuwa Biblia ni kazi ya Mungu kwa sababu ya kutimizika kwa unabii wake. Tunaweza kutumia unabii mwingi na masomo mengi kama mfano, lakini tunaweza kuona bado baadhi ya taarifa za Kristo.

(1) Ilitabiriwa kwamba Kristo atazaliwa na bikira (Isaya 7:13-14). Ilitimia (Luka 1:26-35).

(2) Ilitabiriwa kwamba Kristo atazaliwa katika Bethlehemu (Mika 5:2). Ikawa (Mathayo 2:1-11)

(3) Ilitabiriwa kwamba mtangulizi ataandaa njia kwa ajili ya Bwana (Isaya 40:3; Malaki 3:1-2). Ilitimia kama ilivyotabiriwa. (Yohana 1:22; Marko 1:1-7).

(4) Tuna utabiri pia kwamba Yesu angesafiri kuingia Yerusalemu *"...amepanda punda, Naam, mwana-punda, mtoto wa punda."* (Zekaria 9:9). Ilitimia (Mathayo 21:1-9).

(5) Ilitabiriwa kwamba Mwokozi wetu angesalitiwa na rafiki anayemjua (Zaburi 41:9). Na sasa ni historia (Marko 14:43-49).

(6) Ilitabiriwa kwamba bei ya usaliti ingekuwa vipande thelathini vya fedha na kwamba msaliti angerudisha Jumla yote ya fedha hizo (Zekaria 11:12-13). Tunarekodi ya utimilifu wake katika (Mathayo 27:3-10).

(7) Ilitabiriwa kwamba angepigwa viboko na kudhihakiwa (Isaya 50:6). Na sasa ni historia (Yohana 10:1; Marko 14:65; Mathayo 27:27-31).

(8) Isaya alitabiri kwamba Yesu angeteseka katika ukimya kama kondoo (Isaya 53:4-7). Unabii ulitimilika (Marko 15:2-5).

(9) Katika Zaburi 22:18 tunaona, *"...Waligawanya nguo zangu, Na vazi langu wakalipigia kura."* Hii ikawa (Yohana 19:23-24).

Tunaweza kuona  pia utabiri mwingine mwingi uliotimilika lakini huu watosha. Hata hivyo, labda tunaweza kutumia mfano wa utabiri mwingine ambao sisi wenyewe ni mashahidi wa kutimilika kwake. Paulo alitabiri kwamba baadhi wataiacha imani na kuanzisha mifumo ya dini ambayo watu watakatazwa

kuoa/kuolewa na kuamuliwa wajiepushe na vyakula (1 Timotheo 4:1-3). Kanisa Katoliki la Kirumi linatimiza unabii huu. Wanakataza baadhi ya makundi kuoa/kuolewa na kuwazuia waumini wake kula nyama katika baadhi ya siku au nyakati. Je, Paulo alijuaje hii ingekuja kutokea? Maelezo pekee yanayoweza kutolewa ni kwamba; aliongozwa na Roho Mtakatifu. Hakuna njia nyingine ya kuelezea kutimilika kwa matukio yote yaliyotokea.

I. Mwongozo wa kiroho wa Biblia unathibitishwa kwa kauli zake kuhusu ukamilifu na hali ya mduara (tufe) wa dunia, inavyojizungusha. Ilikuwa mwaka 1543 ambapo "nadharia ya *Copernican*" kwamba dunia ni duara (tufe) na hujizungusha katika mhimili wake ilijulikana zaidi. Mamia ya miaka kabla ya mtu yeyote kuamini kama inawezikana, Mungu alisema; *"Yeye hutandaza kaskazi juu ya nafasi isiyo na kitu, Na kuutundika ulimwengu pasipo kitu"* (Ayubu 26:7). Hakuna mwanasayansi aliyetoa maelezo bora kuhusu dunia

zaidi ya haya. *"Yeye ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia..."* (Isaya 40:22). Hakuna mwanadamu katika wakati huu angeweza kuzungumzia *"duara ya dunia"* kwa sababu watu walidhani dunia ni tambarare. Yesu, katika kuongelea kuja kwake mara ya pili, anasema kuwa atakuja katika mchana na usiku (Luka 17:31,34). Kwa miaka hili lilikuwa fumbo gumu. Watu walijiuliza ni kwa jinsi gani Yesu ataweza kuja mchana na usiku kwa wakati mmoja? Maadui wapinga Biblia walidai kuwa hili ni utata. Lakini fumbo hili kwa sasa ni rahisi tangu binadamu walipogundua kuwa wakati upande mmoja wa Dunia ni usiku upande mwingine ni mchana. Kwa hiyo,wakati wowote ule Yesu atakapo kuja, atakuja katika mchana na usiku. Ukweli huu uliwekwa katika Biblia miaka mingi kabla ya binadamu kufanya ugunduzi huo. Je tunalielezaje hili? Kuna jibu moja tu: Mwandishi alivuviwa na nguvu ya kutoka juu.

J. "Josephus" anathibitisha ukweli wa Biblia kuhusina na Kristo: "Sasa kulikuwa na wakati ambapo Yesu, mtu

mwenye hekima, ikiwa ni sahihi (halali) kumwita mwanadamu; kwa kuwa alikuwa mtenda kazi za kustaajabisha, mwalimu wa watu walioupokea ukweli kwa furaha. Aliwavuta kwake Wayahudi na Wamataifa wengi. Alikuwa ndiye Kristo. Ndipo Pilato, kwa pendekezo la wakuu miongoni mwetu, akamhukumu kwenda msalabani, wote waliompenda mwanzo hawakumwacha; kwa kuwa alionekana mzima tena kwao siku ya tatu; kama ambavyo manabii wa Mungu walivyotabiri haya na mambo mengine kumi elfu ya kushangaza kumhusu. Na kabila la Wakristo, walioitwa kutokana na yeye, wangalipo leo" - Flavius Josephus *(37-100 B.K.)*: *Historia ya Kiyahudi (Jewish Antiquities), Kitabu cha 18, Sura ya 3.*

Huyo alikuwa mwanahistoria maarufu aliishi kati ya mwaka wa 37 B.K. na 100 B.K. Hivyo alikuwa na nafasi kubwa yakuchunguza madai yaliyofanywa kuhusiana na Kristo. Yeye hakuwa Mkristo, kwa hiyo, hakuwa anajaribu kueneza habari za ukristo bali kufanya kazi yake ya historia; kwa kuwa alikuwa mtaalam wa historia na

kazi yake ilikuwa kuandika historia ya yaliyotokea. Josephus anasema kwamba Kristo aliishi; na kwamba alikuwa "mwenye hekima, ikiwa ni sahihi (halali) kumwita mwanadamu;" kwamba alikuwa mtenda kazi za kustaajabisha; na kwamba Pilato alimhukumu kifo msalabani; na kwamba alifufuka siku ya tatu na kuwatokea wanafunzi wake. Huyo ni mwandishi wa historia wa kale, Mwana historia asiye Mkristo akithibitisha ukweli wa Agano Jipya.

Uthibitisho huo pia unawiana na wanahistoria wengine wa kale; Gayo Cornelius Tacticus, alizaliwa katikati ya karne ya kwanza na kufa 117, pia Pliny, "mdogo", 62 B.K.- 114 B.K.

K. Twaamini Biblia imevuviwa na Mungu kwa kuwa hakuna mwanadamu awezaye kuiboresha. Kazi zote za wanadamu zaweza kuboreshwa, fikiria kuhusu maboresho (maendeleo) yaliofanywa katika sayansi, viwanda, elimu, na katika kila tasnia.  Vitabu vya kale vinaachwa dhidi ya vile vilivyoboreshwa. Hata hivyo, kitabu kilichomalizika yapata miaka 1900

iliyopita kinaendelea kuwa chenye kuuzwa zaidi ulimwenguni.  Biblia inapatikana takriban kila makazi na maneno yake yako midomoni mwa mamilioni. "Tamaduni zimechimba kaburi kuizika Biblia, watu waliyokosa uvumilivu wakaichoma, wengi wa akina Yuda wameisaliti kwa Busu; Wengi wa akina Petro wameikana kwa kiapo, wengi wa akina Dema wameiacha; Lakini neno la Mungu limeendelea kustahimili" Hakuna mwanadamu ameweza kuiboresha au kutupatia Biblia bora, Je, hili si lakushangaza! Si katika yote; Ukweli uliandikwa na waandishi walioandika kwa uvuvio wa Mungu.

# 10

## SABABU YA KUMI



<u>SABABU YA KUMI</u>

# Kwa sababu linaamini kuwa Biblia ni kitabu kinachopaswa kutumiwa kwa usahihi

## 1. Utangulizi

PAULO alimpa wosia Timotheo juu ya kutii amri ya kutumia kwa halali Biblia: *"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli"* (2 Timotheo 2:15). Waalimu wengi na wahubiri hawana dhana hiyo ya Kibiblia. Hawajui kwamba mtu anapaswa kujibidiisha katika kutumia kihalali ujumbe toka mbinguni. Kama wangetaka kukufundisha kuhusu uongofu na wokovu wangekupeleka kwenye Agano la Kale (labda Zaburi) badala ya Agano Jipya (mathalani Matendo).

## 2. Mgawanyiko wa vitabu

A. Uainishaji sahihi wa vitabu hufanya kujifunza Biblia kuwa rahisi. Agano

la Kale linaundwa na vitabu thelathini na tisa na Agano Jipya vitabu 27.

B. Katika Agano la Kale tunapata vitabu vya sheria, historia, mashairi na unabii. Vitabu vitano vya kwanza vya Biblia vimeitwa sheria, kwa sababu ndivyo vyenye sheria ya Musa. Vitabu kumi na viwili vilivyofuata vimewekwa kama historia. Na kuna vitabu sita vya mashairi: Ayubu, Zaburi, Mithali, Mhubiri, Wimbo Ulio Bora na Maombolezo. Vitabu Kumi na sita vingine vya Agano la Kale vimewekwa kama unabii.

C. Katika Agano Jipya tuna Injili, historia ya wongofu, barua na unabii. Kwanza vitabu vinne vimeitwa Injili. Matendo ya mitume hujulikana kama historia ya wongofu, vitabu 21 vinavyofuata ni barua kwa makanisa na Wakristo. Ufunuo huwekwa katika kundi la unabii.

## 3. Mgawanyiko wa nyakati

Mgawanyiko sahihi wa nyakati mbalimbali za historia ni wa lazima. Ziko tatu kwa idadi, kwa majina; Nyakati za Mababa (Patriarchal), Uyahudi na Ukristo.

### 1. Nyakati za Mababa (Patriarchal)

(1) Jina Mfumo dume linatokana na maana na neno "Baba wa familia au kabila." "Patriarch" maana yake Baba. Chini ya Nyakati za Mababa dume, baba alikuwa nabii, kuhani na mtawala. Alielekeza mambo yote ya familia, dini na kisiasa. Mungu alizungumza na kichwa cha familia, na yeye, kwa upande wake, alizungumza na jamii ya familia.

(2) Huu uliitwa mfumo wa dini wa familia, ambapo kila familia iliachwa huru mbele za ushahidi wa Mungu kufanya na kutimiliza mambo yake. Iliyo sheria katika familia ya baba mmoja inaweza kutokuwa sheria katika familia za mababa wengine. Kwa mfano, Mungu alimwamuru Nuhu kujenga safina, lakini mababa wengine hawakupokea amri hiyo. Ibrahimu aliamriwa kufanya maandalizi ili amchinje mwanawe, Isaka, lakini amri hii haikuwahusu familia nyingine.

(3) Hakukuwa na mfumo wa maandishi ya dini. Mungu alizungumza na mkuu wa kabila kwa mdomo.

(4) Mfumo huu wadini ulidumu kwa takribani miaka 2500 toka Adam mpaka utoaji washeria ya Musa katika Mlima Sinai; na inaonekana kwamba haukusitishwa hapo, ila baadaye ulitumiwa tu na watu wa mataifa.

## 2. Nyakati za Uyahudi

(1) Mfumo huu ulitokana na ahadi ya baraka ya kidunia kwa Ibrahimu: *"nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka"* (Mwanzo 12:2). Sheria ilikuwa sehemu ya ahadi, na ilipewa miaka mia nne na thelathini baada ya Ahadi hiyo kutolewa (Wagalatia 3:16-17). Ili ahadi iweze kutunzwa, Mungu aliwapa serikali, sheria ya Musa, ambayo ilitumika kuwaongoza kidini na kisiasa.

(2) Mfumo wa kiyahudi au mfumo wa Musa ulikuwa ni mfumo wa kwanza kwa mwanadamu wa maandishi ya dini. Wana wa Ibrahimu, katika msafara wao kutoka Misri, waliongozwa mpaka

miimo ya mlima Sinai, na Mungu akawapa amri kumi zilizoandikwa juu ya mbao mbili za mawe (Kutoka 19,20). Tangu wakati huo, mwanadamu amekuwa na dini ya "kitabu".

(3) Mfumo wa familia wa ibada ulikua na kuendelea mpaka kuwa mfumo wa kitaifa. Badala ya kila baba kuongoza serikali kabila lilichukuwa nafasi ya uongozi. Vivyo hivyo ilikuwa sawa kwa ukuhani; Kabila moja lilitumia muda wake wote kama makuhani, Walikuwa na madhabahu moja na nyumba ya Mungu moja ya kitaifa.

(4) Lengo moja la mpango wa Wayahudi lilikuwa kuweka ukoo wa Ibrahimu tofauti na wa kipekee mpaka kutimilika kwa ahadi ya mzao (Kristo) (Wagalatia 3:16-19). Sifa hii ya upekee wa mfumo wa Musa umekuwa ukiitwa *"kiambaza cha kati kilichotutenga"*, kwa maana uliwatenga Wayahudi kutoka mataifa Mengine (Waefeso 2:14).

(5) Kazi nyingine ya sheria ilikuwa, *"ni kivuli cha mema yatakayokuwa"* (Waebrania 10:1). Bwana alitumia mfumo huu kutoa picha katika aina flani ya takwimu, mfumo wa utukufu

zaidi ambao ungefuata, Paulo anasema, *"Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani"* (1 Wakorintho 10:11). Maajabu katika jangwa yalikuwa mfano wa watu wa Mungu chini ya Agano Jipya. Hema na hekalu vilikuwa ndio aina ya kanisa katika nyakati hizi. Dhabihu ya kondoo mbele ya kanisa ilikuwa kama mfano wa Kristo, Mwana-kondoo wa Mungu, ambaye alikuwa afe kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Hajiri, Ishmaeli, Sarah na Isaka hutumiwa na Paulo kuonesha mifumo miwili. Musa ni mfano wa Kristo atakaye kuja. Hakika, yeye mwenye kuelewa dini ya Kikristo lazima kuelewa sheria ya Musa.

(6) Dhumuni jingine la sheria ilikuwa kuwa mwalimu kiongozi au mkufunzi, ambaye kupitia kwake watu wapate kuletwa kwa Kristo (Wagalatia 3:24). Dunia haikuwa tayari kumpokea Kristo na Injili yake. Hivyo mwalimu mkufunzi (sheria) alipaswa kuwaandaa watu kumpokea Kristo. Kwa kuruhusu agano la kwanza kuwa mwalimu wetu basi

yafaa kuwa tayari na kwa kukubali agano la pili.

(7) Sheria ilikuwa na Dosari; *"Maana kama lile la kwanza lingalikuwa halina upungufu, nafasi isingalitafutwa kwa lile la pili"* (Waebrania 8:7). Paulo pia anasema kwamba sheria ni dhaifu; *"Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili"* (Warumi 8:3). Udhaifu mmoja dhahiri ni kutokuwepo kabisa msamaha wa dhambi na makosa. Dhabihu zote walizotoa mbele ya madhabahu ya Mungu daima ilisababisha kusogeza mbele dhambi mwaka hadi mwaka na kuwafanya kujisikia na hatia; *"Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi"* (Waebrania 10:1-14).

(8) Mungu alikuwa na lengo ya kwamba kipindi cha Kiyahudi kidumu kwa muda tu; *"Torati ni nini basi? Iliingizwa kwa sababu ya makosa, hata aje huyo mzao aliyepewa ile ahadi..."* (Wagalatia

3:19). Hatujaachwa kutabiri juu ya mzao, Paulo alisema; *"Kwa mzao wako, yaani, Kristo"* (Wagalatia 3:16). Hivyo sheria ilibidi kutenguliwa na Kristo.

### 3.Nyakati za Ukristo

(1) Mpango huu ulikua kutoka kwenye ahadi ya kiroho kwa Ibrahimu; *"na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa"* (Mwanzo 12:3). Tunaona upya wa ahadi katika maneno haya: *"na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia"* (Mwanzo 22:18). Familia zote na mataifa yote ya dunia yalibarikiwa toka kwenye ukoo wa Ibrahimu. Moja ya hizo baraka ilikuwa Kristo ambaye alikufa kwa ajili yetu na kuwa mjumbe wa agano lililo bora zaidi.

(2) Hili ni Agano Jipya kama ulivyosema unabii wa Yeremia; *"Angalia, siku zinakuja, asema BWANA, nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda. Si kwa mfano wa agano lile nililolifanya na baba zao, katika siku ile nilipowashika mkono, ili kuwatoa katika nchi ya Misri; ambalo agano langu hilo walilivunja,*

*ingawa nalikuwa mume kwao, asema BWANA. Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema BWANA; Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu"* (Yeremia 31:31-33). Paulo anatangaza kwamba unabii huu wa Agano Jipya umetimia (Waebrania 8:6-13). Kwa hivyo, Mungu ametupa Agano Jipya tunaloliishi chini yake hata sasa.

(3) Mabadiliko ya mfumo wa ukuhani yalifanya umuhimu wa kubadilika kwa sheria: *"Maana ukuhani ule ukibadilika, hapana budi sheria nayo ibadilike"* (Waebrania 7:12).Yesu Kristo ni kuhani mkuu chini ya ukuhani mpya (Waebrania 9:11), na kila mtoto wa Mungu ni kuhani (1 Petro 2:5). Ukuhani ule ulipobadilishwa, sheria nayo ilibadilishwa. Kwa hiyo, sisi tunaishi chini ya sheria tofauti na ile ya nyakati za Uyahudi.

(4) Kristo alikuja kuchukua *"...Aondoa la kwanza, ili kusudi alisimamishe la pili"* (Waebrania 10:9). Hii ilikuwa ni

moja ya madhumuni yake ya kuja. La Pili limeanzishwa; Kwa hiyo, la kwanza limeondolewa.

(5) Kristo aliondoa torati kwa kuipigilia msalabani *"akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani"* (Wakolosai 2:14). Kristo alizaliwa chini ya sheria (Wagalatia 4:4-5), aliishi chini ya sheria, na hatimaye kufa chini ya sheria kutimiza hilo (Mathayo 5:17). Kristo aliishi na alikufa chini ya Agano la Kale. Mambo yaliyotokea kabla ya kifo chake yalitokea kabla ya Agano Jipya kuwa na nguvu.

(6) Agano Jipya lisingekuwa na nguvu au mamlaka ya utendaji kazi mpaka baada ya kifo cha Kristo: *"Maana agano la urithi lilipo, lazima iwepo mauti yake aliyelifanya. Kwa maana agano la urithi lina nguvu palipotukia kufa kwa mtu; kwa kuwa halina nguvu kabisa, akiwa yu hai yeye aliyelifanya"* (Waebrania 9:16-17). Tunaelewa hili vizuri kwa sababu tunaliona mara kwa mara, katika mfano hai, tunajua hakuna

mirathi iliyoandikwa ikafanya kazi mpaka baada ya kifo cha mwandishi wake. Paulo anatangaza uthibitisho wa hilo kuhusu agano la Mwokozi wetu. Kifo cha Kristo juu ya msalaba kinatimiliza kumalizika kwa torati na kukoma kwa sheria (Wakolosai 2:14), na hivyo baada ya hapo wakati mpya wa Ukristo ukaanza.

(7) Kipindi cha Ukristo kimetolewa kwa mataifa yote: *"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi..."* (Mathayo 28:19). *"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe"* (Marko 16:15). "Kiambaza cha kati kilichotutenga" Wayahudi na Wamataifa akakiondosha. *"Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga"* (Waefeso 2:14). Wote wanaweza patanishwa na Mungu katika mwili mmoja (Waefeso 4:4), ambalo ndilo kanisa (Waefeso 1:22-23). *"Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui*

*kwa huo msalaba"* (Waefeso 2:16). Kwa hiyo, *"Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu"* (Wagalatia 3:28).

(8) Leo katika nyakati za Ukristo, basi ni lazima kumtii Kristo. Unabii wa Musa; *"BWANA, Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye."* (Kumbukumbua La Torati 18:15). Petro alifundisha kwamba unabii ule ulitimizwa na kwamba *"Kwa maana Musa kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi. Na itakuwa ya kwamba kila mtu asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake"* (Matendo 3:22-23). Hii ilithibitika katika kugeuka kwa sura ya Kristo. Yesu alipogeuka sura yake, Musa na Eliya wakatokea. Hata Petro alitaka kujenga vibanda vitatu: kimoja kwa kila mmoja. Lakini mpango huo uliharibiwa kwa maneno

haya; *"...Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye"* (Mathayo 17:5). Kuna wakati ambapo wanadamu waliwasikiliza Musa na Eliya, lakini sasa ni lazima wamsikilize Mwana wa Mungu. Paulo anatangaza, *"Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu"* (Waebrania 1:1-2).

# 2 Timotheo 2:15

| | | |
|---|---|---|
| Manabii | — | Kristo |
| Wayahudi | — | Wote |
| Mawe | — | Moyo |
| Wanyama | — | Kristo |




| | |
|---|---|
| **Liliitwa la "Kale"** 2 Kor. 3:14 | **Liliitwa "Jipya"** 2 Kor. 3:6 |
| **Liliitwa la "Kwanza"** Ebr. 10:9 | **Liliitwa la "Pili"** Ebr. 10:9 |
| **Lilikuwa na makosa** Ebr. 8:7 | **Ni kamilifu** Yak. 1:25; 2:12 |
| **Lilikuwa tukufu** 2 Kor. 3:7 | **Lina utukufu zaidi** 2 Kor. 3:9,11 |
| **Kwa Wayahudu tu** Kum. 5:1-15 | **Ni la kilimwengu** Mt. 28:18-20; Efe. 2:11-22 |
| **Lilibeba vivuli na aina** Ebr. 9:24; 10:1; Kol. 2:14-17 | **Linabeba taswira halisi** Ebr. 9:24; 10:1-4; 1 Pet. 3:19-21 |
| **Ukuhani wa kilawi** Ebr. 7:1-28 | **Kristo ni Kuhani mkuu** Ebr. 7:1-28 |
| | **Wakristo ni makuhani** Ufu. 1:5-6; 1 Pet. 2:5,9 |
| **Lilitoa dhabihu za wanyama** Ebr. 9:18-22; 10:1-4 | **Kristo alimwaga damu yake** Ebr. 9:12,14 |
| **Dhambi zilikumbukwa** Ebr. 10:1-4 | **Dhambi hazikumbukwi** Ebr. 8:7-12 |

## La Kwanza (Waebrania 10:9)

1. Agano la Kale (2 Wakorintho 3:14)
2. Aliondoa la kwanza (Waebrania 10:9)
3. Kutokana na manabii (Waebrania 1:1-2)
4. Kutokana naWayahudi (Mwanzo 17:13)
5. Liliandikwa juu ya mawe (2 Wakorintho 3:7)
6. Kivuli cha mambo mema (Waebrania 10: 1)
7. Sadaka mara kwa mara, sadaka hiyo hiyo (Waebrania 10:11)
8. Damu ya wanyama (Waebrania 10:14)
9. Wanyama kama sadaka kwa wafu (Waebrania 10:14)
10. Kumbukumbu ya dhambi (Waebrania 10:3)
11. Haikuweza kukamilisha jambo lolote au kamili (Waebrania 7:19)
12. Tohara ya ngozi (Mwanzo 17:9-11)
13. Huduma ya hukumu (2 Wakorintho 3:9)
14. Walawi ukuhani (Waebrania 7:11)
15. Ukuhani na sheria (Waebrania 7:12)
16. Sheria yenye dosari (Waebrania 8:7)
17. Kufutwa (Wakolosai 2:14)

## La Pili (Waebrania 10:9)

1. Agano Jipya (2 Wakorintho 3:6)
2. Anaanzisha jipya (Waebrania 10:9)
3. Linatokana na Kristo mwenyewe (Waebrania 1:1-2)
4. Limetolewa kwa kila aliye hai (Marko 16:15-16)
5. Iliandikwa katika mioyo (2 Wakorintho 3:3)
6. Kweli tupu (Waebrania 8:1-3)
7. Kristo sadaka ya wote (Waebrania 7:27)
8. Damu ya Kristo (Waebrania 9:14)
9. Mwili wa mwanadamu kama sadaka hai (Warumi 12:1).
10. Hakuna kumbukumbu ya dhambi tena (Waebrania 8:12)
11. Timilifu na kamili katika Kristo (Wakolosai 1:28)
12. Tohara ya moyo (Warumi 2:29)
13. Kuwezesha Haki (2 Wakorintho 3:9)
14. Kila mkristo ni kuhani(1 Petro 2:5)
15. Ukuhani na sheria vya badilika (Waebrania 7:12)
16. Sheria kamilifu (Yakobo 1:25)
17. Ya kudumu (2 Wakorintho 3:11)

## 2. Mwizi msalabani

Katika hatua hii tunahitaji kujibu swali linaloulizwa mara kwa mara. "Vipi kuhusu mwizi pale msalabani? Ikiwa ubatizo ni wa lazima ili kuokolewa kwa nini hakubatizwa?

Rafiki, hata hatujaribu kufikiri kwamba Kristo alijichanganya au kwamba yupo katika mkanganyiko. Hata hivyo, ubatizo ni muhimu kwa wokovu (Marko 16:16; Matendo 2:38; Matendo 22:16; 1 Petro 3:20-21). Hivyo basi, vipi kuhusu mwizi yule msalabani?

A. Kwanza kabisa niruhusu kusema kwamba "haiwezi kuthibitishwa kwamba mwizi yule alikuwa hajabatizwa" Yohana Mbatizaji alipita katika nchi akibatiza watu, hivyo pengine mtu huyo aliyegeuka kuwa mwizi alibatizwa pamoja nao (Luka 7:29-30; Luka 3:21).

B. Katika nafasi ya pili, tunaona kwamba hakuna utata katika mafundisho ya Kristo, kwa sababu hii ilikuwa chini ya sheria ya Musa. Sheria ya Musa ilikuwa bado haijatimilizwa kwa wakati huu, maana Yesu alikuwa hajafa bado pale msalabani; alikuwa bado hai. Hakuna

mtu aliyewahi kuamrishwa abatizwe kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu chini ya nyakati hizo. Mwizi aliishi na kufa chini ya sheria tofauti na ile mpya tulio nao sasa (Wakolosai 2:14).


Pengine mfano utasaidia kufafanua wazo hilo: Texas lilikuwa taifa huru kwa miaka kumi, na kisha kwa hiari walijiunga na kuwa sehemu ya Marekani. Tuseme kwamba baada ya mabadiliko hayo mtu mmoja wa Texas alikataa kuheshimu bendera ya Marekani. Alikamatwa na kuwekwa katika jela. Yeye kwa hasira akipiga kelele, "sikuwa na umuhimu wa kuheshimu bendera ya Marekani tulipokuwa kwenye serikali ya Texas, hivyo siwezi kuiheshimu hata sasa kwenye serikali ya Marekani" Naye aliajiri mwanasheria kumtetea, Sasa basi atakuwa mwanasheria mpotofu asieenda shule kabisa kama atasimama mahakamani na kusema; mteja wangu hakupaswa kuheshimu bendera ya Marekani enzi zile kulikuwa na uongozi wa Texas hivyo hana umuhimu wa kufanya hivyo hata sasa. Basi, vivyo

hivyo, itakuwa ajabu kwa mhubiri atakaye simama kuhubiri, kwamba haikuwa lazima kwa mnyang'anyi na wengine chini ya nyakati za torati kubatizwa ili kuokolewa na hivyo afikiri kwamba hakuna ulazima huo hata sasa katika nyakati za Ukristo.

C. Na katika nafasi ya tatu hakuna utata kwa sababu, *"Mwana wa Adamu* (Kristo) *anayo amri (mamlaka / nguvu) duniani ya kusamehe dhambi"* (Luka 5:24). Wakati Kristo alipotembea na kuongea na watu duniani, aliweza kumwambia kipofu "Ona!": Viziwi, "Sikia!" Kwa wagonjwa,"Inuka na chukua kitanda chako"; na kwa wenye hatia ya dhambi, "Umesamehewa dhambi zako." Kristo alikuwa na mamlaka hayo juu ya nchi; haya yalikuwa kabla ya kuanza kutumika kwa agano lake, kwa kuwa ilifaa lianze kutumika rasmi baada ya kifo chake. Kwa ushahidi tunaweza kumnukuu mwandishi wa kitabu cha Waebrania: *"Maana agano la urithi lilipo, lazima iwepo mauti yake aliyelifanya. Kwa maana agano la urithi lina nguvu palipotukia kufa kwa mtu; kwa kuwa*

*halina nguvu kabisa, akiwa yu hai yeye aliyelifanya"* (Waebrania 9:16-17). Baada ya kufa kwake Kristo Msalabani na mapenzi yake (Agano) kuanza kufanya kazi, mapenzi hayo mapya ni lazima yatekelezwe kulingana na maelekezo yanayopatikana ndani yake. Ole wake mtu ayabadilishaye!

## UCHUNGUZI NA HITIMISHO


MGAWANYIKO WA VIPINDI
2 Timotheo 2:15
KIPINDI CHA MABABA / WAZAZI
2500+ Years
Mlima Sinai
KIPINDI CHA MUSA
1500 Years
KIPINDI CHA UKRISTO
2000+ Years
1. Kuanzia uumbaji hadi Sinai
2. Dini ya kifamilia
3. Mungu alizungumza kwa kinywa
4. Dhabihu za wanyama
(Mwanzo 4)
5. Tohara
(Mwanzo 17:10)
1. Kutoka Mlima Sinai hadi Msalabani
2. Dini ya kitaifa
(Kumbukumbu la torati 5:3; Waefeso. 2:12)
3. Yenye mapangufu
(Waebrania 8:7)
4. Limetoweka
(Wakolosai 2:14-16; 2 Kor 3:7-14)
5. Lilikuwa ni kiongozi
(Wagalatia 3:24-25)
6. Dhabihu ya wanyama; Siku ya Sabato; Sikukuu ya Pasaka; Tohara; Mwizi.
1. Kuanzia siku ya Pentekoste hadi siku ya hukumu
2. Ulimwengu
(Mathayo 28:19)
3. Kristo ana mamlaka yote
(Mathayo 28:18)
4. Lazima kumtii Kristo
(Waebrania 5:8-9; Matendo 3:23)
5. Kanisa au Ufalme
(Matendo 2:47; Wakolosai 1:13)
6. Injili kwa wote
(Marko 16:15; Warumi 1:16)




Inatumiwa kwa idhini ya; "World Video Bible School"{WVBS} yaani Shule ya Biblia kwa njia ya filamu ulimwengu. https://video.wvbs.org/

# KWA NINI MIMI NI MSHIRIKA WA KANISA LA KRISTO

# 11

## SABABU YA KUMI NA MOJA



## SABABU YA KUMI NA MOJA

# Kwa sababu sio la kimadhehebu

### 1. Utangulizi

KANISA la Kristo ni taasisi iliyokuwa "kabla ya madhehebu." Tunaposema "kabla ya madhehebu," hatumaanishi "madhehebu yote." Baadhi ya watu wanaodai kuwa wao walikuwepo "kabla ya madhehebu" kiuhalisia ni wa madhehebu wote. Wote ni wa kimadhehebu kwa maana kwamba wanaunga mkono madhehebu yote. Kanisa la Kristo lilikuwapo "kabla ya madhehebu," sio la kimadhehebu kwa maana kwamba sio madhehebu na kwamba lipo kinyume na dhana ya umadhehebu.

### 2. Umadhehebu unapingana na Biblia

Ni dhahiri kwamba umadhehebu upo kinyume kabisa na Biblia. Kwa mfano, chunguza haya yafuatayo:

# SIO DHEHEBU

# Umadhehebu

1. Taasisi au makanisa mengi
2. Umeanzishwa na wanadamu
3. Vichwa ni wanadamu
4. Kanuni za wanadamu
5. Unavaa majina ya wanadamu
6. Unafuata wanadamu
7. Wingi wa makanisa yasiyotambulika katika Biblia
8. Ushiriki katika madhehebu sio lazima ili kuokolewa.
9. Unahubiri Injili nyingi
10. Unaandika upya kanuni kila baada ya miaka michache.
11. Imani nyingi
12. Ubatizo mwingi
13. Kujiunga na makanisa
14. Unadai unajikita katika matawi ya kanisa.
15. Huongozwa na kanuni tofauti.
16. Wanamshukuru Mungu katika maombi yao kwa makanisa mengi.
17. Unadai kwamba mafundisho si muhimu.

## Ukristo kabla ya madhehebu

1. Mwili au Kanisa Moja (Mathayo 16:18; 1 Wakorintho 12:20).
2. Limeanzishwa na Kristo (Mathayo 16:18).
3. Kristo ndiye Kichwa (Waefeso 1:22-23).
4. Biblia ndiyo kitabu pekee cha kanuni za kidini (2 Timotheo 3:16-17).
5. Linamtukuza Mungu katika jina la Mkristo (1 Petro 4:16).
6. Kufuata wanadamu kumepingwa (1 Wakorintho 1:10-13).
7. Limetajwa katika Biblia (Warumi 16:16).
8. Ushiriki katika kanisa la Kristo ni lazima ili kuokolewa (Waefeso 6:23).
9. Ikiwa mtu atahubiri injli nyingine yoyote tofauti atahukumiwa (Wagalatia 1:8,9).
10. Biblia inabaki kuwa ile ile (Mathayo 24:35).
11. “Imani moja” (Waefeso 4:5).
12. “Ubatizo mmoja” (Waefeso 4:5).
13. Mungu ndiye kulizidisha “kanisa” lake (Matendo 2:47).
14. Yesu alisema “Kaeni ndani yangu” mzabibu wa kweli (Yohana 15:1-6).
15. Wanaenenda kwa kanuni moja (Wafilipi 3:16).
16. Yesu aliomba kwa ajili ya umoja (Yohana 17:20-21).
17. Wanakuwa waangalifu katika mafundisho ili kujiokoa na kuokoa wengine (1 Timotheo 4:16).

Hapo juu ni tofauti chache tu. Zinaweza kuongezeka zaidi. Lakini hii inatosha kuwashawishi wanaoweza kushawishika kwamba umadhehebu unapingana na Biblia.

**3. Uibukaji wa Ukatoliki na Umadhehebu**

Bwana alianzisha kanisa lake takriban miaka elfu mbili iliyopita. Taasisi hii takatifu ilibaki kuwa takatifu bila unajisi kwa kipindi kirefu. Ndipo uasi uliotabiriwa ukaanza kutimizwa (Matendo 20:29-30; 2 Wathesalonike 2:1-4; 1 Timotheo 4:1-3). Amri na uvumbuzi wa wanadamu ulipelekea kukua taratibu kwa madhehebu ya Rumi (Roman Catholic Church). Baadaye wanadamu walijaribu kulifanyia matengenezo kanisa Katoliki, kisha jitihada zao zilipelekea kuanzishwa kwa makanisa mengi ambayo yametengenezwa na wanadamu. Jitihada hizo zilizalisha mamia ya madhehebu yenye mafundisho yanayokinzana. Wanahistoria wote wanajua kwamba umadhehebu ni matokeo ya Ukatoliki. Lakini kanisa lililoanzishwa na Yesu na mitume katika karne ya kwanza halikuwa Kanisa Katoliki wala

Kanisa la Kiprotestanti, bali lilikuwa kanisa la Kristo, kanisa la kweli. Washirika hawakuwa Wakatoliki wala Waprotestant, bali walikuwa Wakristo.

### 4. Urejeshwaji wa Ukristo kabla ya madhehebu

Katika mwanzo wa karne ya kumi na tisa watu walianza kuwasilisha wito mpya kwa ulimwengu, wito ambao umesambaa kwa kasi ya ajabu na unafanya mapinduzi katika ulimwengu wa kidini. Katika mwisho wa karne hiyo kulikuwa na jitihada zilizoenea kote nchini Marekani ili kurejesha Ukristo wa Agano Jipya. Watu hawa hawakufanya kazi ili kurejesha kanisa lolote la kibinadamu bali walifanya kazi ili kurejesha kanisa la kweli ambalo lilikuwa limekwishapotea kwa watu wengi kwa sababu ya mafundisho ya Ukatoliki na umadhehebu. Warejeshaji walitoa wito kwa wanadamu wawe washirika wa kanisa la Kristo pekee na si vinginevyo bali kuwa Wakristo. Walijua kwamba kama wangefanya kile ambacho Wakristo wa karne ya kwanza walifanya, wangekuwa kama Wakristo wa karne ya kwanza walivyokuwa.

Walijua mbegu ile ile ingezaa matunda yale yale na kanisa lile lile. (Angalia mjadala kwenye mada ya 5, Sababu ya B, ukurasa 40).

Tuziangalie baadhi ya kazi za watu hawa, kama ifuatavyo:

A. James O'Kelly na wengineo wa Carolina Kaskazini (USA) waliacha kanisa la Methodist Disemba 25, 1793, na kwa muda walichukua jina la "Republican Methodists." Hata hivyo, mnamo mwaka 1801 waliazimia kuwa watambulike kama "Wakristo" pekee, hakuna mtu ambaye ni kichwa cha kanisa isipokuwa Kristo, kutokuwa na kitabu cha kanuni za imani isipokuwa Biblia.

B. Daktari Abner Jones wa Vermont (USA), Mbaptist, alihubiri kwamba majina ya kichama na kimadhehebu na kanuni za kidini lazima zikomeshwe. Septemba, 1800, alianzisha kanisa huko Lyndon, Vermont (USA). Na baadaye alianzisha kanisa jingine Bradford, na, mwaka 1803, alianzisha jingine huko Piermont, New Hampshire (USA). Elias Smith, mhubiri wa Kibaptist, baadaye aliungana na

harakati za Dk. Jones na washirika wote wa lile kundi walimfuata, akiachana na madhehebu yale.

C. Chester Bullard alisitisha uhusiano wake na Wamethodist kwa sababu baadaye aliamini kuwa kuzamishwa ndilo tendo la ubatizo. Hata hivyo, alikataa kuzamishwa na Wabaptist kwa sababu hakuamini katika madhehebu ya Wabaptist. Bullard hatimaye alibatizwa kwa kuzamishwa na rafiki yake, Landon Duncan, Mdhamini wa Kaunti. Alihubiri usiku huo baada ya kubatizwa, na hatimaye akaanzisha makusanyiko kadhaa huko Virginia (USA).

D. Harakati kubwa zaidi za marejesho ziliongozwa na Barton W. Stone, mhubiri mashuhuri wa Kentucky (USA). Mwanzoni Stone alihubiri katika madhehebu ya Wapresibiteri (Presbyterian), lakini mahubiri yake yalikuwa tofauti na kitabu cha kanuni za kidini (Kukiri kwa Imani ya Westminister; mkutano wa majimbo ya kanisa huko Lexington, Kentucky USA), Kanisa la Wapresibiteri walimtenga yeye pamoja na watu wengine kadhaa.

Mwanzoni walijitenga na kuwa Wapresibiteri huru, Wapresibiteri wa Springfield. Baada ya mwaka mmoja hiyo haikuwa ya kimaandiko, na wakaikanusha. Katika kufanya hivi waliandika kitabu mashuhuri, "The Last Will and Testament of the Springfield Presbytery" [Wosia wa Mwisho wa Wapresibiteri wa Springfield], June 25, 1804. Hizi ni baadhi ya kauli kutoka katika wosia huo:

(1) "Tunatamani, mwili huu ufe, uyeyushwe, uzame, na kuunganika pamoja na mwili wa Kristo kwa ujumla;"

(2) "Tunatamani, kwamba jina letu la heshima, pamoja na cheo chake cha heshima (Reverend) vitasahaulika";

(3) "Tunatamani, kuwa mamlaka yetu ya kutunga sheria kwa ajili ya serikali ya kanisa, na kuzitekeleza kwa mamlaka tuliyopewa yatasitishwa milele;"

(4) "Tunatamani, kwamba kanisa la Kristo lirejee katika hali yake ya asili ya serikali ya ndani";

(5) "Tunatamani, kwamba watu wataichukua Biblia kama mwongozo

wao pekee."

Hii ilisitisha Presibiteri ya Springfield (Springfield Presbytery), na wosia huu ni ushahidi tosha kwamba hawakuanzisha madhehebu mapya. Walivunja madhehebu na kuwa sio wa kimadhehebu (au kabla ya umadhehebu). Baada ya miaka michache kundi hili liliongezeka na kufika maelfu.

Hii ilitokea miaka mitano kabla ya Alexander Campbell kuja Marekani. Hii pekee inaweza kuwanyamazisha wale ambao hawana maarifa ya kutosha ambao wamemshutumu Alexander Campbell wakidai kwamba yeye ndiye aliyeanzisha kanisa la Kristo.

E. Thomas Campbell, mhubiri wa Kipresibiteri alikuja Marekani mwaka 1807. Wapresibiteri walimwona kama mtu mpenda mabadiliko sana, na alijiondoa kutoka katika kanisa hili. Katika mkutano ulioitishwa wa wale ambao walishikilia mawazo sawa, na yeye katika nyumba kuu kuu ya shambani, Campbell alizungumza na akahitimisha hotuba yake kwa kuwasihi kuchukua kanuni zifuatazo: "Pale

ambapo Maandiko yanazungumza, tuzungumze; pale ambapo yapo kimya, tuwe kimya." Kanuni hii ilikubaliwa na ulikuwa mwanzo wa harakati nyingine ya marejesho. Kulikuwa kuna kweli nyingi za msingi ambazo zilikuwa hazijaeleweka, lakini kanuni hii iliwaongoza katika hizo kweli mmoja baada ya mwingine. Mnamo Agosti 17, 1809 iliamuliwa kwamba wangeweza kuungana rasmi na kuwa taasisi ya kawaida inayojulikana kama "Ushirika wa Kikristo wa Washington (Christian Association of Washington)."

F. Alexander Campbell, mwana wa Thomas Campbell, aliwasili Marekani mnamo Septemba 29, 1809. Aliunga mkono harakati za marejesho kwa moyo wake wote. Kanuni hii, "Zungumza kile ambacho Biblia inazungumza na kuwa kimya pale ambapo Biblia ipo kimya," taratibu lakini kwa uhakika walivunja minyororo yao ya umadhehebu. Walibatizwa Juni 12, 1812 na Mzee Luce, mhubiri wa Kibaptisti, kama ukiri alioufanya towashi mbele ya Filipo, Mdo 8. Hii ilikuwa kinyume na mafundisho ya

Kibaptist; na kwa hiyo hawakuwa Wabaptisti. Hata hivyo, mwaka 1813 Cambells na Kanisa la Brush Run walijiunga na chama cha Redstone (Redstone Association), chama cha Kibaptist, wakiwa wamejiwekea masharti kwamba wangeweza kuhubiri kitu chochote kilichopo kwenye Biblia bila kujali kanuni yoyote duniani. Lakini kadiri mbavyo akina Campbell walivyopata ukweli ndivyo walivyozidi kuachana na Ubaptisti. Matokeo yake, ushirika wao pamoja na Wabaptisti haukuwa mzuri kwa makundi yote mawili yaliyovunjika kidogo kidogo.

Mwaka 1832 huko Lexington, Kentucky (USA), kulikuwa na muunganyiko wa nguvu za kundi la Campbell la watu takribani elfu 12 pamoja na kundi la Barton W. Stone, lililokuwa na idadi ya watu takribani elfu 15. Kazi hii ya mawazo ya pamoja na muungano iliendelea kwa sababu Biblia ndiyo iliyokuwa kiongozi wao pekee. Kufikia mwaka 1835 harakati za wanamarejesho ziliunganishwa na kuwa katika lengo moja. Ni vigumu kwa makundi mbalimbali kutengana

wanapokuwa wanahubiri Biblia, Biblia nzima, si kitu kingine isipokuwa Biblia. Ukweli kwamba dunia imegawanyika sana, ni ushahidi tosha kwamba si wote wanahubiri Biblia.

Ni dhahiri kabisa kulingana na historia kwamba Alexander Campbell hakuwa mwanzilishi wa kanisa lolote. Vuguvugu la kurejesha Ukristo wa asili katika dunia lilikuwa limekwishaanza hata kabla hajawasili Marekani.

Alivunja mahusiano na makanisa ya kibinadamu, yanayofungwa na kitabu cha kanuni za imani za kidini na kuwa Mkristo tu. Aliunga mkono harakati za marejesho kwa kuhubiri, kuandika na kwa kufanya mijadala. Kwa uwezo wake wa ajabu alitoa wito sana kwa watu kuliko matengenezo yoyote. Hiki ndicho kilichokuwa kinahitajika ili kanisa liweze kukua. Baadhi ya wahubiri wa kidunia ambao walipendelea zaidi kufuata vyama badala ya ukweli, walifanya uharibifu mkubwa ili kuumiza harakati za marejesho kwa kuzita Ukempbeli (Campbellism) na wakaliita kanisa la Kikempbeli (Campbellite Church).

Kwa nini? Walikuwa wanatumainia kuchochea msimamo dhidi ya harakati na wito kurudi kwenye Biblia na kurejesha Ukristo wa Agano Jipya.


Ni jambo jema tu na la haki kunukuu maneno ya Alexander Campbell katika kujibu swali hili, “Ukempbeli (Campbellism) ni Nini?” Sikiliza jibu lake:

Ni jina la utani lenye dhihaka lililoundwa na kutumiwa na wale ambao wameridhia kubakia wamegawanyika. Hawa hawawezi hata kuanza kuufikiria Ukristo hata kwa njia nyingine yoyote bali kugawanyika. Hata hivyo, madhehebu haya ndiyo hasa yenye kutukanisha na kuaibisha. Wale ambao wanachagua hii migawanyiko na majina ya kidini ambayo si ya kibiblia wanavunja sheria ya Kristo. Anazungumza mabaya juu ya ndugu yake, na anahesabiwa kama mwenye kushutumu au mtukanaji, na anawekwa katika kundi la wamchukiao Mungu na wale ambao hawana nafasi katika ufalme wa mbinguni. Wale ambao wanayakubali kwa kuchagua migawanyiko wanamkana Kristo na

kumtukana; Wanatoa heshima ya Kristo kwa Ibilisi; kwa maana wale wote wazungumzao maovu, wenye kujeruhi, na kuwaharibu wengine ni wa Ibilisi. Kama Wakristo wangekuwa wamejengwa kikamilifu katika mafundisho ya mitume wangejisikia kukwazwa, kuhuzunishwa, na kufedheheshwa kwa kuitwa kwa jina la mtu yeyote. Hili lingewaudhi sawa tu na kuitwa mwizi, mwasherati, au mlevi. Siku zote nimekuwa nikipingana na kila kitu kinachoonekana cha kugawanya (kama madhehebu); na kama watu wa madhehebu tofauti wakinikashifu au yeyote kati ya wale wanaopenda Maandiko kuliko kanuni za kibinadamu, na ufalme wa Yesu Masihi, kuliko dhehebu lolote; nasema, kama wakitukashifu kwa majina na wasifu wetu tunayakana na kuyakataa, inawapasa kutoa majibu kwa yule anayehukumu kwa haki.

“Lakini sisi tunapinga jina, mafundisho, hisia za madhehebu yoyote au faraka katika Ukristo.”—Christian Baptist, kurasa za 451, 452.

Ni dhahiri kwamba kanisa la Kristo




Inatumiwa kwa idhini ya; "World Video Bible School"{WVBS} yaani Shule ya Biblia kwa njia ya filamu ulimwengu. https://video.wvbs.org/

si “mojawapo ya madhehebu.” Ni kanisa ambalo lilikuwapo takriban karne ishirini zilizopita. Kila mshirika ameongezwa kwalo na Bwana mwenyewe (Matendo 2:47). Lililokuwa kabla ya madhehebu likiwa na wito usiokuwa wa kugawanya; wito kwa ajili ya ulimwengu kurudi katika Injili ya awali.

# 12

## SABABU YA KUMI NA MBILI



## SABABU YA KUMI NA MBILI

# Kwa sababu ni la kimaandiko katika kufanya kazi ya kimisionari

**1. Hitaji la kuhubiri**

A. Ni amri ya Kristo kwamba Injili ihubiriwe. Alisema, *"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa"* (Marko 16:15-16). Ni muhimu sana kutii sehemu ya kwanza ya wito mkuu kama ilivyo kutii sehemu yake inayofuatia. Utii katika sehemu inayofuata unategemea utii wa mwanadamu katika sehemu ya kwanza: juu ya kupeleka Injili kwa wale wasioifahamu.

B. Haiwezekani kupata matunda ya Injili bila kuanza kupanda mbegu ya ufalme. Katika mfano wa mpanzi Yesu alionesha upandaji wa mbegu kabla ya uzalishaji wa matunda (Mathayo 13:3-8,18-23).

Mfano huu ni ushahidi kwamba kuhubiri Injili ni muhimu sana katika ukuaji wa ufalme wa Kristo.

C. Hakuna uwezekano wa kuwa na imani pasipo kusikia Neno: *"Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo"* (Warumi 10:17). Kusikia neno la Kristo kunazalisha imani. Hiyo ni sababu mojawapo ya kuwa na Neno lililoandikwa: *"Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake"* (Yohana 20:30-31). Shetani anajua kwamba hivi ndivyo imani inavyozalishwa: *"Wale wa karibu na njia ndio wasikiao, kisha huja Ibilisi akaliondoa hilo neno mioyoni*

*mwao, wasije wakaamini na kuokoka"* (Luka 8:12). Wakorintho waliamini kupitia njia hii: *"... Wakorintho wengi waliposikia, waliamini, wakabatizwa"* (Matendo 18:8).

D. Watu hawawezi kuletwa karibu na Mungu bila kufundishwa juu yake: *"Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; nami nitamfufua siku ya mwisho. Imeandikwa katika manabii, Na wote watakuwa wamefundishwa na Mungu. Basi kila aliyesikia na kujifunza kwa Baba huja kwangu"* (Yohana 6:44-45). Baba anawasogeza wenye dhambi kwa Kristo, na inafanyika kupitia Neno. Hii ni muhimu sana tunapaswa kusema kwa nguvu!

E. Yesu alitanguliza mafundisho kwanza katika mfumo wa uongoaji. *"Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, Na kwa masikio yao hawasikii vema, Na macho yao wameyafumba; Wasije wakaona kwa macho yao, Wakasikia kwa masikio yao, Wakaelewa kwa mioyo yao, Wakaongoka, nikawaponya."* (Mathayo 13:15). Katika nukuu hii tunapata mpangilio

ufuatao:

(1) Mafundisho— *"...Wakasikia kwa masikio yao, Wakaelewa kwa mioyo yao..."*

(2) Kuelewa.

(3) Kurudi (kugeukia upande tofauti) au kuongoka.

(4) Uponyaji au msamaha.

Bila mafundisho, hakuna kuelewa;
bila kuelewa, hakuna kuongoka;
bila kuongoka, hakuna uponyaji au msamaha. Hii inapaswa kuwavutia Wakristo juu ya wajibu wao wa kupeleka Injili. Ni sawa na tunavyoshindwa kutimiza wajibu wetu katika kuhubiri Injili kwa waliopotea tunashindwa kuwafanya ili waweze kuokolewa.

F. Neno la Bwana ni nguvu inayosababisha mchakato wa kuzaliwa upya: *"Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele"* (1 Petro 1:23). Hapawezi kuwa na uzazi wa kimwili pasipo baba, hali kadhalika hakuna kuzaliwa upya bila mafundisho

ya neno la Mungu.

G. Pale pasipo na mahubiri, hakuwezi kuwepo na wokovu. Paulo alisisitiza ukweli huu kwa kusema, *"kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri?"* (Warumi 10:13-14). Hebu tuanze na fungu la mwisho halafu tutarudi kwenye la kwanza: Pale pasipo na mahubiri, hakuwezi kuwepo kusikia, bila kusikia, hakuna kuamini; bila kuamini, hakuna kuongoka, bila kuongoka, hakuna wokovu. Kwa hiyo haijalishi tunaanza na fungu la kwanza halafu tunakwenda la mwisho au tunaanza na la mwisho halafu tunarudi kwenye la kwanza, bado tunapata hitimisho moja, nalo ni: Injili ni lazima ihubiriwe ili roho ziweze kuokolewa.

H. Kutokuwa na msimamo katika madhehebu kunaonekana katika madai yao kwamba Mungu anawaongoa watu moja kwa moja kupitia kazi ya Roho Mtakatifu, hata hivyo, hufanya mikutano ya Injili na kusaidia wamisionari. Kama hili lingekuwa

ni kweli, kwamba Mungu huwaokoa watu moja kwa moja kwa njia ya Roho wake Mtakatikfu akifanya kazi moyoni mwa kila mmoja, basi kusingekuwa na haja ya kuhubiri. Wanapaswa kubaki kimya na kumwacha Mungu awaongoze wenye dhambi kwa njia hiyo, bila kutumia mahubiri wala wamisionari. Kama wanaamini hili, wanapaswa kuachana na mhubiri. Kwa nini mhubiri ahubiri kwamba roho ziweze kuongolewa, kama tu wataweza kuongolewa kupitia kazi ya moja kwa moja ya Roho Mtakatifu pasipokuwa na Neno? Kwa nini wawaite watu kuitikia wakati mafundisho yao ya kiimani hufundisha kwamba wamwombe Roho Mtakatifu kutenda na si mtu? Tazama mkanganyiko huu.

## 2. Kazi la Kanisa

Uwakala huu wa kupeleka Injili ulifanikiwa kiasi kwamba baada ya miaka michache Paulo aliweza kuandika, *"...Injili mliyosikia habari zake, iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu..."* (Wakolosai 1:23). Hii ilikamilishwa bila msaada wa njia za kisasa za usafiri, mashine

za uchapaji na redio. Mungu ametoa majukumu katika kanisa la kila mahali ya kuhubiri Injili:

A. Hekima ya Mungu inatakiwa ifahamike kanisani: *"ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho"* (Waefeso 3:10).

B. Roho Mtakatifu ameliamuru kanisa kushikilia ukweli: *"Lakini nikikawia, upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli"* (1 Timotheo 3:15).

C. Tunafundishwa kumtukuza Mungu kanisani: *"naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina"* (Waefeso 3:21).

D. Mwanadamu ameamriwa kufanya kazi zote za kidini katika jina la Bwana Yesu: *"Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye"* (Wakolosai 3:17).

### 3. Ushirikiano wa makanisa

Makanisa katika karne ya kwanza

yalikuwa yanajitegemea, lakini yalishirikiana katika kutimiza wajibu wao. Lugha ya Paulo iliyovuviwa inasema kwamba makanisa katika wingi wake yanaweza kutuma pesa ili kumsaidia mwinjlisti huyu. *"Nanyi pia, ninyi wenyewe mnajua, enyi Wafilipi, ya kuwa katika mwanzo wa Injili, nilipotoka Makedonia, hakuna kanisa lingine lililoshirikiana nami katika habari hii ya kutoa na kupokea, ila ninyi peke yenu. Kwa kuwa hata huko Thesalonike mliniletea msaada kwa mahitaji yangu, wala si mara moja"* (Wafilipi 4:15-16). Paulo alipokea mshahara (fedha) kutoka kwenye makanisa zaidi ya moja. Aliandika: *"Naliwanyang'anya makanisa mengine mali yao, nikitwaa posho langu ili niwahudumie ninyi"* (2 Wakorintho 11:8). Mafungu haya yanathibitisha kuwa makanisa yanaweza kushirikiana katika kuhubiri Injili. Kama kanisa ni dhaifu sana kiasi cha kushindwa kumsaidia mhubiri katika maeneo mengine, basi makanisa mengine mawili au matatu lazima yashirikiane kusaidia jitihada.

Kanisa la Kristo linaamini katika huduma ya kupeleka ujumbe kwa sababu Biblia inafundisha hivyo.

# 13

## SABABU YA KUMI NA TATU



**Kwa sababu linafundisha kwamba ufalme umekwisha anzishwa tayari na Kristo sasa ndiye mtawala**

## SABABU YA KUMI NA TATU

# Kwa sababu linafundisha kwamba ufalme umekwisha anzishwa tayari na Kristo sasa ndiye mtawala

### Utangulizi


Nadharia ya ufalme unaokuja pamoja na utawala wa Yesu juu ya dunia wa miaka elfu moja kwa kweli imesumbua watu wengi. Nadharia hii imevamia madhehebu mengi ya ulimwengu na imekuwa ikihubiriwa kwa wazi na wahubiri wao. Siwezi nikaunga mkono kanisa ambalo linapigia debe nadharia ya kiwendawazimu kama hiyo iliyotokana na fikra ya kubuni ya wanadamu. Inaitwa nadharia ya kabla ya miaka elfu moja; nadharia ambayo inasema wakati wa kuja kwa Yesu mara ya pili, hali ya mwanadamu ya kidunia haitaondolewa bali zama mpya au mpango mpya wa miaka elfu moja halisi utazinduliwa, wakati ambapo Kristo atatawala duniani huko Yerusalemu kwa miaka elfu moja halisi juu ya dunia ya watu

wakiwa bado wanaishi katika mwili. Bila shaka kuna baadhi ya vitu ambavyo ni vigumu kuvielewa, lakini sio vigumu kuelewa kwamba hii haiwezi kuwa kweli.

**1. Ufalme umekwisha anzishwa**

Kwanza haiwezi kuwa kweli kwa sababu ufalme umekwisha anzishwa tayari.

A. Danieli katika kukumbuka ndoto ya Nebkadneza na katika kutoa tafsiri ya ndoto ile, alisema, *"Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele... nao utasimama milele na milele"* (Danieli 2:44). Wafalme gani? Wafalme wa ufalme wa Rumi, kwa mujibu wa fasiri ya ndoto kwa uelewa wa historia takatifu na ile ya kidunia. Ufalme wa Mungu uliosimama imara na ambao hautaanguka ulikuwa uanzishwe wakati Warumi wanatawala




Inatumiwa kwa idhini ya; "World Video Bible School"{WVBS} yaani Shule ya Biblia kwa njia ya filamu ulimwengu. https://video.wvbs.org/

wanadamu.

B. Katika kipindi cha hao wafalme Yohana Mbatizaji alihubiri kwa kusema, *"Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia"* Mathayo 3:1-2).

C. Baada ya Yohana kuwekwa gerezani Yesu alihubiri, *"...Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia..."* (Marko 1:15).

D. Yesu baadaye aliwafundisha wanafunzi kuomba kwa ajili ya kuja kwa ufalme wa Mungu; *"Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje..."* (Mathayo 6:9-10).

E. Yesu alifundisha kwamba ufalme ungekuja wakati wa uhai wa baadhi ya mitume waliokuwepo wakati huo: *"... Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapouona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu"* (Marko 9:1). Ama ufalme umekwisha anzishwa ama je,kuna baadhi ya watu wanaoishi duniani leo ambao wana umri wa zaidi ya miaka elfu moja na mia tisa. Kwa kuwalinganisha, Methusela alikufa

akiwa katika umri wake wa ujana wa miaka mia tisa na sitini na tisa.

F. Wanafunzi walikuwa bado hawajaingia katika ufalme, maana Yesu alisema, *"akasema, Amin, nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni"* (Mathayo 18:3).

G. Katika kuwaagiza mitume sabini Yesu alisema, *"...Ufalme wa Mungu umewakaribia"* (Luka 10:9). Ulikuwa unaanzishwa hivi karibuni.

H. Lakini katika meza ya Bwana uanzishwaji wake ulikuwa bado ni wa wakati ujao. *"Maana nawaambia ya kwamba tangu sasa sinywi mazao ya mzabibu hata ufalme wa Mungu utakapokuja"* (Luka 22:18).

I. Sasa tunakwenda kwenye tarehe kamili ambayo ufalme ulianzishwa. Unakumbuka kwamba Yesu alisema katika Marko 9:1 kwamba ufalme utakuja na nguvu; unakumbuka tena kwamba nguvu hii itawajia mitume wakiwa Yerusalemu (Luka 24:49). Nguvu hii iliwajia mitume wakiwa Yerusalemu siku ya Pentekoste

kufuatia ufufuo wa Yesu (Matendo 2:1-4); kwa hiyo ufalme ulikuja siku ya Pentekoste. Petro alikuwa amepewa funguo za ufalme (Mathayo 16:19). Funguo ni ishara ya mamlaka. Kwa hiyo, Petro alikuwa amepewa mamlaka ya kufungua mlango wa ufalme au kuhubiri masharti ya kuweza kuingia. Petro alitumia mamlaka haya siku ya Pentekoste (Matendo 2) kwa kuhubiri masharti ya kuingia katika ufalme huu; alitumia funguo hizi na kufungua mlango kwa ajili ya kuingia katika ufalme kwa ajili ya kizazi chake na vizazi vyote kuingia. Watu elfu tatu walikuwa raia wa ufalme huu katika siku hiyo walipojikabidhi kwa Mungu kwa utii wao katika mpango mtakatifu (Injili). *"Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu"* (Matendo 2:41).

J. Paulo, miaka michache baada ya Pentekoste, aliandika kwamba walihamishwa na kuingia katika ufalme: *"Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo*

*lake"* (Wakolosai 1:13) Wasingeweza kuhamishwa na kuingizwa katika ufalme, kama usingekuwapo. Nadharia ya ufalme ujao inapingana na Paulo.

K. Upuuzi wa nadharia hii unaonekana tena unapoilinganisha na Waebrania 12:28: *"Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa …."* Ikiwa hauwezi kutetemeshwa, basi utasimama milele. Ikiwa tumepokea ufalme tayari ambao utasimama milele, basi hauwezi kukoma na kuacha ufalme mwingine ukashika hatamu. Hivyo, hakuna ufalme utakaoanzishwa hapo baadaye.

L. Ni upuuzi kuutazamia ufalme wa kimwili badala ya wa kiroho unaotegemewa kuanzishwa duniani. Ufalme umekwisha anzishwa na ni ufalme wa kiroho na wala sio wa kidunia: *"…Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu…"* (Yohana 18:36). Ni suala la kuhuzunisha kwamba mwanadamu ametunga nadharia ambayo inakanusha kikamilifu maneno haya ya Yesu.

## 2. Kiti cha enzi cha Yesu Kristo kipo mbinguni

Pili, nadharia ya kabla ya miaka elfu moja sio ya kimaaandiko kwa sababu kiti cha enzi cha Yesu Kristo kipo mbinguni:

A. Zekaria alisema kwamba Kristo *"... ataketi akimiliki katika kiti chake cha enzi..."* (Zekaria 6:13). Kristo sasa ameketi katika mkono wa kuume wa Mungu (Matendo 2:30-35). Kwa hiyo, kiti cha enzi cha Yesu Kristo kipo mkono wa kuume wa Mungu. Siyo sayari hii (dunia)!

B. Zekaria alitangaza kuwa Kristo angekuwa kuhani katika kiti chake cha enzi (Zekaria 6:13). Paulo alisema kwamba Kristo nikuhani mkuu aliyeko mbinguni (Waebrania 4:14). Kwa hiyo, Kiti cha enzi cha Yesu kipo mbinguni. Sio duniani!

C. Popote pale ambapo Yesu hawezi kuwa kuhani, hawezi kuwa na kiti chake cha enzi, kwa maana Kristo; *"...na kutakuwa na kuhani katika kiti chake cha enzi..."* (Zekaria 6:13). Kristo hawezi kuwa kuhani duniani: *"Kama angekuwa juu ya nchi, asingekuwa kuhani..."* (Waebrania 8:4). Kwa hiyo, haiwezekani kiti chake cha enzi kuwa

duniani. Ni lazima kiwe mbinguni!

**3. Kristo yupo katika kiti cha enzi cha Daudi**

Tatu, ukweli kwamba Kristo sasa yupo katika kiti cha enzi cha Daudi unakanusha nadharia hii.

A. Mungu aliahidi kwamba angempatia Kristo kiti cha enzi cha Daudi (Luka 1:32). Ahadi hii imetimizwa: *"Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi; yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu"* (Matendo 2:30-31). Kristo alifufuliwa ili kukaa katika kiti cha enzi cha Daudi: kwa hiyo sasa yupo katika kiti cha enzi cha Daudi. Kusema kwamba Yesu Kristo hayupo juu ya kiti cha enzi cha Daudi sasa ni kusema kwamba Yesu hakufufuka.

B. Zekaria anatuhabarisha kuhusu Kristo *"Naam, yeye atalijenga hekalu la BWANA; naye atauchukua huo*

*utukufu; ataketi akimiliki katika kiti chake cha enzi; na kutakuwa na kuhani katika kiti chake cha enzi; na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili"* (Zekaria 6:13). Kuketi na kutawala kungeweza kutokea kwa wakati mmoja na sambamba. Yesu alipoanza kuketi pia alianza kutawala na kinyume chake ni sawa. Kama tunaweza kuthibitisha kwamba sasa ameketi, tutaweza kuthibitisha kwamba sasa anatawala. Sikiliza ushahidi: *"Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake. Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia. Maana Daudi hakupanda mbinguni; bali yeye mwenyewe anasema, Bwana alimwambia Bwana wangu, Keti upande wa mkono wangu wa kuume. Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako"* (Matendo 2:32-35 Kristo sasa ameketi upande wa kuume wa Mungu; kwa hiyo, sasa anatawala katika kiti chake cha enzi.

## 4. Siku za mwisho

Nne, nadharia hii si ya kweli kwa sababu inafundisha kwamba hatuishi katika siku za mwisho. Kauli ya Petro katika siku ya Pentekoste, "Hizi ni siku za mwisho" inatosha kuthibitisha kuwa hii nadharia ni ya uongo kabisa. Wale wote wanaoshikiria nadharia hii (kwamba Yesu anatawala sasa katika ufalme wake wa kiroho, lakini wakiamini ufalme ujao wa kimwili wa miaka 1,000 duniani), wanaamini kwamba hatuishi siku za mwisho. Wanafundisha kwamba Kristo atazindua kipindi cha siku zinazoishia miaka elfu moja siku atakapokuja. Lakini Petro alisema, *"lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli,*
*Itakuwa siku za mwisho, ..."* (Matendo 2:16-17). Petro anasema hivi, siku ya Pentekosti, siku ambayo ufalme ulianzishwa ilikuwa ni siku za mwisho. Kwa hiyo, siku hizi zitakapokuwa zimekwisha hakutakuwa na siku nyingine zaidi; basi kutakuwa na siku ya milele. Wakati fulani hawa wana nadharia ya kabla ya miaka eflu moja wanakuwa wanahitilafiana na Roho

Mtakatifu!

### 5. 1 Wakorintho 15:23-25

Tano, upotovu (fikra isiyo sahihi) wa wananadharia ya kabla ya miaka elfu moja unaonekana tena unapoilinganisha na 1 Wakorintho 15:23-25. Tunapokuwa tukisoma fungu hili nitaweka maneno machache kwenye mabano kwa ajili ya msisitizo: *"Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja [ufufuo wakati wa kuja kwa Kristo]. Hapo ndipo mwisho, [siyo mwanzo wa miaka elfu moja] atakapompa Mungu Baba ufalme wake [siyo kuuanzisha]; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu [siyo kwamba anakwenda kuanza kutawala]. Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake"* [sio kuanza kutawala, bali kutawala sasa na kuendelea kutawala milele]. Mafungu haya yanathibitisha kwamba nadharia hii inahitilafiana na Biblia katika hoja nyingi.

**6. Dunia itachomwa moto**

Sita, Kristo hatatawala dunia hii pale atakapokuja (rudi mara ya pili), kwa sababu wakati huo dunia itakuwa imeungua: *"Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea"* (2 Petro 3:10). Wananadharia wa ufalme unaokuja watauweka wapi ufalme wa Kristo na kuweka kiti cha enzi? Siyo sayari hii (dunia)! Kwa sababu utayeyuka kwa moto mkali!

**7. Ufunuo 20:1-6. Haithibitishi nadharia ya kabla ya miaka elfu moja**

A. Fungu la kwanza la wananadharia ya kabla ya miaka elfu moja ni Ufunuo 20:1-6, lakini halithibitishi madai yao: Ukweli kwamba kitabu cha Ufunuo ni kitabu cha ishara na lugha ya mfano unafanya iwe vigumu kuelezea. Lakini angalia kile ambacho mafungu haya hayataji ambacho ni muhimu kuthibitisha madai ya nadharia hii:

(1) Kuja kwa Yesu mara ya pili.

(2) Kristo atatawala kimwili duniani.

(3) Ufufuo wa mwili.

(4) Hakitaji kwamba Kristo atakuwa katika ulimwengu huu tena.

(5) Hakisemi kwamba tutatawala pamoja naye - kinasema "*nao... [kama ilivyo katika mstari wa 4, wale "waliokatwa vichwa" kwa kumshuhudia Yesu] ...wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu.*"

B. Fungu hili (Ufunuo 20:1-6) limejaa lugha ya mfano, kama ifuatavyo: *"ufunguo wa kuzimu" (mst. 1) "mnyororo mkubwa mkononi mwake" (mst. 1) "akamfunga, akatia muhuri juu yake" (mst. 3) "viti vya enzi"* (mst. 4) *"nikaona roho zao"* (mst. 4) *"yule mnyama"* (mst. 4) *"sanamu yake"* (mst. 4) *"chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikono yao"* (mst. 4) *"ufufuo wa kwanza"* (mst. 6) *"mauti ya pili"* (mst. 6) *"watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu"* (mst. 6). Wananadharia wa kabla ya miaka elfu moja wamechagua mafungu haya yenye ishara nyingi - wanakiri

hili - na wakaamua kuchagua kirai, *"watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu"* na kusisitiza kwamba hiyo ni miaka halisi, hata kama inapingana na kauli halisi inayofundisha kinyume chake. Fikiria kwamba kwa nini wanatuambia miaka elfu moja inatakiwa ichukuliwe kama miaka halisi wakati maneno mengine katika mafungu haya yachukuliwe kwa lugha ya mfano.

C. Kuhusiana na mafungu haya, mwandishi wa kidini, Adam Clarke amesema katika maoni yake, "Ni njozi ngapi zimeshawahi kuonwa kuhusiana na mada hii, katika nyakati za kale na nyakati za sasa! Hiki, na kile kilichosemwa katika mafungu ya 3, 4 na 5 bila shaka kinarejea wakati ambapo ushawishi wa Shetani dhoofishwa kabisa, na kanisa la kweli la Mungu likifurahia mafanikio makubwa ambayo yatadumu kwa muda mrefu. Lakini haimaanishi kwamba namba, miaka elfu moja, ichukuliwe kama miaka halisi.

Inaweza kumaanisha kwamba kutakuwa na hali ya utulivu ya Ukristo

kwa muda mrefu; na kwamba roho ya Injili ulimwenguni kote itadumu, kwamba itaonekana kana kwamba Kristo alitawala duniani; Matokea yake kiuhalisia itakuwa kweli, kwa sababu roho yake itatawala katika mioyo ya watu; na katika kipindi hiki watakatifu waliokufa kwa kuchinjwa wanaelezwa kama waishio tena; na ushuhuda wao ukiwa umehuishwa, na ukweli ambao waliufia, na ambao ulithibitishwa kwa damu yao, ambayo sasa imeenea kila sehemu. Maneno "miaka elfu moja" ni nambari yenye maana maalum iliyojificha miongoni mwa Wayahudi." Kulingana na kwamba lugha yenyewe ni ya kiishara, Adam Clarke aliandika, "Huenda ikamaanisha"; hakuwa na uhakika.

Ni kinyume kabisa katika lugha yake ikilinganishwa na maneno ya nadharia ya kabla ya miaka eflu moja iliyojaa majivuno!

Nafasi haiwezi kuruhusu kuzama kwa kina katika sura hii kama mwandishi alivyotamani; kwa hiyo anapendekeza kusoma kitabu hiki cha Kiingereza kinachoongelea kwa kina mada hii,

kitabu ambacho amechukua baadhi ya mambo kwa ajili ya sura hii. Neal-Wallace Discussion On The Thousand Years Reign of Christ, kimechapishwa na the Gospel Advocate Co., Nashville, Tennessee (USA).

# 14

## SABABU YA KUMI NA NNE



## SABABU YA KUMI NA NNE

# Kwa sababu linatoa majibu ya kimaandiko kwa swali -- nifanye nini ili niweze kuokolewa?

### 1. Swali limechambuliwa

NINI." Hili neno linaonesha kuwa kuna kitu ambacho kinahitajika kutoka kwa mwanadamu ili aweze kuokolewa. Mtu anayeuliza swali hili anaelewa ukweli huu.

B. "Paswa." Neno hili linaonesha kwamba sio suala la nini "natakiwa", au nini "naweza," bali ni nini "napaswa" kufanya? Sio suala la kuchagua. Neno "paswa" linaonesha ulazima wa matakwa.

C. "Mimi." Sio kile ambacho Mungu, Kristo na Roho Mtakatifu anapaswa kufanya, bali ni "mimi" napaswa kufanya nini. Wote wanafahamu kwamba Utatu Mtakatifu una nafasi katika wokovu wa mwanadamu. Mungu, Kristo na Roho Mtakatifu wamefanya sehemu yao kwa

ukamilifu katika wokovu wa mwanadamu. Lakini muulizaji hatafuti kuelewa kazi ya Utatu Mtakatifu. Neno "mimi" katika swali linadokeza wajibu wa mtu mmoja mmoja katika ukombozi wa mwanadamu.

D. "Fanya." Sio kile ninachopaswa kupata, kufikiri, kuhisi au kuamini. Neno "fanya" linadokeza shughuli kwa upande wa mwanadamu ili aweze kuokolewa. Wakovu siyo "jambo la kukaa kufanyiwa" bila kufanya lolote, lakini ni "kutenda" ambapo tunafanya jambo fulani. Mungu anaokoa; mwanadamu bado anaweza kujiokoa kwa kutii Injili ya Mungu - nguvu ya Mungu iokoayo (Warumi 1:16; Matendo 2:40). Ondoa neno "fanya" kwenye Ukristo na utakuwa umeuharibu. Hutaweza kumsoma mtu aliyevuviwa akimwambia mwenye dhambi kwamba hakuna kitu chochote

anachoweza kufanya ili aweze kuokolewa.

E. “Kuokolewa.” Neno hili linadokeza lengo la kufuata masharti “Kuokolewa” ni kitu kinachotafutwa na muuliza swali. Neno hili vile vile laleta wazo kwamba tendo la wokovu wa msamaha nit endo lifanywalo na mwingine (na Mungu ambaye husamehe tunapotii). Lakini mtu anapaswa kufanya nini ili aokolewe na Baba wa Mbinguni?

**2. Njia ya uhakika ya kujibu swali hili**

A. Hakuna njia rahisi, ya hekima na ya uhakika ya kujibu swali hili zaidi ya kuigeukia Biblia na kusoma swali na jibu lililotolewa. Ikiwa swali linajirudia mara mia moja, basi soma kila swali na kila jibu lililotolewa. Hii inakuwa ni ya kimaandiko na ni sahihi bila shaka yoyote; zaidi inaweza kutoa ukweli wote juu ya mada hii. Lakini hatulioni swali hili likijirudia mara mia moja. Kimsingi, tunaliona mara nne tu katika Agano Jipya, na moja ya haya lilikuwa katika sheria ya Musa.

B. Swali hili mara ya kwanza liliulizwa na kijana tajiri alipokwenda kwa Yesu

(Marko 10:17). Yesu alimwelekeza kwenye amri kumi. Sheria za Musa zilikuwa bado zinafanya kazi wakati huu, kwa maana Kristo alikuwa bado hajafa na kuzigongomelea msalabani (Wakolosai 1:14). Ulikuwa ni wajibu wa Wayahudi kuifuata na kuitii. Kijana tajiri alipojibu kwamba amezishika amri zote tangu utoto wake, Yesu akasema, *"...Umepungukiwa na neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate"* (Marko 10:21). Sheria ya Musa ilikuwa bado haijatanguliwa na alipaswa kuitunza; pia alitakiwa aondokane na utajiri kitu ambacho kilikuwa kizuizi kwake; aidha alielekezwa kumfuata Kristo, kama walivyofanya wanafunzi, na angeweza kufundishwa vizuri kwa ajili ya kufanya kazi katika mpango wa Mungu uliokuwa unatarajiwa na muda wa kuja kwa Ukristo. Jibu hili lisingeweza kutolewa leo kwa sababu ilikuwa ni kabla ya Agano Jipya kuanza kazi kikamilifu (Waebrania 9:16-17).

Ni vema tuelewe kwamba Myahudi huyu *"...akaenda zake kwa huzuni;*

*kwa sababu alikuwa na mali nyingi"* (Mathayo 19:22). Alionekana ni mwaminifu katika kutaka kujua nini cha kufanya, lakini hakutaka kujua. Alikusudia kutii, ikiwa tu ingemfurahisha. Kwa bahati mbaya, wengi leo wapo kama hivyo. Kuna watu ambao wanadhani kwamba wanataka waokolewe, lakini kwa uhalisia hawataki.

C. Swali hili limerekodiwa mara tatu katika Matendo. Cha kushangaza, yametolewa majibu matatu tofauti. Kila jibu limetolewa kwa mamlaka ya Roho mtakatifu. Yote yanapaswa kufanyika. Hebu tuchunguze kila moja na tuone ufanano kwenye majibu haya yanayoonekana yanakinzana.

### 3. Wayahudi siku ya Pentekosti

A. Swali na jibu lake. Katika Matendo 2 tunasoma kushuka kwa Roho Mtakatifu kwa mitume. Lengo kufanya hivi lilikuwa ni kuwaongoza na kuwaelekeza katika kuhubiri Injili. Wayahudi kutoka katika kila taifa walikusanyika hapo. Kila mmoja aliposikia katika lugha yake, alijawa na

shauku kubwa. Baadhi walishangaa, lakini wengine walidhihaki kile walichokisikia na kukiacha kipite kwa kuwashutumu mitume kwamba *"wamelewa kwa mvinyo mpya."* Somo la Petro lilifuatiwa na shutuma hizi. Mahubiri ya neno la Mungu yalichoma mioyo yao na wakauliza, *"Tutendeje, ndugu zetu?"* (Matendo 2:37) Petro akajibu: *"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"* (Matendo 2:38). Kwa nini hawakuambiwa waamini? Kwa nini amri ya kuamini haipo katika fungu hili la maandiko? Kwa sababu walikuwa wamekwisha amini sana ndio maana walitaka kujua nini cha kufanya ili waweze kuokolewa. Petro aliwaambia hawa waamini watubu na kubatizwa ili wapate ondoleo la dhambi. Kwa mujibu wa Petro, ubatizo ni muhimu kama ilivyo kutubu. Neno "tubu" na neno "batiza" yote yanarejelea kwenye lengo la ondoleo la dhambi, kwa sababu yameunganishwa na neno "na." Haya maneno mawili lazima yawe pamoja ili kukamilisha kusudi moja la ondoleo la

dhambi. Ikiwa kutubu ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi, basi ndivyo ilivyo hata kwa ubatizo.

B. Wokovu unahitaji zaidi ya imani na badiliko la moyo. Sio tu kwamba waulizaji huko Yerusalemu waliamini, bali walibadili nia zao (badiliko la moyo wa kiroho). Mwanzoni mwa tukio waliwashutumu mitume kwamba walikuwa wamelewa. Baadaye, baada ya kusikia Injili, walitaka kujua nini cha kufanya ili waweze kuokolewa. Walikuwa wamekwisha amini na kubadili nia zao (badiliko la moyo wa kiroho), lakini walikuwa hawajaokolewa. Tuna uhakika na hili kwa sababu Petro hakusema, kama ambavyo wahubiri wengine wanavyosema, "Unachotakiwa kufanya ili uweze kuokolewa ni kuamini tu na kupata badiliko la moyo." Hapana! Petro aliwaambia watubu na kubatizwa ili wapate ondoleo la dhambi. Waliamini; walibadili nia zao (badiliko la moyo wa kiroho), lakini zaidi ya hili, walipaswa kutubu na kubatizwa ili dhambi zao ziweze kuondolewa.

**4. Sauli wa Tarso**

A. Sauli, ambaye baadaye alijulikana kama Paulo, anatambulishwa kama mtesaji. Mara ya kwanza anatajwa katika tukio la Stefano kupigwa mawe (Matendo 7:58; Matendo 8:1) Baadaye akajisema yeye mwenyewe, *"kwa habari ya juhudi, mwenye kuliudhi Kanisa"* (Wafilipi 3:6). Alikuwa mkali sana akijaribu kuziba vinywa vya Wakristo (Matendo 26:10-11). Ingawa alikuwa ni mtesaji asiyekuwa na msamaha, dhamiri yake ilikuwa dhahiri. Alisema, *"...Ndugu zangu, mimi kwa dhamiri safi kabisa nimeishi mbele za Mungu hata leo hivi"* (Matendo 23:1) Dhamiri yake ilikuwa haimuumizi, kwa sababu alikuwa anadhani anafanya kitu sahihi (Matendo 26:9). Huu ni ushahidi wa uhakika kwamba dhamiri ya mwanadamu haiwezi kukubaliwa kama mwongozo wa masuala ya kidini. Ili mradi tu mtu anafikiri kwamba yupo sahihi, basi dhamiri yake ni safi. Sauli alikuwa na dhamiri safi, akidhani kwamba alikuwa sahihi; lakini hakuwa sahihi. Hii ni kweli kwa watu wengi leo hii.

B. Swali la Sauli na jibu limetolewa.

Wakati Paulo akisafiri kuelekea Dameski kuwatesa Wakristo, na nuru ikamwangazia kote kote na akasikia sauti ya Yesu. Yesu hakumtokea Sauli ili kumsamehe, kama baadhi wanavyofikiri, bali kumfanya awe *"mtumishi na shahidi"* (Matendo 26:16). Tukio hili la kimiujiza halikumwokoa. Baada ya kuuliza nini cha kufanya, Yesu akamjibu, *"Lakini simama, uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda"* (Matendo 9:6). Ni wazi kwamba kuna kitu cha kufanya. Sauli alipungukiwa kitu. Sio imani; alikuwa amekwisha amini. Wala sio toba; alikuwa mwenye kujuta sana kiasi cha kutumia siku tatu akiwa amefunga na kuomba (Matendo 9:9,11), huku akisubiri kuambiwa kile anachotakiwa kufanya. Wala sio kwamba alikuwa hana moyo wa kubadilika, moyo wake ulikuwa umekwishabadilika kutoka kuwa na nia ya kuwatesa Wakristo na kuwa na nia ya kuwa Mkristo. Alikuwa amepungukiwa kitu, lakini sio imani, toba au badiliko la moyo. Hakuna mtu aliyewahi kuonesha ushahidi mkubwa wa haya zaidi ya Sauli. Alikuwa ameokolewa? Hapana! Dhambi zake

zilikuwa hazijafutwa (hazijaoshwa). Kristo alisema kwamba angeambiwa kile anachopaswa (ni lazima) kufanya. Kilikuwa ni nini? Anania alikwenda kwake na akasema, *"Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake"* (Matendo 22:16). Hili ni jibu la pili kwa swali. Iko wazi kwamba watu wanakosea kufikiria kwamba imani, toba na badiliko la moyo ndio mambo pekee ambayo Mungu anahitaji ili mtu aweze kuokolewa.

**5. Mlinzi wa Gereza**

Paulo na Sila walikuwa wafungwa katika gereza la Wafilipi. Wakati wa usiku wa manane kukatokea tetemeko. *"milango ikafunguka, vifungo vya wote vikalegezwa."* (Matendo 16:26) Mlinzi wa gereza *"akaamka"* Akaona milango ya gereza ipo wazi, akidhani kwamba wafungwa wametoroka, *"alifuta upanga, akataka kujiua."* Lakini Paulo aliuzuia mkono wake (alimzuia). Mlinzi wa gereza, akitetemeka kwa hofu, *"akawaangukia Paulo na Sila; kisha akawaleta nje akasema, Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate*

*kuokoka?"* (Matendo 16:29b-30). Huyu muuliza swali hakuwa muumini. Hakuna ushahidi kwamba alikuwa ameshawahi kusikia mahubiri ya Injili. Wakamwambia *"Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako"* (Matendo 16:31). Lakini kisa hiki hakiishii hapa: *"Wakamwambia neno la Bwana"* (Matendo 16:32). Kwa nini? Ili aweze kuamini (Warumi 10:17). Mlinzi wa gereza akatubu ( *"akawaosha mapigo yao"*) "na *"akabatizwa, yeye na watu wake wote wakati uo huo"* (Matendo 16:33). Sauli aliambiwa abatizwe ili aoshe dhambi zake (Matendo 22:16). Hakika, alimwambia mlinzi wa gereza abatizwe kwa sababu hiyo *"...Mungu hana upendeleo"* (Matendo 10:34).

**6. Majibu matatu tofauti kwa swali lile lile**

Tumekwisha soma majibu matatu tofauti kwa swali lile lile. Ufafanuzi sio mgumu:

A. Mlinzi wa gereza hakuwa muumini. Aliambiwa aamini. Walimhubiria kwa lengo la kuamini. Kisha akatubu na akabatizwa.

B. Watu siku ya Pentekosti waliamini. Kwa hiyo waliambiwa watubu na kubatizwa ili wapate ondoleo la dhambi.

C. Sauli, alipokuwa njiani kuelekea Dameski, alifanyika mtu wa imani na mwenye kutubu. Aliambiwa abatizwe na kupata ondoleo la dhambi.

D. Walipewa majibu tofauti, kwa sababu walikuwa katika maeneo tofauti katika njia ya kuelekea wokovuni. Lakini wote walifanya mambo yale yale na walisafiri katika njia moja. Kwa mfano, mtoto mmoja anauliza kuna umbali gani kutoka hapa hadi Dar es Salaam. Anaambiwa ni kilomita thelathini. Anaendesha hadi kilomita kumi kisha anauliza tena. Safari hii anaambiwa ni kilomita ishirini. Msafiri anaendesha gari hadi kilomita kumi zaidi na anauliza tena swali lile lile. Jibu linakuwa tofauti tena. Sasa anaambiwa ni kilomita kumi. Amepewa majibu matatu tofauti kwa swali lile lile. Hii ni sawa na swali, “Napaswa kufanya nini ili niokolewe?” Huyu mtu ambaye hajaamini alikuwa hajaanza safari kuelekea msamaha. Aliambiwa aamini; na, baada ya kuamini

alitubu na akabatizwa. Waamini hawakuambiwa waamini, bali kutubu na wabatizwe. Sauli, muumini mwenye toba, hakuambiwa aamini na atubu; aliambiwa abatizwe na kupata ondoleo la dhambi. Wote walisafiri kwenye njia moja. Wote waliongolewa sawa. Biblia haijipingi. Kwa kujibu swali hili kimaandiko, mtu anatakiwa kutoa majibu yote matatu yaliyotolewa na Roho Mtakatifu. Ikiwa huwezi kutia giza jua, kubadilisha upepo, au kuzuia mvua, basi huwezi kuibadili sheria hii ya Mungu.


04
BATIZWA
MK. 16:16; 1 PET. 3:21
03
KIRI IMANI
RUM. 10:9,10; MDO. 8:37
02
TUBU DHAMBI
MDO. 2:38; 17:30
01
AMINI INJILI
YN. 8:24; EBR. 11:6
00
SIKIA INJILI
RUM. 10:13–N.K.
Y. 6:44–45

# UCHUNGUZI NA HITIMISHO

# 15

## SABABU YA KUMI NA TANO



## SABABU YA KUMI NA TANO

# Kwa sababu linafundisha kwamba mtu anaokolewa kwa imani lakini sio kwa imani pekee

### 1. Imani ni nini?

IMANI ni kuamini kitu kama matokeo ya ushuhuda au ushahidi. Biblia ni kitabu cha ushuhuda, kilichotolewa ili kutengeneza imani katika moyo wa mwanadamu, *"...Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini..."* (Yohona 20:30-31). Watu ambao hawana ufunuo huu hawajui chochote kuhusu Kristo. Pale pasipo na ushuhuda au ushahidi, hakuwezi kuwapo imani.

A. Kwa maana pana, *"... imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana"* (Waebrania 11:1). Imani ni uhakika au msingi wa vitu vitarajiwavyo. Hili linatia nguvu matumaini yetu yote. "*Kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo*" maana yake ni kwamba

vitu hivyo vipo. Sijawahi kufika London, Paris au Mexico City, lakini nina uhakika kwamba miji hiyo ipo duniani. Sijawahi kumwona Kristo ana kwa ana, lakini nina uhakika kwamba alikufa na *"maana yu hai sikuzote."*



**2. Imani inapatikanaje**

Watu wengi wanaamini kwamba imani inapatikana kama matokeo ya kazi ya kimiujiza katika moyo wa mwanadamu. Kama hii ingekuwa ni kweli, watu wote wangeweza kuamini; maana *"Mungu hana upendeleo"* (Matendo 10:34) Kwa hiyo ukuaji wa imani hauwezi kuwa ni kazi ya wakala anayeshuka kutoka mbinguni ambaye anampata mmoja na kuwakosa wengine. Imani inakuja kwa watu wenye urazini, kwa njia ya urazini, kama tutakavyoona:

A. Maandiko matakatifu

yalitolewa kwa ajili ya kuijenga imani: *"Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo"* (Yohana 20:31).

B. Ombi la Kristo linafundisha kwamba tunamwamini yeye kupitia maneno ya mitume: *"Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao"* (Yohana 17:20).

C. Paulo anasema kwamba imani inakuja kupitia neno la Kristo: *"Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo"* (Warumi 10:17).

D. Petro anasema kwamba imani inategemea kusikia: *"Na baada ya hoja nyingi Petro akasimama, akawaambia, Ndugu zangu, ninyi mnajua ya kuwa tangu siku za kwanza Mungu alichagua miongoni mwenu ya kwamba Mataifa walisikie neno la Injili kwa kinywa changu, na kuliamini"* (Matendo 15:7).

E. Katika uongofu wa Wakorintho, kusikia neno kilikuwa ni kichocheo cha kuleta imani: *"... Wakorintho wengi waliposikia, waliamini, wakabatizwa"* (Matendo 18:8).

F. Kwamba malaika wanajua neno la Mungu linaleta imani, hii inashuhudiwa katika rekodi ya mazungumzo ya Kornelio: *"akatueleza jinsi alivyomwona malaika aliyesimama nyumbani mwake na kumwambia, Tuma watu kwenda Yafa ukamwite Simoni aitwaye Petro, atakayekuambia maneno ambayo yatakuokoa, wewe na nyumba yako yote."* (Matendo 11:13-14). Maneno yanamwezesha kuamini na kumwongoza kuokolewa.

G. Shetani anajua kwamba neno la Mungu ni msingi wa imani; kwa maana hiyo anafanya kazi kwa bidii kuliondoa mioyoni: *"...kisha huja Ibilisi akaliondoa hilo neno mioyoni mwao, wasije wakaamini na kuokoka"* (Luka 8:12).

Mafungu haya yanalifanya wazo hili kuwa dhahiri. Mungu, Kristo, Roho Mtakatifu, mitume, malaika, na Shetani wanajua kwamba imani inatokana na Neno.

## 3. Ulazima wa imani

Ulazima wa imani umesisitizwa kuanzia mwanzo wa Biblia hadi mwisho. Ni

muhimu sana kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Kukataa kukubali imani kama sharti la kuokolewa ni kuikataa Biblia, kwa sababu:

A. Moyo wa mwanadamu unatakaswa kwa imani (Matendo 15:9).

B. Mtu anahesabiwa haki kwa imani (Warumi 5:1).

C. Imani ni ya lazima kwa ajili ya kupata wokovu (Matendo 16:31; Marko 16:16).

D. *"Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona"* (2 Wakorintho 5:7). Katika maisha haya tunaenda kwa imani, lakini mbinguni tutaenenda kwa kuona. Tutaweza kuona vitu ambavyo kwa sasa havionekani (2 Wakorintho 4:16–18; 2 Wakorintho 5:6–8).

E. Maisha ya Kikristo ni kuishi kwa imani (Wagalatia 2:20).

F. *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza..."* (Mungu) (Waebrania 11:6).

G. *"Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi"* (Warumi 14:23). Kila tendo la utii na huduma katika dini ya Kikristo

vimejikita katika imani. Kuongozwa na maoni yako binafsi katika masuala ya kidini hakukubaliki mbele za Mungu. Lazima kuwepo na imani, vinginevyo tendo hilo sio sahihi.

**4. Fundisho la imani pekee linapingana na Biblia**

Nukuu hizo hapo juu, zinatilia mkazo umuhimu wa imani katika mpango wa Mungu. Kwa bahati mbaya watu wameongeza neno "pekee" au "tu" kwenye mafungu haya katika jitihada za kuthibitisha kuhesabiwa haki kwa imani pekee. Upotofu huu umesambaa sana, unafundishwa na makanisa mengi na watu wengi waaminifu wamepotoshwa nao. Hakuna mtu anayeona hitaji la imani kuliko mimi, lakini ili kufasiri mafungu haya yanayotaja imani ili kufundisha haki kwa imani pekee kungekuwa ni kupingana kabisa na mafungu mengine. Kwa mfano:

A. Yakobo anasema kwamba imani bila matendo, imekufa: *"Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake"* (Yakobo 2:17).

B. Ikiwa fundisho la "imani peke yake" lingekuwa kweli, basi ingewaokoa mashetani; maana *"... Mashetani nao waamini na kutetemeka"* (Yakobo 2:19).

C. *"Imani peke yake"* imetajwa katika Agano Jipya; lakini badala ya kufundisha kuhesabiwa haki kwa yenyewe, inafundisha kinyume kabisa: *"Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake"* (Yakobo 2:24). *"Si kwa imani peke yake."* Kila mtu anayefundisha kuhesabiwa haki kwa imani pekee anakwenda kinyume na Maandiko na anaukana ujumbe uliovuviwa wa Yakobo.

D. Yakobo anafafanua suala hili kwa kusema kwamba imani bila matendo imekufa kama maiti: *"Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa"* (Yakobo 2:26). Mtu anayefundisha wokovu kwa imani pekee anasambaza mafundisho mafu kama alivyo mtu mfu. Maneno ya Yakobo pekee yanapaswa kunyamazisha uenezaji wa fundisho

hili.

E. Watawala wengi waliamini, lakini hawakuokolewa: *"Walakini hata katika wakuu walikuwamo wengi waliomwamini; lakini kwa sababu ya Mafarisayo hawakumkiri, wasije wakatengwa na sinagogi. Kwa maana walipenda utukufu wa wanadamu kuliko utukufu wa Mungu"* (Yohana 12:42-43). Walimkana Kristo. Uangamivu wao ni hakika: *"Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni"* (Mathayo 10:33). Watawala waliamini; hata hivyo, hawakuokolewa. Walimkana Bwana wetu kwa sababu kulikuwa na kitu walichokipenda zaidi kuliko utukufu wake. Watu wengi leo wapo katika hali hiyo hiyo. Wanaamini, lakini wanapenda kazi za mwili kuliko utii.

### 5. Unaokolewa kwa imani pale unapotii imani

Mtu anaokolewa kwa imani: *"Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka..."* (Matendo 16:31). Lakini ni wakati gani ambapo

mtu anaokolewa kwa imani? Wakati anapoamini? Au pale imani inapotii? Tutaangalia:

A. Kuta za Yeriko zilianguka kwa imani sio wakati watu walipoamini, lakini baada ya kuwa wametii masharti ya kiungu waliyopewa: *"Kwa imani kuta za Yeriko zikaanguka, zilipokwisha kuzungukwa siku saba"* (Waebrania 11:30). Kama baadhi ya wahubiri wa "imani tu" au "imani pekee" wangelikuwapo kwa dhamiri njema lakini katika hali ya upofu, wakiwaongoza watu katika hali ya kutokutii, wangekuwa wamesema, "Hamna haja ya kufanya chochote bali kuamini; kaeni hapa tu na msubiri ili kuta zianguke," Je, zingeanguka? Hapana, hiyo isingekuwa imani katika Mungu. Imani katika Mungu ni kuamini kile Mungu anachosema. Aliwapatia masharti wanayotakiwa kuyafuata (Yoshua 6). Kufanya kinyume na kile Mungu alichoelekeza ni ushahidi tosha wa kukosa imani. Hili lilikuwa jaribio la imani yao. Waliamini na kuta zikaanguka kwa imani, lakini ni wakati gani? "Baada ya kuta kuwa zimezungukwa kwa siku saba." Mtu

anaweza kuiita ni dini inayotembea au kitu chochote anachopenda, lakini ukweli unabaki kwamba kuta hazikuanguka kwa imani hadi pale imani ilipotii.

B. Kwa imani Nuhu na Nyumba yake waliokolewa (Waebrania 11:7) — lakini ni wakati gani? Hilo ndilo swali. Tuchukulie leo kwamba Nuhu aliamini kama wahubiri wengi wa kimadhehebu leo, wakiwaambia watu, "imani pekee" au "imani tu" inaweza kuokoa." Hakuna haja ya kujenga safina.Ikiwa nitajenga, itaonekana kwamba, siamini kama Mungu anaweza kuniokoa." Ni kweli, wangekuwa wamepotea. Sio suala la Mungu anaweza kufanya nini, bali Mungu atafanya nini. *"Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake..."* (Waebrania 11:7). Aliokolewa kwa imani. Lakini ni wakati gani! Wakati ambapo imani ilitii!

C. Katika Hesabu 21 tunasoma kwamba wana wa Israeli waligongwa na nyoka wenye sumu kali. *"...Watu wengi*

*wakafa"* (Hesabu 21:6). Musa aliomba kwa Mungu kwa niaba ya watu wake. Njia ya kiungu waliyopewa kwa ajili ya kujinasua ilikuwa inategemea imani: *"...Jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi"* (Hesabu 21:8). Yalizungumzwa maneno ya wokovu. Watu waliokuwa wanakufa wangeweza kuokolewa. Kwa imani pekee? Hapana! Kwa kufuata masharti. Waliokolewa pale imani ilipotii. Endapo watu wa madhehebu ya kidini wa nyakati hizi wangekuwepo wakati huo, wangeweza kuhubiri: "Amini tu na utaokolewa. Wala huna haja ya kuangalia nyoka ya shaba. Hiyo ni dini ya nyoka na wokovu wa nyoka." Hivi ndivyo ambavyo wangesema wakati huo kwa sababu ndivyo wasemavyo leo: "Amini tu na utaokolewa." Pia wanasema, "Huna haja ya kubatizwa." Na tena, "Hiyo ni dini ya maji na wokovu wa maji." Kutazama nyoka ya shaba haukuwa wokovu wa nyoka; ulikuwa ni waokovu kwa njia ya imani. Wala ubatizo sio wokovu wa maji; ni wakovu kwa njia ya imani. Hakuna utata kuhusiana na wokovu kwa njia

ya imani. Swali ni kwamba, "Ni wakati gani mtu anaokolewa kwa imani?" Pale ambapo imani inafuata masharti!

**6. Mambo ambayo hupelekea kupata haki.**

Agano Jipya linatoa mambo ambayo hupelekea kupata haki. Tutaorodhesha baadhi ya mambo haya:

A. *"wanahesabiwa haki bure kwa neema yake..."* (Warumi 3:24) - Neema ya Mungu, ambayo ndiyo sababu ya kuhesabiwa haki (kitu kinachohamasisha).

B. *"na kwa yeye* (Kristo) *kila amwaminiye huhesabiwa haki..."* (Matendo 13:39) - Kristo, Mwokozi aliyetayari na mwenye hiari.

C. *"kuhesabiwa haki katika damu yake"* (Warumi 5:9) - Damu ya Yesu, kitu kilichopo / kipatikanacho.

D. *"mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo"* (1 Wakorintho 6:11) – Jina au mamlaka ya Bwana, kitu chenye nguvu.

E. *"kuhesabiwa haki itokayo katika imani"* (Warumi 5:1) - Imani ya mwanadamu, imani ya mwanadamu kwa Mungu.

F. *“huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake”* (Yakobo 2:24) - Matendo ya mwanadamu, mwitikio wa mwanadamu kwa Mungu.

Mfano unaoweza kusaidia kufafanua kweli hizi: Mtu anasikia kilio cha maumivu cha mtu anayezama majini jirani na nyumbani kwake. Akiwa ameguswa na neema na nia njema, anamtuma kijana wake kwenda kumwokoa huyo mtu. Kijana anamrushia kamba huyu mtu anayekwenda kuangamia na anamwambia kuishika ile kamba ili aweze kuokolewa. Huyu mtu anayezama anakamata kamba na anaokolewa. Kitu kinachohamasisha katika wokovu wake ni rehema na nia njema ya baba huyu ambaye alisikia kilio; mwana aliyekuwa tayari na mwenye hiari; tendo la kutupa kamba lilikuwa ni jambo lenye kupatikana / kuwapo; kamba ilikuwa ndiyo kitu chenye nguvu; Wakati mfamaji alipoamini kwamba mtu aliye nchi kavu angeweza kumsaidia kwa kamba, hii inaonesha imani ya mfamaji; Kushikilia (kukamata) kamba ilikuwa ni mwitikio

wa mfamaji.

Kwa hiyo, waliopotea katika dhambi wanahesabiwa haki kwa neema, kwa Kristo, kwa damu, kwa jina au mamlaka ya Kristo, kwa imani na kwa matendo. Mtu anapodhani kwamba imani ni jambo pekee katika wokovu wa mwanadamu, kwa kuacha mambo mengine, hakika atakuwa amepotoshwa. Imani ni sehemu ya mpango wa wokovu, lakini sio mpango mzima. Kila sehemu itendayo kazi katika kuhesabiwa haki kwa mwanadamu inahitajika (ni lazima) na haiwezi kuachwa.

## UCHUNGUZI NA HITIMISHO

## KWA NINI MIMI NI MSHIRIKA WA KANISA LA KRISTO

# 16

## SABABU YA KUMI NA SITA



## SABABU YA KUMI NA SITA

# Kwa sababu linafundisha kuwa mwanadamu ameokolewa kwa damu ya Kristo

### 1. Umuhimu wa damu katika uchumi wa kiuungu

Kwa nyakati zote za Biblia nguvu na ufanisi vimekuwa vikipatikana katika damu. Sadaka ya damu siku zote imekuwa sadaka ya uhai, *"kwani ile damu ndiyo uhai"* (Kumbukumbu La Torati 12:23). Katika kila kipindi cha Biblia, Mungu amekuwa akihitaji sadaka ambayo ni damu kwa asili. Hii pekee inasisitiza nguvu ya upatanisho ya damu; lakini tunajifunza zaidi.

A. Katika nyakati za awali (Mwanzo 4) Habili, *"akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake"* sadaka kwa Bwana. Ilikubaliwa. Lakini Kaini, kaka yake, *"akaleta mazao ya ardhi."* Ilikataliwa. Sadaka ya kwanza ya damu ilikuwa mfano wa damu ya Kristo iliyomwagika kwa ajili ya dhambi ya ulimwengu.

B. Ibrahimu mwaminifu, rafiki wa Mungu, alielewa umuhimu wa kutoa sadaka ya damu kwa Mungu. Wala hakusita alipoamriwa kumtoa Isaka sadaka, mtoto wa ahadi, kwenye madhabahu. Lakini alipokuwa anachukua kisu kumchinja kijana wake, malaika wa Yehova aliuzuia mkono wake. Kondoo aliyekamatwa kichakani alitolewa badala ya Isaka (Mwanzo 22:1-19).

C. Pasaka ni uthibitisho mwingine wa umuhimu wa damu katika mpango wa kiuungu. Wakati Yehova alipokwenda kuwaokoa wana wa Israeli na kuwaangamiza maadui zao (Wamisri), damu ya mwana kondoo katika "... kizingiti cha juu, na miimo miwili ya mlango..." (Kutoka 12:22) ilikuwa ni ishara ya usalama na ulinzi. Mungu aliahidi "*...nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu,*

*lisiwapate pigo lo lote likawaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri"* (Kutoka 12:13). Wana wa Israeli walitii na hakukuwa na kifo hata kimoja miongoni mwao. Katika hili tunapata onyo: Siku itakuja ambapo mjumbe wa uharibifu atakapokuja *"...katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu"* (2 Wathesalonike 1:7-8). Kama ilivyo kwa Wana wa Israeli walivyookolewa kwa damu ya mwana kondoo, ndivyo pia wale waliookolewa kwa damu ya Kristo watakavyookolewa siku ya mwisho. Ni furaha kiasi gani kusimama miongoni mwa wale "waliosafisha mavazi yao, na kuyafanya kuwa meupe katika damu ya Mwanakondoo."

D. Maagano kuwekwa muhuri kwa damu pia ni ushahidi kwamba damu ni muhimu katika mpango wa Mungu. Wana wa Israeli walionesha nia ya kutunza sheria ambazo Musa alizipokea kutoka kwa Mungu. Sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani zilipanda juu kwa Yehova, na damu za wanyama hawa zilikuwa zinatumika

kuweka muhuri kwenye agano kati ya Mungu na mwanadamu. Tuna ufafanuzi wa sherehe katika Kutoka 24:6-8. Mwandishi wa Waebrania alizungumzia juu ya sherehe hii katika (Waebrania 9:19-20).

E. Pia, hema na vyombo vyote vya huduma vilitakaswa na kuwekewa muhuri kwa damu ya wanyama: *"Na ile hema nayo na vyombo vyote vya ibada alivinyunyizia damu vivyo hivyo. Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo."* (Waebrania 9:21-22).

F. Mfumo wa Kiyahudi ni ule ambao sadaka ya wanyama ilikuwa inatolewa mara nyingi, lakini haikuweza kuondoa dhambi hata moja. *"Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao. Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na*

*dhambi? Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka. Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi"* (Waebrania 10:1-4). "Sadaka zile zile" ziliendelea kutolewa "mwaka hadi mwaka." Lakini damu iliyomwagika katika madhabahu ya Israeli isingeweza kuondoa dhambi hata moja. Lakini sasa, kusudi lake lilikuwa ni nini? Ilisogeza mbele tu uzito wa dhambi kwa mwaka mmoja kwa wakati. Muda ulipokwisha ilikuwa ni lazima kurudia tendo lile lile la kutoa sadaka katika mwaka mwingine. Huu ulikuwa ndio utaratibu chini ya sheria ya Musa. Damu ya mafahali na mbuzi isingeweza kuondoa dhambi. Lakini Wayahudi ambao walitoa damu ya wanyama kwa Mungu kwa uaminifu, hatimaye dhambi zao ziliondolewa kupitia damu ya thamani ya Kristo.

G. Katika Waebrania 9 na 10 tuna mlinganisho wa wazi kabisa kwa kumbukumbu ya damu za wanyama na damu ya Kristo:

   (1) Agano la kwanza lilikuwa limetolewa kwa damu, vile vile Agano Jipya lilitiwa muhuri kwa

damu.

(2) Wana wa Israeli walikuwa na mizigo ya dhambi ambayo ilisogezwa mbele kwa kutoa sadaka  mwaka hadi mwaka,  lakini tunaweza kusamehewa dhambi kwa damu ya Kristo.

(3) Kuhani Mkuu alikwenda Patakatifu pa Patakatifu kila mwaka akiwa na damu, *"atoayo kwa ajili ya nafsi yake na kwa dhambi za kutokujua za hao watu"*; hata hivyo Kristo Kuhani wetu Mkuu Mkamilifu, hakutoa damu ya wanyama kwa dhambi zake, maana hakuwa na dhambi, bali alitoa damu yake mwenyewe kwa dhambi za wanadamu, na kisha kwa faida ya damu hiyo alipaa mbinguni na kwenda mbele za Mungu kwa ajili yetu.

H. Hitimisho ni: *"... pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo"* (Waebrania 9:22).

**2. Damu ya Kristo ilimwagika kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu**

Katika Biblia hakuna kilichofundishwa kwa wazi zaidi kuliko sentensi hiyo

hapo juu. Kumbukumbu ilifanywa kwenye ukweli huu katika sehemu zilizotangulia, lakini sio kosa kuchunguza baadhi ya mafungu mengine mengi yanayofundisha wazo hili takatifu.

A. Isaya alitabiri kuponywa kwetu kwa kupigwa na kujeruhiwa kwake Kristo: *"Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na BWANA ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote"* (Isaya 53:5-6).

B. Zekaria alitabiri juu ya kufunguliwa chemchemi kwa dhambi: *"Katika siku hiyo watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, watafunguliwa chemchemi kwa dhambi na kwa unajisi."* (Zekaria 13:1). Unabii huu umetimizwa, na leo tunaimba (Tenzi namba 86, beti la kwanza):

 Damu imebubujika
 Ni ya Imanueli;
 Wakioga wenye taka,
 Husafiwa kweli.

C. Kristo, alipokuwa anaanzisha meza ya Bwana, alisema, *"...hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi"* (Mathayo 26:28).

D. Moja ya kweli za msingi za Injili ni *"...Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko..."* (1 Wakorintho 15:1-4).

E. Sikia maneno ya Paulo yanayohusiana na kuteswa kwa Yesu kwa ajili ya watu wengine: *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi"* (Warumi 5:8).

F. Wamataifa, *"...mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ile. Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani..." "...mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo"* (Waefeso 2:11-13).

G. Damu ilimwagika kwa kila kabila, daraja, lugha na rangi, kwa kila mwanadamu. katika kila ukingo na kila nchi. Yesu alionja *"...mauti kwa*

*ajili ya kila mtu"* (Waebrania 2:9). Katika ufunuo wa Yohana tunaambiwa, *"...kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa"* (Ufunuo 5:9)

H. Petro anasema kwamba mlikombolewa kwa damu ya Kristo: *"Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo"* (1 Petro 1:18-19).

I. Paulo pia anasema kwamba kwa damu ya Kristo tunao ukombozi wetu: *"Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake"* (Waefeso 1:7).

J. Maono ya Yohana juu ya jeshi la waliokombolewa yanajumuisha wale waliokuwa *"...wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo"* (Ufunuo 7:14).

### 3. Tunasafishwaje kwa damu

Watu wote wanaoiheshimu Biblia wanakubali kwamba mwenye dhambi anaokolewa kwa damu ya Kristo. Hakuna ugomvi hapa. Lakini ukweli kwamba Kristo alimwaga damu yake kwa watu wote (Waebrania 2:9) na kwamba wachache tu ndio watakaookolewa (Mathayo 7:13-14) ni ushahidi wa uhakika kwamba kuna kitu ambacho mwanadamu anatakiwa kukifanya ili aweze kupokea msamaha na mibaraka iliyopatikana kwa kumwagika damu ya Mwokozi. Swali ni kwamba: Ni kwa masharti gani damu inasafisha dhambi?

A. Katika Yohana 19:34 tunajifunza kwamba Yesu alimwaga damu katika kifo chake. Kwa sababu hii ni kweli, mwanadamu lazima aje katika kifo cha Kristo ili aweze kuifikia damu inayookoa. Je, hii inawezekana? Ndio! Paulo aliweka bayana njia ya kuingia katika kifo cha Yesu, mahali ambapo damu ilimwagika. Msikilize: *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya*

*ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima"* (Warumi 6:3-4). Ni kupitia ubatizo katika nyakati hizi ndipo mwanadamu anakutana na damu inayookoa. Kwa hiyo tusishangae Yesu alipotaja kuwa ubatizo kama sharti mojawapo la wokovu (Marko 16:16); kwamba Petro alisema ubatizo ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi (Matendo 2:38); kwamba Anania alimuamuru Paulo kubatizwa ili apate kuoshwa dhambi zake (Matendo 22:16). Hatushangazwi na kauli hizo tunapokumbuka kwamba muumini mwenye kutubu anabatizwa katika kifo cha Kristo, mahali ambapo damu ilimwagika, na hapo ndipo anakutana na nguvu ya kuoshwa (utakaso, kusamehe, kuondoa).

B. Katika Matendo 20:28 tumeambiwa sehemu ambamo damu inatakasa: *"Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake*

*mwenyewe."* Damu ya Yesu ilimwagika ili kununua kanisa la Mungu. Kwa hiyo, ni ukweli unaokubalika kwamba, ikiwa mwanadamu anaokolewa na kununuliwa kwa damu ya Kristo, ni lazima iwe kwa maadili ya muunganiko na uhusiano wake na kanisa lililonunuliwa kwa damu. Ukweli kwamba damu yote ya Yesu ilitumika kununua kanisa la Kristo ni ushahidi kwamba napaswa kuwa katika kanisa hilo ili niwe mnufaika wa damu. Mungu aliwaongeza watu wote walioamini, waliotubu, na kubatizwa ili kupata ondoleo la dhambi pekee katika kanisa lililonunuliwa kwa damu (Matendo 2:37-47). Kwa hiyo hata leo mtu anapaswa kuamini, kutubu na kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi ili kupata nguvu ya utakaso wa damu. Hili linapofanyika Mungu anamwongeza kanisani (kwenye mwili wake au katika ufalme wake). Sasa hapa ndipo anafurahia ahadi za wokovu; maana Paulo anasema kwamba, *"Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili"* (Waefeso 5:23).

C. Yohana ametufundisha jinsi damu inavyoweza kutusafisha na kutuweka safi: *“bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote”* (1 Yohana 1:7). Yohana alikuwa anazungumzia juu ya Wakristo, washirika wa kanisa lililonunuliwa kwa damu. Ikiwa washirika *“tukienenda nuruni”* wanafanya mapenzi ya Mungu, “*twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote”* yaani inaendelea kutusafisha na kutuweka safi. Ni ahadi nzuri ilioje, *“bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru”* ni sharti la kuipata ahadi hii. Yeyote anayesahau na kuiacha nuru ya mafundisho ya Kristo, kwa hiyo atakuwa ameingia katika kosa la, *“... kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema?”* (Waebrania 10:29).

# 17

## SABABU YA KUMI NA SABA



## SABABU YA KUMI NA SABA

# Kwa sababu linafundisha kwamba badiliko la moyo ni muhimu kwa wokovu wa mwanadamu

### 1. Utangulizi

DINI ambayo haigusi moyo na kuubadilisha sio dini iliyotolewa na Kristo. Moyo ni chanzo cha matendo tunayofanya. Ikiwa moyo umenajisiwa na dhambi matendo mabaya yanakuwa yanafuatia. *"Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati; wivi, ushuhuda wa uongo, na matukano"* (Mathayo 15:19). Dhambi hizi za machukizo zinaanza kufanywa moyoni. Ikiwa chemchemi itakuwa safi, mto pia utakuwa safi. Ikiwa moyo wa mwanadamu utakuwa safi, maisha yake pia yatakuwa safi. Hii inatosha kuthibitisha kuwa kuna ulazima wa badiliko la moyo. Hata hivyo, kuna madai kwamba washirika wa kanisa la Kristo, hawaamini katika badiliko la moyo. Msomaji anaweza kutambua kwamba madai haya

si ya kweli na si ya haki. Shitaka lao linakuja kutokana na ujinga kwa jinsi moyo ulivyo, mafundisho na matendo ya moyo, na namna unavyokuwa unabadilishwa. Shitaka lao linazaliwa na uovu. Mada hii ni miongoni mwa mada zilizojadiliwa sana na ambayo haijaelewaka kabisa. Lakini Mungu hapaswi kulaumiwa kwa ajili ya huu mkanganyiko, maana Maandiko yanaelezea mada hii kwa namna rahisi na ya kueleweka.

### 2. Asili ya mwanadamu ya pande mbili

Neno "moyo" linafasiriwa kama kiini (shina) cha uhai. Katika mwonekano wa nje wa moyo wa mwanadamu ni kiungo chenye mishipa iliyopo upande wa kushoto, inayowezesha mzunguko wa damu. Wengi wamezungumza kuhusu kiungo hiki cha nyama chenye kusukuma damu utadhani ndicho kilichokuwa mada ya Injili. Ni mara ngapi umeona watu

wakigusa upande wa kushoto wa kifua huku wakisema, “Ninauhisi hapa, Ninausikia hapa!” Wanazungumza juu ya badiliko la moyo kana kwamba ni moyo wa nyama uliopo kifuani. Kutokuelewa kwao kumetokea kwa kushindwa kuzingatia kwamba Biblia inafundisha kwamba mwanadamu ni kiumbe wa nje na wa ndani, wa kimwili na kiroho, na kwamba kila mmoja ana kiini (shina) cha uhai au moyo. Paulo, katika kuzungumzia asili ya pande mbili za mwanadamu, anasema, *“Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku”* (2 Wakorintho 4:16). Moyo wa mwili wa nje wa mwanadamu unapokuwa umechomwa (umevunjika), kifo kinafuatia. Tuna mfano wa hili katika 2 Samweli 18:14: *“...Akachukua vyemba vitatu mkononi mwake, akamchoma Absalomu moyoni, ....”*. Lakini moyo wa utu wa ndani au wa kiroho unapokuwa umechomwa (umevunjika), mtu wa nje anakuwa haguswi (inamaanisha kimwili tunabakia hai). Kwa mfano: *“Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na*

*mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?"* (Matendo 2:37). Mioyo ya hawa Wayahudi ilichomwa (ilivunjika) na wakaishi. Moyo wa Absalomu ulichomwa na vyemba na akafa. Mioyo hii miwili tofauti ilichomwa na silaha mbili tofauti. Ulikuwa ni moyo wa mtu wa ndani (moyo wa kiroho, siyo kiungo kinachosukuma damu) uliokuwa umeguswa na Injili. Ni dhahiri kwamba huu ndio moyo uliobadilika na kumfuata Mungu. Ukweli huu unaeleweka vizuri kwa kujifunza uchanganuzi wa moyo na unavyofanya kazi.

**3. Uchanganuzi na utendaji kazi wa moyo**

A. Moyo (wa kiroho) ni sehemu ya mwanadamu inayoitwa akili, ambayo:

(i) Inawaza. *"...Mbona mnawaza maovu mioyoni mwenu?"* (Mathayo 9:4)

(ii) Inafikiri. *"...Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu?"* (Marko 2:8)

(iii) Inaelewa. *"...Wakaelewa kwa mioyo yao..."* (Mathayo 13:15).

(iv) Inaamini. *"...kwa moyo mtu huamini..."* (Warumi 10:10).

Biblia inasema kwamba moyo wa mwanadamu unawaza, unafikiri, unaelewa na unaamini. Mungu anaiita sehemu hii ya mtu moyo, lakini mwanadamu anaiita akili. Kwa hiyo kile ambacho Biblia inakihusianisha na moyo, mwanadamu anakihusianisha na akili.

B. Moyo pia umehusishwa na sifa ya mwanadamu inayoitwa hisia ambao:

(i) Unadharau. *"...akamdharau moyoni mwake"* (2 Samweli 6:16).

(ii) Unatamani. *"Ndugu zangu, nitakayo sana moyoni mwangu, na dua yangu nimwombayo Mungu, ni kwa ajili yao, ili waokolewe"* (Warumi 10:1).

(iii) Unapenda. *"... Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote..."* (Mathayo 22:37).

(iv) Unatumaini. *"Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote..."* (Mithali 3:5).

Kwa hiyo kile ambacho Mungu anaita moyo, mwanadamu anakiita hisia. Tunaona kwamba moyo wa mwanadamu unakumbatia hisia, wepesi wa kuhisi au mihemko ya mwanadamu. Neno la Mungu linasema moyo

unadharau, unatamani, unapenda na unatumainia.

C. Moyo ni sifa ya mwanadamu inayoitwa nia, ambao:

(i) Unakusudia. *"...amekusudia moyoni mwake..."* (1 Wakorintho 7:37).

(ii) Unania. *"...mawazo na makusudi ya moyo"* (Waebrania 4:12).

(iii) Unalenga (Unakusudia) *"...waambatane na Bwana kwa kusudi la moyo"* (Matendo 11:23).

(iv) Unatii. *"... mliitii kwa mioyo yenu..."* (Warumi 6:17).

Kwa hiyo moyo unakusudia, unania, unalenga na unatii. Mwanadamu sifa hii anaiita nia, ridhaa, au mapenzi. Mungu anaiita moyo.

D. Moyo ni sehemu ya mwanadamu inayoitwa dhamiri, ambao:

(i) Unahukumu au hauhukumu. *"ikiwa mioyo yetu inatuhukumu; kwa maana Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu naye anajua yote. Wapenzi, mioyo yetu isipotuhukumu, tuna ujasiri kwa Mungu"* (1 Yohana 3:20-21).

Biblia inazungumzia juu ya sehemu ya mwanadamu inayohukumu au kuthibitisha. Mungu anaiita sehemu hii moyo. Mwanadamu anaiita dhamiri.

Mafungu hayo hapo juu yanaweka wazi kwamba moyo wa utu wa ndani, ni sehemu  ya mwanadamu ambayo inashikilia akili, hisia, nia na dhamiri. Hivi vyote vinaunda asili ya ndani ya mwanadamu.

**4. Badiliko la moyo**

A. Badiliko kamili linahitajika. Ikiwa moyo wa mwanadamu unashikilia akili, hisia, nia na dhamiri, hakuwezi kuwepo na badiliko kamili hadi pale kila sehemu itakapokuwa imebadilika. Kila sehemu ni lazima ibadilike ili moyo wote wa mwanadamu ubadilike. Moyo unatakiwa ubadilike kutoka katika mawazo maovu kwenda katika mawazo mema, kutoka fikra ovu kwenda fikra njema, kutoka katika ujinga wa kutojua neno la Mungu kwenda kupata maarifa ya neno lake, kutoka kutokuamini kwenda kuamini, kutoka kuwa na dharau kwenda kuwa na shauku, kutoka kutotamani kufanya

mema kwenda kutamani kufanya mema, kutoka kupenda ulimwengu kwenda kumpenda Bwana, kutoka kutumainia vitu vya kidunia kuanza kumtumainia Mungu, kutoka kuwa na makusudi yasiyokuwa ya haki kwenda kuwa na makusudi ya haki, kutoka kuwa na makusudi yasiyokuwa ya kimaandiko kwenda kuwa na makusudi ya kimaandiko, kutoka kutotii kwenda kutiii, na kutoka kuwa na dhamiri ya hukumu kwenda kuwa na dhamiri inayoridhia. Hili ndilo badiliko la moyo ambalo ni muhimu sana kwa wakovu wa mwanadamu.

B. Moyo wa mwanadamu unabadilikaje?

(1) Akili inabadilishwa kwa ushahidi au ushuhuda. Inabadilika kutoka hali moja kwenda nyingine kulingana na ushahidi uliotolewa. Mawazo, fikra, uelewa na imani ya Tomaso haikubadilika hadi Yesu alipojitokeza kwake na kusema, *"...Lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu; ulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu, wala usiwe asiyeamini, bali aaminiye"* (27) Kisha Tomaso akajibu, *"...Bwana wangu na Mungu wangu!..."* (Yohana 20:24-

29). Angalia mfano mwingine: Sio muda mrefu umepita, baba na mama wa baharia walipokea ujumbe kutoka Washington kwamba kijana wao ameuawa katika shambulio la bandari ya Pearl, Mawazo yao, fikra, uelewa na imani vilibadilika vyote. Majuma machache baadaye wakapokea ujumbe kutoka mamlaka ile ile wakisema kwamba ujumbe wa kwanza sio sahihi na kijana wao ni mzima. Ushuhuda huu ulizalisha badiliko jingine katika akili. Kwa hiyo ni rahisi kuona kwamba ushahidi au ushuhuda unadhibiti akili. Neno la Mungu ni ushuhuda ambao Mungu ameutoa ili kuibadilisha akili ya mwanadamu. *"hizi zimeandikwa ili mpate kuamini"* (Yohana 20:31). *"Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo"* (Warumi 10:17).

(2) Hisia zinabadilika kwa imani katika ushuhuda uliotolewa. Kuamini ushuhuda huleta badiliko katika hisia. Matwezo, shauku, upendo na tumaini ni matokeo ya vitu vilivyoaminiwa. Baba na mama tuliowazungumzia hapo juu furaha yao ilibadilika kuwa

huzuni na kinyume chake kwa sababu ya kitu walichokiamini. Ni imani katika ushuhuda wa Kristo ambao unazalisha badiliko katika hisia za mdhambi kutoka kuwa na shauku ya kufanya dhambi na kuwa na shauku ya kufanya mema, kutoka kupenda ulimwengu na kumpenda Kristo, na kutoka kutumainia vitu vya dunia na kumtumainia Bwana.

(3) Ridhaa inabadilishwa na nia iliyozalishwa na imani. Sauli aliamua, alikusudia, na kudhamiria kutomtii Kristo, akifikiri kwamba Yesu alikuwa laghai. Tunamwona huyu mtesaji akiwa na dhamira thabiti akisafiri barabarani kwenda Dameski ili kuwatesa Wakristo. Sauli hakuwa na Agano Jipya kwa ajili ya kusoma, lakini neno la mdomo la Kristo lilibadilisha moyo wake kutoka kutokuamini na kuamini. Alipoambiwa kubatizwa ili aondolewe dhambi zake (Matendo 22:16), alitii bila kupinga. Na moyo usiotii ulibadilishwa kwa nia iliyozalishwa na imani: Nia ya imani katika wema wa Kristo (Warumi 2:4); Nia ya kuamini katika thawabu ya mwenye kutii (Waebrania 5:9); Nia ya kuamini katika hukumu kwa

wasiotii (Ufunuo 20:15). Kila nia moja inatuhamasisha. Dhambi za Sauli ziliondolewa kupitia tendo la utii. Moyo wa utii ni muhimu kwa wokovu wa mwanadamu. Mtu anakuwa huru kutoka katika dhambi na kuwa mtumishi wa haki kwa kutii kutoka moyoni: *"... maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki"* (Warumi 6:17-18). Kiwango cha imani kinachoongoza katika wokovu ni imani kwa moyo wote, kinachopelekea utii kamili kutoka moyoni. Mtu hawezi kuwa mtumwa wa Kristo hadi atakapotii kutoka moyoni. Hakuna moyo ulio sahihi mpaka uwe moyo wa utii.

(4) Dhamiri inabadilishwa kwa imani kwa kufanya kitu sahihi. Ikiwa mtu anaelewa na kuamini kile Kristo alichoamuru, hawezi kuwa na dhamiri inayothibitisha hadi atakapoifanya. Kwa mfano, ubatizo ni amri, (Matendo 10:48); Kwa sababu hii ni kweli, ikiwa mtu anaelewa na anaamini kwamba

ubatizo ni amri inayopaswa kutiiwa ili kupata ondoleo la dhambi (Matendo 2:38), basi hawezi kuwa na dhamiri safi hadi atakapobatizwa: *"Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo"* (1 Petro 3:21). Ni imani katika kufanya yaliyo sahihi, kutii amri za Mungu, ndiko kunakobadilisha dhamiri ihukumuyo. Dhamiri haiumizi hadi pale mtu atakapoamini kwamba amefanya kitu kisicho sahihi. Hii ndiyo sababu watu wengi wanaoishi katika dhambi na kutomtii Mungu wana dhamiri ya wazi. Hawajui au hawaamini kwamba wanaishi katika kutomtii Mungu. Hii ni sawa na kwa Sauli. Kwa dhimiri safi kabisa (Matendo 23:1), aliwatesa Wakristo, na wala hakuwa na dhamiri ihukumuyo hadi alipoujua na kuuamini ukweli. Dhamiri ya Sauli ilibadilishwa kutoka kwenye hali ya kuhukumu kwenda kwenye hali ya kukubaliwa kutokana na utii wake kwa Kristo.

Pale ambapo akili, hisia, nia na dhamiri

ya mwanadamu inabadilishwa, moyo wote wa mwanadamu unabadilika. Ni dhahiri kwamba baadhi ya watu ambao wanazungumzia juu ya "dini ya kuguswa moyo" si watu waliobadilika mioyo katika namna ya kimaandiko. Wanahubiri badiliko la juu juu tu la moyo, wakiwaambia watu kwamba imani pekee, akili iliyobadilika, ndicho kitu muhimu pekee katika wokovu wa mwanadamu. Lakini kuongoka na kumfuata Mungu kunahitaji badiliko la moyo wote (badiliko la moyo wote wa kibiblia). Hiyo inajumuisha badiliko la akili, hisia, nia na dhamiri. Ona, ni rahisi kuona kuwa ni kundi gani linalohubiri dini ya moyo wote.

# 18

## SABABU YA KUMI NA NANE



### Kwa sababu ya mafundisho na taratibu zake kuhusiana na maombi

## SABABU YA KUMI NA NANE

# Kwa sababu ya mafundisho na taratibu zake kuhusiana na maombi

### 1. Utangulizi

Wakisasa miongoni mwetu hawasisitizi (hitaji, tegemeo, au mkazo) maombi. Hii ni kwa sababu ya imani yao ndogo. Maombi ni kipimo kikubwa cha imani kwa Mungu na neno lake. Shughuli au tendo la sala kwa mtu asiye na imani ni kama kilio cha mtu aliyeko jangwani ambapo hakuna mtu atakayemsikia. Hata hivyo, shughuli au tendo kwa mtu wa imani ni utambulisho kwa Mungu aliye na uwezo wa kujibu. Hata hivyo wanadini wengi, wanaosisitiza maombi - wanafundisha kuhusu maombi, wanazungumza kuhusu maombi, wanaomba nyumbani, wanaomba katika ibada ya pamoja, wanaomba pamoja na waombolezaji - hawajajifunza kwamba Mungu ameanzisha masharti fulani kwa ajili ya mtu kuyafuata ili kwamba maombi yake

yaweze kujibiwa.

**2. Kanisa la karne ya kwanza lilikuwa ni kanisa la maombi**

A. Kwa kuzungumzia washiriki elfu tatu waliongezwa katika kanisa, Luka anasema, *"Wakawa wakidumu ... katika kusali"* (Matendo 2:41,42).

B. Kundi la Wakristo, waliounganishwa na Petro na Yohana waliotishiwa na baraza la Wayahudi, *"... wakampazia Mungu sauti zao kwa moyo mmoja..."* (Matendo 4:24).

C. Wakati huo mitume kumi na wawili walitoa maelekezo kuhusiana na watu watakaochaguliwa kuhudumu mezani, *"na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno"* (Matendo 6:4).

D. Petro alipowekwa gerezani na Herode *"...nalo kanisa likamwomba Mungu kwa juhudi kwa ajili yake"* (Matendo 12:5).

E. Paulo na Sila, wakati wakiwa wafungwa huko Filipi wakati wa usiku wa manane, waliomba na kumwimbia Mungu nyimbo (Matendo 16:25).

F. Wakati Paulo alipokuwa anahitimisha hotuba yake kwa wazee wa Efeso, *"... akapiga magoti, akaomba pamoja nao wote"* (Matendo 20:36).

G. Kanisa lote huko Tiro lilipiga magoti ufukweni na kusali wakimuaga Paulo na wenzake (Matendo 21:4–5).

H. Makanisa yaliaswa kuomba:

(1) Kwa watakatifu huko Rumi: *"...katika kusali, mkidumu"* (Warumi 12:12).

(2) Kwa kanisa la Mungu huko Korintho: *"... ili mpate faragha kwa kusali..."* (1 Wakorintho 7:5).

(3) Kwa watakatifu na waaminifu katika Kristo Yesu huko Efeso: *"kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote"* (Waefeso 6:18).

(4) Kwa kanisa la Filipi: *"Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na*

*kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu"* (Wafilipi 4:6).

(5) Kwa watakatifu na ndugu waaminifu katika Kristo huko Kolosai: *"Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani"* (Wakolosai 4:2).

(6) Kwa kanisa la Mungu huko Thesalonike: *"ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu"* (1 Wathesalonike 5:17-18). Kilichoendelea ni ushahidi kwamba kanisa la Kristo kuanzia mwanzo lilikuwa ni taasisi inayosali. Kwa hiyo, hakuna kundi la watu linaloweza kuitwa kanisa la mitume ikiwa chombo hicho hakina maombi wala kufuata maandiko katika shughuli zake.

I. Yesu, mwanzilishi wa kanisa, aliamini katika maombi na aliomba sana:

(1) Mwanzoni mwa huduma yake ya hadhara, mara baada ya kubatizwa kwake, aliomba (Luka 3:21).

(2) Usiku kabla Yesu hajawachagua thenashara *"... akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika*

*kumwomba Mungu"* (Luka 6:12).

(3) *"Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba. Na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake"* (Mathayo 14:23).

(4) *"Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko"* (Marko 1:35).

(5) *"Lakini yeye alikuwa akijiepua, akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba"* (Luka 5:16).

(6) Katika ujumbe wake wa hitimisho alipokuwa anaachana na mitume aliinua macho yake juu na akaomba (Yohana 17).

(7) Muda mfupi kabla ya kukamatwa kwa ajili ya kuteswa aliwachukua Petro, Yakobo na Yohana na wakaenda katika bustani ya Gethsemane na wakaomba mara tatu (Mathayo 26:36-44).

(8) Alipokuwa anakufa msalabani aliomba (Luka 23:34-46).

Kwa kuwa Yesu, mwanzilishi wa kanisa,

alitumia muda mwingi katika maombi, ni dhahiri kwamba ikiwa tunahitaji kuwa washiriki wa kweli wa kanisa hili nasi pia tunapaswa tudumu katika maombi. Hakika mtu asiyekuwa na maombi hawezi kuwa mfuasi wake yeye aliyeomba sana.

### 3. Jibu la Mungu katika maombi ni la masharti

Taasisi nyingi za kidini ambazo zimekuwa zikisisitiza umuhimu wa maombi hazijawahi kuhubiri juu ya masharti mahususi, ya kimaandiko ambayo watu wanatakiwa kuyafuata kabla ombi lao halijajibiwa. Tusisahau kwamba mtu anaweza kuomba na asiweze kusikilizwa. Yakobo alisema, *"Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu"* (Yakobo 4:3). Sio wote wanaoomba wanasikilizwa, lakini wote wangesikilizwa kama kusingekuwepo na masharti. Zingatia masharti yafuatayo ya ombi linalokubalika:

A. Kuwa mwenye haki. *"Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na*

*masikio yake husikiliza maombi yao..."* (1 Petro 3:12).

B. Tunza amri za Mungu. *"...lo lote tuombalo, twalipokea kwake, kwa kuwa twazishika amri zake, na kuyatenda yapendezayo machoni pake"* (1 Yohana 3:22). Kinyume cha hili ni kwamba maombi ya wale ambao hawatunzi amri za Mungu hayatasikilizwa.

C. Omba kwa imani. *"Ila na aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku. Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana"* (Yakabo 1:6-7). Ni lazima tumwamini Mungu na tuamini kwamba atatupatia kile alichoahidi kutupatia. Ikiwa tunaomba vitu ambavyo Mungu hakuahidi kutupatia, tunaomba pasipo imani; maana imani huja kwa neno la Kristo (Warumi 10:17).

D. Omba katika Jina la Yesu. *"Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya"* (Yohana

14:13-14).

E. Omba kulingana (kufuatana) na mapenzi ya Mungu. *"Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia"* (1 Yohana 5:14). Lakini tukiomba sawa sawa na mapenzi yetu badala ya mapenzi ya Mungu, hatutapokea.

F. Kuwa na roho ya kusamehe. *"Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu"* (Mathayo 6:15). Mungu hatajibu maombi yako kama hutawasamehe wale waliokukosea.

G. Lazima uwe katika hali nzuri ya kiroho. *"Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa"* (Yohana 15:7). Mioyo yetu lazima ikae na neno la Kristo ili maombi yetu yaweze kujibiwa.

H. Omba ukiwa na kusudi jema akilini mwako. *"Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu"* (Yakobo 4:3). Maombi yajayo kutokana na nia

mbaya hayatasikiwa.

**4. Kuomba kwa ajili ya wenye dhambi**

A. Kuomba kwa ajili ya wenye dhambi ni desturi iliyoenea na inahitaji kujifunza kwingi. Tumeona kwamba mtu anatakiwa kufuata masharti fulani ya kiroho ili maombi yake yaweze kukubalika. Je, watu hao wanalazimika kuwaombea wenye dhambi?

(1) Yesu aliwaombea genge la wenye dhambi waliomsulubisha: *"... Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo..."* (Luka 23:34).

(2) Yesu alitufundisha kuomba kwa ajili ya wenye dhambi, akisema *"lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi"* (Mathayo 5:44).

(3) Paulo aliomba kwa ajili ya Israeli: *"Ndugu zangu, nitakayo sana moyoni mwangu, na dua yangu nimwombayo Mungu, ni kwa ajili yao, ili waokolewe"* (Warumi 10:1).

Tumeona kwamba ni jambo la kimaandiko kuw aombea wenye dhambi. Kwa kufanya hivyo, tunafuata

mafundisho ya Yesu na mifano ya Yesu na Paulo. Hili linatupeleka katika swali jingine na kipengele kingine cha kujifunza.

B. Je, tuidhinishe mfumo wa dini ya waombolezaji? Je, watu ambao hawajawahi kupata wokovu (wenye dhambi) wamuombe Mungu awape wokovu moja kwa moja?

(1) Na tueleze: Mfumo utumiao kitu kiitwacho “fomu ya waombolezaji” (benchi la waliaji au huzuni) ni ule wa kuombea wadhambi ili waokolewe bila kutii masharti ya wokovu. Hii ni desturi sehemu nyingi. Wenye dhambi wanaojutia wanaitwa kwenye “fomu ya waombolezaji” ambapo maombi marefu na ya dhati yanatolewa ili kwamba waweze kuokolewa katika hali zao za sasa bila kutii sheria ya msamaha. Je, Mungu atatenda? Je, Mungu ataweka kando sheria na mapenzi yake ili kutii mapenzi yao?

(2) Katika kujibu swali hili tutazingatia kanuni ifuatayo ya utendaji ambayo inafanya kazi katika nyanja zote za kimwili na kiroho. Mungu anapoweka sheria ambayo kwayo mtu anatakiwa

kuifuata na kupokea baraka, ni chukizo kuomba mibaraka bila kutii sheria, Suleimani alisema *"Yeye aligeuzaye sikio lake asiisikie sheria, Hata sala yake ni chukizo"* (Mithali 28:9).

Kufuata sheria ya asili mkulima anaweza kuvuna mazao. Sheria ya asili kwa ajili ya kuvuna mavuno ni hii: Lima ardhi, iandae kwa ajili ya kupanda mbegu, panda mbegu na palilia mazao. Chukulia kwamba mkulima anataka Mungu ampatie mavuno bila kufuata sheria hii, na anamwomba Mungu ampatie mavuno bila kufuata masharti yaliyowekwa. Je, Mungu atampatia? Hapana! Sio tu kwamba ombi kama hilo halitajibiwa, bali kimsingi litakuwa ni chukizo. Ikiwa anataka mazao basi, na aitii sheria. Sote ni lazima tuombe, - *"Utupe leo riziki yetu"* (Mathayo 6:11). Sote pia tufuate masharti ya upandaji na uvunaji ili kupata mavuno.

(3) Je Mungu ana sheria ya Msamaha? Ikiwa Mungu ana sheria ya msamaha ambayo kwayo mtu anaweza kuifuata na kuokolewa, basi haina maana kabisa kumwomba Mungu kumwokoa mtu kabla hajafuata sheria hiyo. Hii

itakuwa ni machukizo (Mithali 28:9). Ombi hili lingekuwa la kumwomba Mungu aweke pembeni sheria yake na kupuuzia matakwa yake na kutii matakwa ya mwanadamu. Mungu ana sheria ya msamaha kwa walio nje ya Bwana; inawataka kuamini (Waebrania 11:6), watubu dhambi zao (Luka 13:3), na kukiri imani katika Kristo kama Mwana wa Mungu (Mathayo 10:32; Matendo 8:37), na kubatizwa ili kupata ondoleo la dhambi au kwamba dhambi ziweze kuondolewa (Matendo 2:38; Matendo 22:16). Mfumo wa dini wa "fomu ya waombolezaji" hauwaambii wenye dhambi masharti ya wokovu na kuwasisitiza kuyafuata unasisitiza mdhambi huyu kuja katika "fomu ya waombolezaji" kwa kuikataa sheria ya Mungu ya msamaha  na kuomba kwamba Mungu amwokoe katika kutotii kwake sheria ya Mungu. Ombi kama hilo ni sawa na kusema, "Eh Mungu, mapenzi yako yasitimizwe, bali mapenzi yangu yatimizwe." Hii sio ya kimaandiko kabisa! Hatushangai kwamba hakuna mfano wowote katika Maandiko ya dhambi zao kuondolewa na muombaji. Wadhambi walio nje

ya Bwana, waliokuwa wanahitaji kujua nini cha kufanya ili waokolewe, hawakuweza kualikwa katika "fomu la waombolezaji." Hii ni fomu ambayo wangeitumia katika kulia na kuomba ili dhambi zao zisamehewe na Mungu angewaokoa pale pale. (Angalia Sura ya Kumi na Nne ili kujua kile walichoambiwa.)

C. Vipi kuhusu ombi la Yesu kwa ajili ya wenye dhambi?

(1) Yesu alipokuwa anakufa msalabani aliomba, *"... Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo..."* (Luka 23:34). Yesu siku zote alitenda mapenzi ya Mungu; kwa hiyo tuna uhakika kwamba hakumuomba Mungu kuwaokoa hawa wadhambi kwa kukiuka sheria takatifu. Elewa kwamba, Yesu hakusema, "Baba, wasamehe sasa, sasa hivi, wakati huu huu." Tunajua kwamba Yesu hakuwaombea ili waokolewe (katika sekunde au dakika hiyo hiyo), kwa kuwa ombi halikujibiwa wakati huo huo.

(2) Je, ombi lilijibiwa wakati gani? Katika siku ya Pentekoste, siku hamsini baada ya ombi, lilikuwa

bado halijajibiwa. Ushahidi ni huu hapa: Mungu anaposamehe dhambi, hazikumbuki kabisa milele (Waebrania 10:17). Mungu hasamehi dhambi halafu baadaye akiibua tena kwa kumkumbusha mdhambi. Katika siku ya Pentekosti Petro aliwashitaki watu hawa kwa mauaji ya Kristo, akisema, *"Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo"* (Matendo 2:36). Ukweli kwamba shitaka hili limeletwa dhidi yao ni ushahidi kwamba walikuwa bado hawaja samehewa: kama wangekuwa wamekwisha samehewa, Mungu asingeikumbuka dhambi yao milele. Hata hivyo, katika siku hii waliamini kama matokeo ya kusikiliza injili na wakataka kujua nini cha kufanya. Petro aliwaambia watubu na wabatizwe ili wapate ondoleo la dhambi (Matendo 2:38). Watu elfu tatu walifanya hivi na Bwana akawaongeza katika kanisa (Matendo 2:41,47).

Kwa hiyo wakaokolewa kwa kutii sheria ya msamaha, na ombi la Yesu  likawa

limejibiwa. Kwa mtazamo wa ukweli hapo juu ni dhahiri kwamba Mungu hatajibu maombi yetu kwa niaba ya wenye dhambi hadi watakapotii sheria ya msamaha. Ni sahihi kiasi gani ombi la kimaandiko! Na ni bure kiasi gani kwa kila ombi linalopingana na mapenzi ya Mungu!

# 19

## SABABU YA KUMI NA TISA



## SABABU YA KUMI NA TISA

# Kwa sababu linafundisha na kusimamia ubatizo wa kwenye Biblia

### 1. Utangulizi

Idadi kubwa ya madhehebu yanatenda kitu wakiitacho ubaptizo [isipokuwa "Kanisa la Marafiki" (Quakers) na "Kanisa la sayansi ya Kikristo" (Christian Science)] kwa sababu ya hilo tutaweza kuona kwamba watu wanaliona ni muhimu. Kwa sababu hii na kwa sababu za kimaandiko, tunapaswa kuzingatia kwa umuhimu mada hii. Mwandishi anafanya hivyo. Ni moja ya sababu zangu nyingi kwa nini mimi ni mshirika wa kanisa la Kristo; maana nadai kuwa mshirika wa kanisa la kimaandiko, kanisa ambalo linafundisha Maandiko, mashauri yote ya Mungu, katika kila kipengele cha mafundisho na ibada.

### 2. Tunaweza kuwabatiza akina nani?

Jibu ni watahiniwa (watafutaji) wa kimaandiko, watahiniwa waliozungumzwa katika Maandiko.

Tutaziorodhesha:

A. Watu waliofundishwa: *"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu"* (Mathayo 28:19).

B. Watu wanaoamini: *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa"* (Marko 16:16).

C. Watu wanaotubu: *"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo..."* (Matendo 2:38).

D. Watu ambao wamekiri kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Towashi, kabla ya kubatizwa, alikiri: *"...Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu"* (Matendo 8:37)

(1) Kukiri huku kunapaswa kufanyike mbele za watu (Mathayo 10:32).

(2) Kunatakiwa kufanywe kwa mdomo (Warumi 10:10); hii ni tofauti na kukiri kwa kusaini

kadi, au kwa kuinua mkono wako juu ambapo kila mtu katika umati ameinamisha kichwa isipokuwa mhubiri tu.

Mafungu hayo juu ni mahususi katika kuweka mafundisho, imani, toba na kukiri kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu kabla ya ubatizo. Wale wanaowabatiza watoto wachanga wamekiuka kabisa sheria ya Mungu, na wanasema, "Tuwabatize sasa na kuwafundisha, kuamini, kutubu na kuungama watakapukuwa wakubwa." Hakuna namna katika dunia hii ambapo mtu atawabatiza watoto wachanga bila kukiuka mpangilio wa Mungu na kukiuka neno la Mungu; kwa sababu mafundisho, imani, toba na ungamo ni masharti ya kupata ubatizo wa kimaandiko.

Ninapata amani kusisitiza maandiko haya kwa kuzingatia ukweli kwamba ndugu zangu wameshutumiwa kwa kuamini katika wokovu katika maji. Tunaiamini Biblia na wala haifundishi hivyo. Inafundisha kwamba  mafundisho, imani, toba na ungamo ni lazima vitangulie ili

uweze kuwa wa kimaandiko na fanisi; kama sio wa kimaandiko, basi huo sio ubatizo kabisa machoni pa Mungu. Kushutumiwa kwamba tunaamini katika wokovu kwa njia ya maji kunashangaza sana kwa sababu wengi wanaoshutumu wanafanya kitu hicho hicho. Kwa mfano, ikiwa kumnyunyizia mtoto maji kunambariki, hivyo ni nini kilichombariki mtoto? Wala sio mafundisho, imani, toba au ungamo; kwa hiyo kama alipokea baraka kutoka kwenye maji, ilikuwa ni maji na maji pekee ndiyo yaliyombariki. Sasa hiyo ni "baraka ya maji" au "wokovu wa maji" ambao wengi wanaamini katika huo, hata hivyo sisi hatuamini hivyo. Ni ukweli kwamba ni njia ya kupata washiriki wengi, lakini pia ni ukweli kwamba wanakuja kwa vizazi badala ya kuzaliwa upya (wongofu).

### 3. Je, ubatizo unataka nini?

Kunyunyizia, kumwaga au kuzamisha? Ni dhahiri kwamba sio vyote vitatu. Neno "batiza" ni kitenzi na kitenzi kinaelezea tendo moja mahususi badala ya matendo mengine mengi yasiyofanana. Biblia kamwe haijawahi

kuongea moja kwa moja juu ya mpango wa ubatizo kwa sababu neno lenyewe ubatizo linamaana zamisha. Kitu tunachoweza kusema kuhusu hili ni kwamba neno "batiza" ni kitenzi mahususi na kinaelezea kile haswa kinachotakiwa kufanyika. Kunyunyizia, kumwagia na kuzamisha, kila kimoja ni kitendo mahususi na tofaauti na vingine. Ikiwa neno "batiza" maana yake ni kunyunyizia, basi halimaanishi kumwaga na kuzamisha; ikiwa kinamanisha kumwaga, basi hakimaanishi kunyunyizia na kuzamisha; ikiwa kinamaanisha kuzamisha basi hakimaanishi kunyunyizia na kumwaga. Ikiwa neno "batiza" halimaanishi kitendo kimoja mahususi - bali linamanisha kunyunyizia, kumwaga na kuzamisha, vyote vitatu - basi mtu asingeweza kubatizwa hadi awe amefanya vitendo vyote vitatu. Hakuna mtu anayeamini kwamba maana yake ni hiyo. Kitendo kimoja tu ndicho kinaweza kuwa sahihi. Je, ni kunyunyizia, kumwaga au kuzamisha? Katika kujifunza maandiko kuhusiana na mada hii (pia imeonyeshwa kwenye jedwali) unaweza

# MATAKWA YA KILA KIMOJA

| UBATIZO | KUZAMISHA | KUNYUNYIZIA | KUMWAGIA |
|---|---|---|---|
| Maji (Matendo 8:36) | Ndiyo | Ndiyo | Ndiyo |
| Maji mengi (Yohana 3:23) | Ndiyo | Hapana | Hapana |
| Fika mahali penye maji (Matendo 8:36) | Ndiyo | Hapana | Hapana |
| Telemka kwenda majini (Matendo 8:38) | Ndiyo | Hapana | Hapana |
| Kwamba mbatizaji na mbatizwaji wote wanakwenda ndani ya maji (Matendo 8:38-39) | Ndiyo | Hapana | Hapana |
| Ni maziko (Warumi 6:4) | Ndiyo | Hapana | Hapana |
| Ufufuo (Wakolosai 2:12) | Ndiyo | Hapana | Hapana |
| Kuzaliwa (Yohana 3:5) | Ndiyo | Hapana | Hapana |
| Mwili kuoshwa (Waebrania 10:22) | Ndiyo | Hapana | Hapana |
| Panda kutoka majini (Matendo 8:39; Mathayo 3:16) | Ndiyo | Hapana | Hapana |

ukaamua mwenyewe.

Kila mtu ambaye ananyunyizia au anayemwaga maji kama ubatizo siku ya mwisho atajibu Maandikjo yaliyotolewa katika jedwali hapo juu. Tutahukumiwa na wao na wengine wote (Ufunuo 20:12). Kama unavyolipata neno "nyunyiza" ndani ya Biblia, utaona kwamba kamwe halijawahi kutumika likihusianishwa na tendo la ubatizo (kuzamisha).

(1) *"Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi; nitawatakaseni na uchafu wenu wote, na vinyago vyenu vyote"* (Ezekieli 36:25). Hii ilifanyika chini ya sheria ya Musa, na katika Hesabu 19:1-10 tuna kumbukumbu ya uandaaji wa maji ya kusafisha na kutakasa. Ilijumuisha majivu ya mtamba (ng'ombe) mwekundu, ngozi yake, nyama, damu, kinyesi yake, mti wa mwerezi, na hisopo na sufu nyekundu.

(2) *"ndivyo atakavyowasitusha mataifa mengi..."* (Isaya 52:15). Neno "shitusha" limetumika katika toleo moja la Biblia ya Kiingereza (NRSV) badala ya "nyunyizia," na hii inaendana

na muktadha kabisa.

**4. Ushuhuda wa wengine**

1. Martin Luther: “Ubatizo ni neno la Kiyunani, na linaweza kufasiriwa kama kuzamisha, kama tunavyoweza kuzamisha kitu kwenye maji, ili kiweze kufunikwa chote.”
2. John Calvin: “Neno kubatiza linamaanisha kuzamisha, na ni hakika kwamba kuzamisha ilikuwa ni desturi ya kanisa la awali.”
3. John Wesley: “Tumezikwa pamoja naye-hii inadokeza namna ya zamani ya kubatiza kwa kuzamishwa” (Maoni ya Wesley juu ya Warumi 6:4).
4. Lyman Coleman: “Maana ya msingi ya neno asili ni chovya, tumbukiza, zamisha; na nomino yake ni kuzamisha”
5. Saiklopedia ya Edinburgh: “Katika nyakati za mitume aina ya ubatizo ilikuwa rahisi. Mtu aliyekuwa anabatizwa alikuwa anatumbukizwa mtoni au kwenye chombo”.
6. Liddell na Scott: “Baptizo” (neno la Kiyunani), Ubatizo: “kuzamisha ndani au chini ya maji.”

7. Thayer: "Baptizo" (neno la Kiyunani), Ubatizo: "kutumbukizwa kwa kurudia, kuzamishwa."
8. Kanisa Katoliki la Ugiriki linashuhudia kwamba, kuzamishwa ilikuwa ni tendo la asili na linaendelea kufanya ubatizo wa kuzamisha.
9. Kanisa Katoliki la Rumi linakiri kwamba kuzamishwa ilikuwa ni tendo la asili.
10. Kanisa la Uingereza (Anglikana) linakiri kwamba kuzamishwa ilikuwa ni tendo la asili.
11. Kanisa la Methodisti linakubali kuzamishwa na linawazamisha watu wanaoomba ubatizo wa kuzamishwa.
12. Kamusi ya Webster: "Kudumbukiza au kuzamisha majini, au kumwaga au kunyunyiza maji juu ya." Wala haishangazi kuona hili, kwa sababu ni kazi ya kamusi kutoa matumizi ya maneno yanayotumiwa leo hii. Neno hili linachukua maana zote tatu kwa sababu ya matumizi yake; na ikiwa watu wataanza kuweka miguu yao kwenye maji na kuuita huo ubatizo, kamusi italazimika kuliweka hilo kama mojawapo ya maana yake.

## 5. Mwanzo wa "ubatizo" usio wa kimaandiko

A. Tukio la kwanza la ubatizo wa kunyunyiziwa ni lile la "Novation", 251 B.K., ambaye alipokea ubatizo wa namna hiyo alipokuwa amelala kitandani. Hilo ni jambo la kwanza lisilofuata sheria, lilikuwa linafanyika kwa wagonjwa (wanaoumwa) pekee, lakini hatimaye, lisilofuata sheria likawa desturi inayokubalika.

B. Sikiliza ushuhuda wa Karl Hefele, askofu msomi wa kanisa Katoliki: "Kanisa siku zote limekuwa likiwahurumia wagonjwa; na kwa sababu hiyo akaanzisha ubatizo wa 'kitabibu'." *Historia ya Mabaraza ya Kanisa, ukurasa wa 153*. Uliitwa ubatizo wa "kitabibu" kwa sababu ulikuwa unatolewa kwa wagonjwa. Kanisa Katoliki linadai kuwa hakuna mamlaka ya kimaandiko kwa ubatizo wa kunyunyizia, lakini linakiri kwamba liliuanzisha.

C. Hata hivyo ubatizo wa kunyunyiziwa haukuruhusiwa kisheria na Kanisa Katoliki hadi mwaka 1311 B.K. Tunanukuu: "Baraza la Ravenna, 1311, lilihalalisha ubatizo wa kunyunyizia,

lakini desturi ya ‘kitabibu’ au ‘ubatizo unaofanyika kwenye kitanda cha mgonjwa’ ulikuwa unatumika toka zamani na ukasambaa kutoka katika chumba cha mgonjwa hadi makanisani.” (Johnson’s Universal Cyclopedia, kitabu cha 1, ukurasa wa 488).

Kweli hizi haziwezi kupingwa na mtu yeyote mwenye taarifa za kutosha, Mkatoliki au Mprotestanti. Wale wanaofanya tendo la “ubatizo wa kunyunyizia”, kwa tendo hilo hawana mamlaka nao isipokuwa Kanisa la Katoliki. Wakatoliki wanadai kuwa kanisa lao lina mamlaka ya kubadilisha mapenzi ya Mungu na kuweka kunyunyizia kama ubatizo. Siamini hivyo! Ninapinga kwamba sio Kanisa Katoliki wala kanisa jingine lina mamlaka ya kubadilisha mapenzi ya Mungu katika mada yoyote.

## 6. Kwa nini unapaswa kubatizwa

Swali hili linaulizwa mara kwa mara. Linatakiwa lichunguzwe kwa makini na kwa heshima. Ukweli ni kwamba ubatizo umezungumzwa na

umedokezwa zaidi ya mara mia moja katika Agano Jipya ni ushahidi kwamba ni kitu maarufu katika dini ya Kikristo. Mada ambayo inayojadiliwa mara nyingi sana haipaswi kupuuzwa.

Mtu si mamlaka kamili inayoweza kujibu swali hili. Tunatakiwa tulipeleke swali kwenye Biblia na pale tunaweza kutafuta jibu lake, na wale wote wanaotaka kuongozwa na Bwana wataridhika. Hizi ni baadhi ya sababu zinazopatikana katika neno la Mungu:

1. Kristo hakuwa na dhambi na kubatizwa kwake ilikuwa ni kutimiza haki yote (Mathayo 3:15).
2. Imeamriwa (Matendo 10:48; Mathayo 28:19).
3. Ni jibu la dhamiri njema (1 Petro 3:20-21).
4. Mtu anaweza kufurahia (Matendo 8:39; 16:33-34).
5. Kuingia kwa Kristo (Wagalatia 3:27).
6. Kuingia katika kifo cha Kristo (Warumi 6:3).
7. Kufufuliwa pamoja na Kristo (Wakolosai 2:12).

8. Kuenenda katika upya wa uzima (Warumi 6:4).
9. Kuingia katika ufalme wa Mungu (Yohana 3:5).
10. Kuosha dhambi (Matendo 22:16).
11. Kuokolewa (Marko 16:16; 1 Petro 3:21).
12. Kutoyakataa mafundisho ya Mungu (Luka 7:30).
13. Kwa ajili ya ondoleo la dhambi (Matendo 2:38).

Imekuwa ikipingwa na baadhi ya watu ambao wamekuwa wakijaribu kuepuka umuhimu wa ubatizo kwamba neno la Kiyunani *"eis"* katika fungu hili ambalo limetafsiriwa kama *"mpate ondoleo"* limetafsiriwa vibaya, na kwa hiyo linatakiwa litafsiriwe "kwa sababu ya." Hili lingefanya fungu hili kufundisha kwamba tunatubu na kubatizwa kwa sababu tayari tuna ondoleo la dhambi badala ya kufundisha kwamba toba na ubatizo ni kwa kusudi la au ili kupata ondoleo la dhambi. Tunaweza kukupatia fungu hili kutoka katika tafsiri ishirini na nne tofauti ili uweze kuamua juu ya tafsiri hizo. Ili

kupunguza nafasi tutaondoa maneno yote ambayo sio muhimu ili kuonesha maana ya neno la Kiyunani *"eis."*

i) Tafsiri ya Biblia ya "King James Version" (KJV): *"kwa" - (for)*[1]

ii) Tafsiri ya Biblia ya "American Standard Version" (ASV): *"mpate" - (unto)*[2]

iii) Tafsiri ya Biblia ya "Rotherham's Emphasized" (EBR): *"mpate" (into)*[3]

iv) Tafsiri ya Biblia ya "Modern Speech" (WNT): *"kwa lengo" (with a view to)*[4]

v) Tafsiri ya Biblia ya "Modern English" (Ferrar Fenton): *"kwa" (for)*[5]

vi) Tafsiri ya Biblia ya "Twentieth Century" (TCNT): *"kwa" (for)*[6]

vii) Tafsiri ya Biblia ya "Anderson": *"kupata" (in order to)*[7]

viii) Tafsiri ya Biblia ya "Living Oracles": *"kupata" (in order to)*[8]

---

1 https://www.biblegateway.com/verse/en/Acts%202:38

2 https://www.biblegateway.com/verse/en/Acts%202:38

3 http://www.qbible.com/ebr-rotherhams-emphasized-bible-1902/acts/2.html#38

4 https://www.biblestudytools.com/wnt/acts/2.html

5 https://thetencommandmentsministry.us/ministry/ferrar_fenton/pdf/acts.pdf

6 https://www.bibliatodo.com/en/the-bible/twentieth-century-1904/acts-2

7 https://studybible.info/Anderson/Acts%202:38

8 https://studybible.info/Living_Oracles/Acts%202:38

ix) Tafsiri ya Biblia ya "R. A. Knox's Translation" (Katoliki, hakimiliki, 1944, na Sheed & Ward, Inc.) : *"ili" (to have)*[9]

x) Tafsiri ya Agano Jipya ya "Centenary Translation of the New Testament" na Helen Barrett Montgomery (Imechapishwa na American Baptist Publication Society (MNT): *"kwa" (for)*[10]

xi) Tafsiri ya Biblia ya Agano Jipya ya "Riverside New Testament" na William G. Ballantine: *"mpate" (for)*[11]

xii) Tafsiri ya Biblia ya "William Tyndale's Translation", 1534 (TYN): *"kwa" (for)*[12]

xiii) Tafsiri ya Agano Jipya ya "New Testament Translation", na George Campbell, James Macknight, na Philip Doddridge, 1828 (Kanisa la Scotland) *"kwa" (in order to)*[13]

xiv) Tafsiri ya Biblia ya "English Revised Version", 1881 (ERV): *"ili" (unto)*[14]

9 http://catholicbible.online/side_by_side/NT/Act/ch_2
10 https://studybible.info/MNT/Acts%202:38
11 https://studybible.info/Riverside/Acts%202:38
12 https://www.biblestudytools.com/tyn/acts/2.html
13 https://books.google.com/books/about/The_New_Testament.html?id=RYIfAAAAYAAJ
14 https://www.bibliatodo.com/en/the-bible/revised-version-1881/acts-2;

xv) Tafsiri ya Biblia ya “American Bible Union Translation” (1869) (ABU): *“kwa” (unto)*[15]

xvi) Tafsiri ya Biblia ya “Modern Readers’ Bible” (Moulton): *“ili” (unto)*[16]

xvii) Tafsiri ya Biblia ya “Emphatic Diaglotte”: *“ili” (for)*[17]

xviii) Tafsiri ya Biblia ya “Moffat Translation”: *“kwa” (for)*[18]

xix) Tafsiri ya Biblia ya “Goodspeed’s Translation”: *“ili” (in order to)*[19]

xx) Tafsiri ya Biblia ya Weymouth’s Modern Speech” (Toleo la Robertson): *“kwa” (for)*[20]

xxi) Tafsiri ya Biblia ya “Syriac Version”: *“kwa” (for)*[21]

xxii) Tafsiri ya Agano Jipya ya “Worrell Translation of the New Testament” (kutoka kiwanda cha uchapishaji cha American Baptist Publication Society): *“mpate” (unto)*[22]

---

https://studybible.info/ERV/Acts%202:38
15 https://studybible.info/ABU/Acts%202:38
16 https://archive.org/details/modernreadersbib1920moul/page/n5/mode/2up?ref=ol&view=theater
17 https://www.bibliatodo.com/en/the-bible/diaglott-nt/acts-2
18 https://studybible.info/Moffatt/Acts%202:38
19 https://studybible.info/Goodspeed/Acts%202:38
20 https://theword-modules.com/english/weymouth-new-testament/
21 https://archive.org/details/syriacnewtestam00murdgoog
22 https://studybible.info/Worrell/Acts%202:38

xxiii) Tafsiri ya Biblia ya “Douay Version” (Katoliki) (DRA): *“kwa” (for)*[23]

xxiv) Tafsiri ya Agano Jipya ya “Wycliffe’s Translation of the New Testment” (imetafsiriwa mwaka 1308 na nitafsiri ya Kiingereza ya zamani zaidi) (WYC): *“mpate” (into)*[24]

Kwa hiyo mtu anayesema kwamba Matendo 2:38 inafundisha kwamba ubatizo ni “kwa sababu ya” kuondolewa dhambi, yupo kinyume na wasomi wa dunia.

Watu wanasema kwamba ubatizo ni “matendo” (kazi) ya Mkristo, lakini siyo. Matendo yote (kazi zote) ya Mkristo yanarudiwa zaidi ya mara moja (mara kwa mara). Ni “kazi” ya Mkristo kuimba, lakini hatuwezi kupumzishwa daima kwa kuimba wimbo mmoja. Pia ni “kazi” ya Mkristo kuomba, lakini ombi moja haliwezi likaondoa kazi ya kuomba daima. Majukumu yote ya Mkristo yatakiwa kufanywa kwa kurudiwa mara nyingi. Kwa wahubiri wanaofundisha kwamba ubatizo ni “kazi” tu, ili kuwa na msimamo, watakuwa wanawabatiza washirika wao angalau kila juma au majuma mawili. Ukweli kwamba ubatizo ni amri

23 https://www.biblegateway.com/verse/en/Acts%202:38
24 https://www.biblegateway.com/verse/en/Acts%202:38

inayotakiwa kutiiwa mara moja tu milele yote, ni dhahiri kwamba sio “kazi” ya Mkristo, bali ni ushahidi kwamba ni amri inayotakiwa kufuatwa ili kuwa Mkristo. Inapofuatwa kimaandiko, amri hiyo inakuwa na mtu huyo milele.

“for” (37)
KJ21, AMPC, BRG, CSB, CEB, DARBY, DLNT, EHV, ESV, ESVUK, EXB, GNV, HCSB, ICB, ISV, JUB, AKJV, LEB, TLB, MEV, MOUNCE, NABRE, NASB, NASB1995, NCV, NET, NIV, NIVUK, NKJV, NLT, NMB, OJB, RGT, RSV, RSVCE, TLV, WEB.

“so that” (11)
CEV, GW, GNT, PHILLIPS, NOG, NCB, NRSV, NRSVA, NRSVACE, NRSVCE, NTE

“then” (3)
ERV, NIRV, VOICE;

“into” CJB;

“so” MSG;


“and” NLV;

“to” YLT;

“to have” TPT;

“will be” WE.

https://www.biblegateway.com/verse/en/Acts%202:38







Inatumiwa kwa idhini ya; "World Video Bible School"{WVBS} yaani Shule ya Biblia kwa njia ya filamu ulimwengu. https://video.wvbs.org/

## SABABU YA ISHIRINI



## SABABU YA ISHIRINI

# Kwa sababu linafundisha kwamba mtoto wa Mungu anaweza kufanya dhambi na hivyo akapotea milele

### 1. Utangulizi

Fundisho kwamba mtoto wa Mungu hawezi kutenda katika dhambi na kupotea milele, sio fundisho jipya kwa namna yoyote ile. Hii imezungumziwa pia hata katika Biblia. Lilihubiriwa toka zamani sana na nyoka katika Bustani ya Edeni; yeye ndiye mwanzilishi wake na alihubiri kwa mara ya kwanza kwa Adam na Hawa. Mungu alisema siku ambayo wangekula tunda la mti uliokatazwa wangekufa. Kinyume chake, Shetani akawaambia, *"...Hakika hamtakufa"* (Mwanzo 3:4). Kwa lugha ya sasa, angesema, "Hutahukumiwa kwa sababu haiwezekani wewe uanguke dhambini na kupotea." Lakini tuna neno la Mungu, mateso ya mwanadamu, na minara mingi ya makumbusho ambayo inashuhudia kinyume. Shetani aliwashawishi kuanguka dhambini kwa kuhubiri kwamba

ilikuwa haiwezekani kuondoka katika njia sahihi au kuiacha (kutoweza kukengeuka). Hili ni onyo kubwa! Kwa sababu hii na sababu nyinginezo, siwezi kushiriki katika mifumo ya dini inayofundisha fundisho hili.

**2. Biblia inafundisha kwamba mtoto wa Mungu anaweza kuanguka na kupotea**

A. Kuna mambo ambayo Wakristo wanapaswa kufanya yatakayowazuia kuanguka: *"Kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe"* (2 Petro 1:10) au kuanguka. Mambo gani? Mambo yaliyotajwa katika mafungu matano yaliyotangulia. Kama mtu hafanyi mambo haya ataanguka. Mtoto wa Mungu anaamrishwa kufanya bidii ili kujihakikisha wito wake na uchaguzi wake. Amri hii imetolewa ili kuhakikisha

kuchaguliwa kwa Mkristo.

B. Wakristo wa Korintho walionywa kuwa waangalifu la sivyo wangeanguka: *"Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke"* (1 Wakorintho 10:12). Kama mtu hawezi kuanguka, kwa nini amri hii ilitolewa? Kama ulijua kwamba ni kitu ambacho hakiwezekani kabisa mtu aliyesimama juu ya jengo ataanguka, ungemkimbilia na kumwambia kuwa, "Angalia ndugu, usije ukaanguka!" Wala Roho Mtakatifu asingeweza kutoa onyo hilo kama haiwezekani Mkristo kuanguka.

C. Paulo alijua kwamba inawezekana yeye kukataliwa. Alisema. *"bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa"* (1 Wakorintho 9:27). Paulo alijua kwamba ilikuwa inawezekana kwake kupotea; na kuzuia hali hiyo aliutesa (kuutiisha, kuudhibiti, kuuzoeza) mwili wake.

D. Mtoto wa Mungu anaweza kuacha kuamini, na anapofanya hivyo ataanza anaanguka: *"Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na*

*Mungu aliye hai"* (Waebrania 3:12).

E. Wagalatia walifundishwa kwamba Mkristo anaweza kuanguka kutoka katika hali ya neema: *"Mmetengwa na Kristo, ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria; mmeanguka na kutoka katika hali ya neema"* (Wagalatia 5:4). Katika kujaribu kuhesabiwa haki kwa njia ya sheria ya Musa, walipata hatia ya ukengeufu kamili (kutoka katika ukweli). Sio tu kwamba inawezekana kwa Mkristo kuanguka, lakini katika fungu hili kimsingi lilitokea, ingawa watu wanasema haiwezekani. Zingatia:

(1) Mtu anaokolewa kwa neema (Waefeso 2:8).

(2) Mkristo anaweza kuanguka kutoka katika hali ya Neema (Wagalatia 5:4).

(3) Kwa hiyo Mristo anaweza kupotea.

F. Mkristo anaweza kufanya dhambi na akapotea milele, kwa sababu anaweza kufanya dhambi na kuwa na hali mbaya zaidi kuliko aliyokuwanayo kabla hajawa Mkristo: *"Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi*

*Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua, kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaa-gaa matopeni"* (2 Petro 2:20-22).

(1) Walikuwa wamekimbia machafu ya dunia.

(2) Wakanaswa tena na kushindwa

(3) Hali ya mwisho ni mbaya kuliko ya kwanza. Kama huu sio ushahidi kwamba Mkristo anaweza kutenda dhambi na kwa hiyo akapotea milele, sasa, kwa nini hali ya mwisho inakuwa mbaya kuliko ya kwanza? Je, hatua ya mwisho inaweza kuwa mbaya ikiwa mtu huyu anakwenda mbinguni?

G. Mfano wa mpanzi unaonesha kosa la fundisho kwamba hakuna uwezekano wa kupotea (Mathayo 13:3-8; Mathayo 18-23; Luka 8:4-15): Mbegu katika

mfano ni neno la Mungu (Luka 8:11). Mpanzi ni mhubiri au mwalimu wa Injili (1 Wakorintho 3:6). Udongo ni moyo wa mwanadamu (Luka 8:15). Msikilizaji wa njiani hukubadilika na kuwa Mkristo. Ardhi ya mwamba inawakilisha wale walisikiao na kukubali neno lakini wakanyauka kwa sababu ya shida au mateso na majaribu (Mathayo 13:20-21; Luka 8:13). Walibadilika na kuwa Wakristo lakini hawakuzaa matunda Hatima yao imeandikwa katika Mathayo 7:19: *"Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni."* Ardhi ya miiba inawakilisha wale ambao walikuwa Wakristo lakini wakafungwa na mambo ya dunia, udanganyifu wa utajiri, au anasa za maisha haya na wakashindwa kuzaa matunda (Mathayo 13:22; Luka 8:14). Walikubali neno la Mungu lakini baadaye wakaanguka. Mfano huu ni onyo kwa Wakristo kwamba wanaweza kuanguka na kupotea.

H. Mfano wa mti wa mzabibu na matawi ni ushahidi mwingine kwamba tawi katika mzabibu, Mkristo, linaweza kuchomwa moto: *"Kila tawi ndani*

*yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha, ili lizidi kuzaa ... Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea"* (Yohana 15:2-6). "*Kila tawi ndani yangu"* anasema Yesu. "Ndani yangu!" Sio kitu rahisi kukiondoa; bali ki ndani yangu, Kristo. Hoja kwamba, "ikiwa mtu hataanguka, huyo hakuwa katika Kristo," inaonekana kama mazungumzo yasiyokuwa na maana ikiwa itaangaliwa kwa kurejea fundisho hili. Kwa hiyo, sentensi fupi "ndani yangu" inaharibu moja ya hoja za muhibiri zinazopendwa, na inaondoa utata endapo tawi lililopotea lilikuwa ndani ya Kristo ama la. Nini kinachotokea kwa tawi lisilozaa matunda? "Analitupilia mbali." Halafu nini kinatokea? Baada ya kuwa limenyauka litatupwa motoni. Na 'moto' wenyewe ni *"jehanum ya moto"* (Mathayo 5:22).

I. Tunajifunza kutoka katika mfano wa talanta mtumishi wa Bwana anaweza akapotea (Mathayo 25:14-30):

(1) Watu wanaozungumziwa ni watumishi

wa Bwana mwenyewe.

(2) Wote wawili walikuwa waaminifu na walikuwa wamebarikiwa; mwingine alikuwa hana faida; mwovu na mvivu, na Bwana akaamuru atupwe nje katika giza ambapo kutakuwa na kilio na kusaga meno.

(3) Kwa hiyo mmoja kati ya watumishi wake Mungu mwenyewe anaweza kupotea milele.

J. Yesu alisema angewakusanya watu fulani nje ya ufalme wake na kuwatupa katika tanuru la moto: *"Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno"* (Mathayo 13:41-42). Raia wa ufalme wa Kristo viumbe waliozaliwa upya, watoto wa Mungu, wanaosababisha makwazo na uovu watatupwa katika tanuru la moto mkali.

K. Kristo alisema kwamba angewatapika Walaodikia: *"Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala*

*moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu"* (Ufunuo 3:16). Hivyo kunauwezekano kuwa nje ya Kristo!

L. Paulo alisema kwamba watu wangeasi na kuiacha au kuanguka katika imani (1 Timotheo 4:1-3). Ni hitimisho dhahiri kwamba walikuwa na imani. Utawezaje kiacha imani ambayo hukuwa nayo? Hatma ya wale wanaoiacha imani inaonekana katika 1 Timotheo 5:12: *"nao wana hukumu kwa kuwa wameiacha imani yao ya kwanza."*

M. Mavuno ya Mkristo yanategemea kile alichopanda: *"Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho"* (Wagalatia 6:7-9). Ujumbe huu ulikuwa unatolewa kwa Wakristo; kwa hiyo sheria ya ujumla ya kupanda na kuvuna inafanya kazi kwa Wakristo vile vile kwa wadhambi. Mkristo anaweza kupanda kwa mwili wake na mavuno

yake yatakuwa ni uharibifu; anaweza kupanda kwa Roho na mavuno yake yatakuwa uzima wa milele, kama hatazimia. Sheria hii haibadiliki.

N. Waamini wanaweza kufanya dhambi na wakawa hatarini mwa kifo: *"Ndugu zangu, ikiwa mtu wa kwenu amepotelea mbali na kweli, na mtu mwingine akamrejeza; jueni ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi"* (Yakobo 5:19-20).

(1) Hawa walikuwa ni waamini (Yak. 2:1): hao tu ndio wapo katika hatari ya kifo, kwa sababu wasioamini tayari wamekwishakufa (Waefeso 2:1,5).

(2) Kwa hiyo, waamini wanaweza kupotelea mbali na ukweli na wakawa katika hatari ya kifo.

O. Tunaweza kufanya dhambi dhidi ya ndugu zetu na tukawasababishia kupotea: *"Na yule aliye dhaifu aangamizwa kwa ujuzi wako, naye ni ndugu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake"* (1 Wakorintho 8:11). Kifo hiki ni kifo cha pili (Ufunuo 20:14) sio kifo

cha kwanza au kifo cha mwili ambacho kinawapata wote. Hakuna mwanadamu anayeishi anayeweza kuyaoanisha mafungu haya katika nadharia ya "ukiokolewa mara moja umeokolewa milele."

P. Wanafunzi wengi wa Kristo walijitenga mbali na yeye: *"Kwa ajili ya hayo wengi miongoni mwa wanafunzi wake wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena"* (Yohana 6:66).

(1) Inakubalika kwamba mtu hawezi akaokolewa pasipokupitia kwa Kristo (Yohana 15:5). Mwanadamu hawezi kuokolewa nje ya Kristo.

(2) Wengi wa wanafunzi wa Yesu walijitenga naye (Yohana 6:66)

(3) Kwa hiyo, hawa wanafunzi wa Kristo walipotea milele.

Q. Mtoto wa Mungu anaweza akapotea kwa sababu anaweza kudanganya, na akafa katika hali hiyo. Je, anaweza kufa katika hali hiyo? Anania na Safira walikufa (Matendo 5). Hatma ya wale wanaokufa katika hali hiyo inaonekana katika Ufunuo 21:8: *"...na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa*

*liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili."* (Ufunuo 21:8). Kwa hiyo, inawezekana mtoto wa Mungu kufanya dhambi na kupotea milele.

R. Ama inawezekana kwa mtoto wa Mungu kupotea au haiwezekani kwa mtoto wa Mungu kuonja mauti kabisa, chini ya masharti fulani. Hakuna mlevi *"hawataurithi ufalme wa Mungu"* (1 Wakorintho 6:9-10). Je, mtoto wa Mungu anaweza kuwa mlevi? Wewe unasema, "Ndiyo." Lakini watu wanasema kwamba Mungu hatamwacha afe katika hali hiyo. Kama ingekuwa kweli kwamba Mungu asingemwacha mtu afe namna hiyo, basi Mkristo angeweza kuwa mlevi na akabakia kuwa mlevi na asingekufa kamwe bali angeishi milele hapa hapa duniani. Ni upuuzi kiasi gani!

S. Kama mtoto wa Mungu hawezi kupotea, basi Shetani ni mjinga. Amekuwa akifanya kazi kwa takribani miaka elfu sita akizidanganya roho za watoto wa Mungu; na kama hakuweza kufanikiwa kudanganya roho hata moja ya mtoto wa Mungu, basi ni mjinga, hapaswi kuendelea.

### 3. Uchunguzi wa baadhi ya matini za ushahidi

A. *"Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani"* (Yohana 5:24). Nukuu hii inatumika kuthibitisha kwamba muumini ana maisha ya milele sasa, na kwa hiyo haiwezekani yeye kupotea. Tunajua kwamba andiko moja halipingani na jingine, hivyo maelezo yake ni nini?

Kauli ya Yesu kuhusiana na kumwaga kwake damu itasaidia: *"kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi"* (Mathayo 26:28). Kristo alizungumza kana kwamba damu yake ilikuwa imekwisha mwagika, wakati bado ilikuwa inazunguka katika mishipa yake; ilipaswa kumwagwa hapo baadaye. Kimsingi, katika Yohana 5:24, Yesu aliitazama siku ya hukumu ijayo na kuizungumzia kana kwamba ni sasa. Akiizungumzia hukumu ya wakati ujao kana kwamba yupo Yesu alisema kwamba mshirika amekwisha kuwa na

uzima wa milele.

Waamini wana maisha ya milele katika maana mbili:

(1) Katika ahadi (1 Yohana 2:25).

(2) Na ana Yesu ambaye ni "(... uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu)" (1 Yohana 1:2).

Hata hivyo, Biblia inafundisha katika maeneo mengi kwamba mwamini katika dunia hii hana uzima wa milele kwa sasa katika uhalisia wake, kwa mfano:

(1) Vyote maisha na hukumu ya milele vipo katika upande mwingine wa bonde la mauti (Danieli 12:2).

(2) Sasa tupo katika tumaini la uzima wa milele (Tito 1:1–2), na hatutumainii kile tulicho nacho (Warumi 8:25).

(3) Bwana atatoa maisha ya milele (Warumi 2:6–7).

(4) Maisha ya milele yatakuja mwishoni (Warumi 6:22).

(5) Wenye haki watapokea maisha ya milele hatimaye waovu watapokea hukumu ya milele (Mathayo 25:46).

(6) Maisha ya milele yatapokelewa katika

ulimwengu unaokuja (Marko 10:30).

B. *"Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? Kama ilivyoandikwa, ya kwamba, Kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa, Tumehesabiwa kuwa kama kondoo wa kuchinjwa. Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu"* (Warumi 8:35-39). Ikiwa mafungu haya yanarejea upendo wetu kwa Mungu badala ya Upendo wa Mungu kwetu, bado hayafundishi kutowezekana kupotea, badala yake vitu hivyo vya nje haviwezi kututenganisha na upendo wa Mungu, lakini hii haitufundishi kwamba hatuwezi kujitenga na upendo wa Mungu. Iko wazi kwamba tunaweza

kujitenga na upendo wa Mungu:

(1) *"...kaeni katika pendo langu"* (Yohana 15:9).

(2) *"Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu..."* (Yohana 15:10).

(3) *"jilindeni katika upendo wa Mungu..."* (Yuda 21). Kama utapenda kusema mafungu haya yanamaanisha upendo wa Mungu kwa mwanadamu, bado haithibitishi kutowezekana kwa kupotea; kwa sababu ukweli kwamba Mungu anampenda mwanadamu, sio hakikisho la wokovu wa mwanadamu, maana Mungu aliupenda ulimwengu wote (Yohana 3:16) na alitupenda tungali bado tu wenye dhambi (Warumi 5:8).

C. *"Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu"* (1 Yohana 3:9). Yohana anasema kwamba mtu hawezi kutenda dhambi kwa sababu uzao wakaa ndani yake. Mbegu ni neno la Mungu (Luka 8:11), na Shetani anaweza akainyakua

mbegu kutoka katika moyo wa mtu (Luka 8:12).Yohana katika fungu hili hafundishi kwamba haiwezekani kwa Mkristo kutenda dhambi, kwa sababu anafundisha katika mafungu mengine ya wazi kwamba anaweza:

(1) *"Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu"* (1 Yohana 1:8).

(2) *"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote"* (1 Yohana 1:9).

(3) *"Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi..."* (1 Yohana 2:1)

(4) *"...Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki"* (1 Yohana 2:1). Mtu ambaye anafasiri fungu moja na kusema kwamba linapingana na fungu jingine, hakika amelifasiri vibaya. Kwa hiyo maelekezo mengine yaliyotumika, kuhakikisha ili fundisho potovu yanashindwa!

D. Warumi 7:15-25 linatumika katika jitihada za kuthibitisha kwamba ni

mwili wa binadamu ndio unaotenda dhambi wala sio roho yake. Kama ndivyo hivyo, vipi kuhusu mtu atavuna alichopanda (Wagalatia 6:6-7) - halafu mwili wake utatupwa motoni na roho yake itapaa mbinguni. Hiki ni kitu kipya chini ya jua: roho ya mwanadamu mbinguni na mwili wake motoni! Ukweli wa swala hili ni kama ifuatavyo:

(1) Roho ya mwanadamu inafanya dhambi itawale mwilini (Warumi 6:12).

(2) Ni roho ndiyo inayojua badala ya mwili (1 Wakorintho 2:11).

(3) Dhambi nyingine zinafanywa kuufurahisha mwili, lakini zinafanywa kwanza moyoni na zinakua kutoka moyoni (Marko 7:21-23).

E. *"Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila yeye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto"* (1 Wakorintho 3:15). Kazi ya mwalimu inayoweza kuchomwa ni watu walioongolewa kwa Kristo. Hii itakuwa ni hasara, lakini yeye mwenyewe anaweza kuokolewa. Wakorintho walikuwa ni kazi ya Paulo na aliogopa

kwamba baadhi wangeweza kupotea. Fungu hili linapinga badala ya kuafiki kutowezekana kwa kupotea (wangeasi au kuanguka katika imani).

F. *"Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho"* (1 Petro 1:5). Tunalindwa na nguvu ya Mungu hata tupate wokovu, na ni "kwa njia ya imani." Chanzo cha nguvu ni Mungu; sehemu yetu ni kuamini, na tutafanya vizuri kukumbuka kwamba mtu anaweza kuacha kuamini (Waebrania 3:12) na kwa hiyo akashindwa kulindwa na nguvu za Mungu.

G. Mathayo 7:21-23 inatumika kuthibitisha kwamba Kristo hawajui na hajawahi kuwajua wale wanaoanguka. Lakini fungu hili halithibitishi hivyo. Linathibitisha tu kwamba Kristo hakuwahi kuwajua manabii hawa wa uongo, kwa sababu tunajifunza katika fungu la kwanza kuwa hawa ndio wanaozungumziwa.

H. *"Walitoka kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu. Maana kama wangalikuwa wa kwetu, wangalikaa pamoja nasi.*

*Lakini walitoka ili wafunuliwe kwamba si wote walio wa kwetu"* (1 Yohana 2:19). Katika fungu la kumi na nane tunajifunza kwamba Yohana anazungumzia wapinga Kristo. Hawa wapinga Kristo waliacha mafundisho ya Mitume wakaanza kuhubiri mafundisho mengine. Huu ulikuwa ni ushahidi kwamba hawakuwa wamoja na mitume; kama isingekuwa hivyo, wangeweza kuendelea pamoja nao, wakihubiri mafundisho waliyokuwa wanayahubiri; maana Roho Mtakatifu ambaye alikuwa kwa mitume asingewaacha mitume wahubiri fundisho jingine, na watu hawa wahubiri fundisho jingine tofauti. Yohana anasema kwamba si *"wote"* walikuwa wa kwetu. Hawa ndio ambao wamevutwa na waalimu wa uongo kwao.

I. *"Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili"* (1 Wakorintho 10:13). Mungu ni mwaminifu kuweka fursa ya

mlango wa kutokea kwa Mkristo, na Mkristo anapaswa kuinyakua fursa hii la sivyo ataanguka; maana fungu lililotangulia linasema: *"Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke"* (1 Wakorintho 10:12).

J. *"Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu"* (Yohana 10:27-28). Ahadi nzuri hizi ni za masharti na zinategemea mtu kumfuata Kristo: "wananifuata." Yesu anafundisha katika fungu la kumi na mbili kwamba kondoo wanaweza wakapokonywa na kutawanyika. "Na mbwa mwitu akawanyakua na akawatawanya."

Mafungu kumi yaliyojadiliwa hapo juu si mafungu yote yaliyotumika kuthibitisha fundisho la uongo lisemalo, "Ukiokolewa mara moja umeokolewa milele." Hata hivyo, haya ni baadhi tu kati ya yale makuu.

KWA NINI MIMI NI MSHIRIKA WA KANISA LA KRISTO

# 21

## SABABU YA ISHIRINI NA MOJA



## SABABU YA ISHIRINI NA MOJA

# Kwa sababu linafundisha kwamba watoto wachanga wanazaliwa wakiwa safi na bila hatia badala ya kupotea kabisa.

### 1. Utangulizi

WATU wengi kwa kujua na kwa kutokujua— "wengi ni bila kujua— wamejiunga na kanuni za kidini za kanisa zinazofundisha urithishwaji wa kupotea kabisa.

**Mwanadamu alipotea kabisa katika dhambi (Total Hereditary Depravity):** "Urithi kamili wa ukengeufu" kurithi kuanguka kikamilifu, ovu, kujaa dhambi kabisa au kuwa na dhambi ya asili. Inaelezwa kutokuwa mwema kabisa ambapo ingekuwa kujaa uovu kabisa.

Kwa makusudi ya kitabu hiki, kwa ujumla tutatumia kirai "*kupotea kabisa*" kuwakilisha fundisho hili.

Kwa mujibu wa "Kamusi ya Webster," "*urithishaji*" maana yake ni "kilichoambukizwa au kusafirishwa, kama sifa ya umbile au hali kutoka kwa mzazi kwenda kwa mtoto;" na "*kupotea kabisa*" maana yake ni "hali ya kuwa mwovu, kupotoka, kuharibika." Ni nadharia inayosema kwamba uharibifu wa dhambi umeambukizwa kwa mtoto kutoka kwa mzazi, kwa hiyo mtoto anarithishwa uovu; kwamba kwa kurithi sio msafi; kwamba ni mtoto wa Shetani.

A. Kosa moja linapelekea kosa jingine. Fundisho la "kupotea kabisa" linapelekea kosa jingine la ubatizo wa watoto wachanga. Hapa kuna nukuu ya John Wesley, mwanzilishi wa Kanisa la Methodisti: "Lakini swali kubwa ni, Watahiniwa halisi wa ubatizo ni akina nani? - watu wazima pekee au na watoto wachanga pia? Ili kujibu hili kikamilifu, kwanza natakiwa nielezee ubatizo wa watoto wachanga,

kutoka katika maandiko, sababu, desturi za kiulimwengu za msingi; na pili kujibu madai dhidi yake.

John Wesley alisema, “Kutoka na msingi wake: Kama watoto wachanga wana hatia ya dhambi ya asili, kwa hiyo ni wahusika sahihi wa ubatizo; kwa kuangalia katika njia ya kawaida, hawawezi kuokolewa, isipokuwa wamesafishwa kwa ubatizo. Imethibitishwa kuwa hii dhambi ya asili ipo kwa kila mtoto wa mwanadamu; kwa hiyo ni watoto wa ghadhabu, na kwa hiyo wanawajibika katika hukumu ya milele. Watoto wachanga wanahitaji kusafishwa dhambi ya asili; kwa hiyo ni wahusika sahihi wa ubatizo”.—Wesley’s Works, Miscellaneous, kitabu cha 2, uk. 16. Neander pia anasema kuwa ubatizo wa watoto wachanga umetokana na mafundisho ya dhambi ya asili.—*Church History,* kitabu cha *1, kurasa za 426, 427.*

B. Ingekuwa sio haki kuonekana kwamba wanaohubiri juu ya ubatizo wa watoto wachanga ni wao pekee ndio wamefundishwa “kupotea kabisa”. Hii isingekuwa haki kwa Wabaptisti.

Kwa hiyo tunaingiza nukuu kutoka katika kanuni za imani za kanisa lao: "Tunaamini kwamba mwanadamu aliumbwa katika utakatifu, chini ya sheria ya Muumbaji wake, lakini kwa kuanguka dhambini kwa hiari alitoka katika hali hiyo ya utakatifu na ya furaha; kitu kilichopelekea binadamu wote sasa kuwa wenye dhambi, sio kwa kikwazo bali kwa kuchagua; kwa asili bila huo utakatifu unaotakiwa na sheria ya Mungu, ananaswa dhambini; na kwa hiyo kuwa chini ya hukumu ya haki ya uangamivu wa milele, bila utetezi au udhuru."—*Church Manual Designed For The Use of Baptist Churches, na J.M. Pendleton, ukurasa wa 46* "Wanadamu wote" haiachi mtu yeyote. Inajumuisha watoto wachanga na watu wazima pia.

C. Hakuna taswira nyeusi iwezayo kupakwa rangi iliyotolewa na wahubiri wa fundisho la kupotea kabisa. Mwandishi hawezi akahusishwa na kundi linalofundisha fundisho hili la kuchukiza na lisilokuwa la kimaandiko.

## 2. Uchunguzi wa baadhi ya matini wanazozitumia kama ushahidi

A. Wahubiri wa nadharia hii mara nyingi wanatumia Zaburi 14:2-3 kama fungu la ushahidi, lakini linapingana na nadharia hii: *"Toka mbinguni BWANA aliwachungulia wanadamu, Aone kama yuko mtu mwenye akili, Amtafutaye Mungu. Wote wamepotoka, wameoza wote pamoja, Hakuna atendaye mema, La! hata mmoja."* Hii inathibitisha kwamba watu walikuwa waovu, lakini haithibitishi kwamba walizaliwa wakiwa katika hali hii. Fungu hili linasema, *"Wote wamepotoka, wameoza wote pamoja..."* (14:3). Isingewezekana kwao kupotoka na kuoza wote kwa pamoja kama wangekuwa wamezaliwa katika hali hiyo. Ukweli kwamba walipotoka na kuoza ni uthibitisho kwamba hawakuzaliwa katika hali hiyo.

B. Zaburi 51:5, fungu lao jingine la uthibitisho, halifundishi hivyo: *"Tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu; Mama yangu alinichukua mimba hatiani."* Wanaohubiri wanaofundisha "kupotea kabisa" wanasema kwamba Daudi alizaliwa

akiwa mwenye dhambi, lakini fungu hili wala halina maana hiyo. Dhambi imetajwa katika fungu, lakini ilifanywa kabla Daudi hajazaliwa. Daudi hakuwepo mama yake alipomchukua mimba. Kwa hiyo, hatia na dhambi inayozungumzwa ilikuwepo kabla ya Daudi hajakuwapo.

C. Kauli ya Paulo katika Waefeso 2:3 pia linatumika kuthibithisha fundisho hili: *"...tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine"* (Waefeso 2:3). "*Kwa tabia*" hata hivyo, sio mara zote inamaanisha "kwa urithi." Adam Clarke, muumini wa fundisho la "kupotea kabisa," asingeweza kutumia fungu hili kama fungu la uthibitisho. Badala yake angesema, "Mtume inaelekea anazungumzia juu ya matendo ya dhambi."

D. Tuchunguze tena Zaburi 58:3: *"Wasio haki wamejitenga tangu kuzaliwa kwao; Tangu tumboni wamepotea, wakisema uongo."* Hii inasema kwamba walipotea baada ya kuwa wamezaliwa. Hawakuzaliwa wakiwa wamepotea. Dhambi zao zilijumuisha kusema uongo. Watoto wachanga hawawezi

kusema uongo; kwa hiyo dhambi hii haikufanyika katika hali ya uchanga.

**3. Mafungu yanayokanusha fundisho hili la uongo.**

A. Mtu akawa mwenye dhambi katika ujana wala sio utotoni: *"... BWANA akasema moyoni, Sitailaani nchi tena baada ya hayo kwa sababu ya wanadamu, maana mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake..."* (Mwanzo 8:21). Kama moyo wa mwanadamu ulikuwa mbaya kuanzia ujana, basi ni lazima unakuwa mwema kabla ya ujana.

B. Roho ya mwanadamu amepewa na Muumbaji wake: *"Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, Nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa"* (Mhubiri 12:7). Kama Mungu amempa mwanadamu roho iliyoharibika, huoni kwamba sio haki Mungu kumwajibisha mwanadamu kwa ukengeufu wake? Si sawa na si haki.

C. Mtoto mchanga si mwovu (hajapotea) kwa sababu Mungu si mwovu. Paulo alisema katika hotuba yake mashuhuri huko Athene aliyoitoa

katikati ya Areopago, *"...Maana sisi sote tu wazao wake"* (Matendo 17:28). Kuwa mzao wa Mungu, mtoto sio mwovu, kama Mungu asivyo mwovu. Hakuna mtu anayeweza kusema kwamba Mungu ni mwovu. Sasa kwa nini usema wazao wake ni waovu?

D. Roho mtakatifu anasema kwamba mwana hatauchukua uovu wa mzazi wake: *"Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake"* (Ezekieli 18:20). Angalia kile tunachokipata katika fungu hili:

Kwanza, haki na uovu vyote vipo juu ya mtendaji wake na wala si juu ya mtu mwingine. Haki inataka hivi.

Pili, "*mwana hatauchukua uovu wa baba yake*" Wale wanaothibitisha kwamba mtoto lazima achukue uovu wa baba (Adam) wanapingana na kauli hii.

E. Mtoto mchanga sio mwovu (hajapotea), kwa sababu mtu ni lazima awe kama

mtoto mchanga ili aweze kuingia ufalme wa mbinguni: Yesu akasema, *"...Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni"* (Mathayo 18:3). Halafu bado wanadini wengi wanafundisha kwamba mtoto ni mwovu (amepotea) kamili kwa urithi. Je, Yesu alifundisha kwamba mtu lazima awe mwovu na mkengeufu ili aweze kuingia katika ufalme wa mbinguni? Hapana, hakufundisha hivyo!

F. Daudi hakuamini kwamba mtoto wake alikufa akiwa na ukengeufu wa asili na hatia ya dhambi. Kinyume chake alisema, *"...nitakwenda kwake lakini yeye hatanirudia mimi"* (2 Samweli 12:23).

G. Haiwezekani dhambi kurithishwa: Dhambi ni uasi wa sheria ya Mungu ama kwa kutenda au kutotenda. Kuhusiana na kutenda: *"Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi"* (1 Yohana 3:4). Kuhusiana na kutotenda: *"Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi"* (Yakobo 4:17). Dhambi ni ama kufanya kilichokatazwa na Mungu au

kutofanya alichotuamuru tufanye. Kwa sababu usemi wa kwanza ni kweli, basi haiwezekani kabisa kwa mtu kurithi hii “hali ya asili ya kupotea,” “asili ya dhambi,” au “dhambi,” kwa sababu sio sifa inayorithiwa.

H. Ukweli kwamba Mungu hajatoa mpango kwa ajili ya kuwaokoa watoto wachanga ni uthibitisho wa uhakika kwamba hawajapotea, kwamba sio wadhambi.

# UCHUNGUZI NA HITIMISHO

# 22

## SABABU YA ISHIRINI NA MBILI



## SABABU YA ISHIRINI NA MBILI

# Kwa sababu linafundisha kwamba udhihirishaji wa kimiujiza wa Roho Mtakatifu umesitishwa

### 1. Utangulizi

Makundi mengi ya kidini leo yanajishuhudia kwamba yanazungumza kwa uvuvio na kufanya miujiza. Mahubiri ya aina hiyo yamesababisha mkanganyiko katika akili za watu wengi. Basi tujifunze somo hili pamoja. Ikiwa Biblia inafundisha kwamba karama za miujiza zilikuwa zinaendelea karne hadi karne, basi nitakuwa katika kundi lisilo sahihi; lakini ikiwa linafundisha karama hizo zilitolewa kwa ajili ya kukamilisha kazi fulani na baadaye kukoma, basi wote wanaodai nguvu hii wamekosea. Lazima iwe njia moja ama nyingine; na kwa hiyo, lazima twende kwenye Maandiko.

### 2. Kristo alifanya miujiza mingi

A. Yesu alilazimika kufanya miujiza ili

kuthibitisha kwamba alikuwa Mwana wa Mungu. Kama kusingekuwa na ishara za miujiza ya kuambatana na kazi Yake, wanadamu wasingekuwa wameshawishika kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.Nguvu ya kufanya miujiza ilitia muhuri kazi ya Kristo kwa muhuri mtakatifu. Nikodemu, mtawala wa Wayahudi, alikiri kwa kusema, *"Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye"* (Yohana 3:2). Kwa kuwa na sifa hizo za kiungu, alitambulika kama *"...mwalimu, umetoka kwa Mungu."*



B. Dai la Yesu lilihitaji miujiza na alilithibitisha dai hili kwa kwa kufanya *"...ishara nyingine nyingi ... zisizoandikwa katika kitabu hiki"* (Yohana 20:30).

Hata hivyo, ishara nyingi zimaendikwa na baadhi yake ni:

(1) vipofu walipata kuona (Yohana 9:1-12) ;

(2) viwete walitembea (Mathayo 21:14);

(3) wakoma walipata kusafishwa (Luka 17:11-19);

(4) viziwi walisikia (Marko 7:31-37);

(5) wagonjwa waliponywa (Mathayo 8:14-17);

(6) mapepo yalitolewa (Mathayo 8:28-34);

(7) Alitembea juu ya maji (Mathayo 14:22-33);

(8) upepo na bahari vilimtii (Mathayo 8:27);

(9) maelfu walilishwa kwa vipande vichache vya mkate na samaki wakala na kusaza. (Mathayo 14:13-21);

(10) Alifufua wafu (Yohana 11:32-45); na

(11) Alikwenda mbali zaidi na Akafanya ushahidi usioweza kupingika milele kwamba Alikufa na Akafufuka kutoka katika wafu (Yohana 20:19-31), Akajionyesha kwamba yu hai kwa

vithibitisho vingi (Matendo 1:3).

C. Ishara za uhakika za Kristo zilirekodiwa kwa makusudi ya kuzalisha kuamini: *"Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake"* (Yohana 20:30-31). Tunaona kusudi la kurekodi baadhi ya ishara hizi: kuzalisha kuamini katika Kristo. Aidha, tunaona kwa nini ishara nyingine nyingi hazikuandikwa: haizikuhitajika kwa ajili ya kusudi hili. Kwa kuwa hii yote ni kweli, basi hakuna haja hivi leo kuonesha nguvu zisizo za kawaida ili kumshawishi mtu juu ya nguvu za uungu za Kristo. Kwa hiyo, kudai miujiza leo ili kwamba uamini katika Kristo ni tusi kwake Yeye ambaye tayari ametoa njia ya kuzalisha imani na kutuwezesha kuamini.

### 3. Uvuvio na uthibitisho wa ujumbe

A. Ilikuwa ni muhimu kwamba wahubiri wa kwanza wa injili walivuviwa ili

kujua nini cha kusema, na halafu kufanya miujiza ili kuthibitisha kile walichosema. Kulikuwa hakuna njia nyingine, kwa sababu kulikuwa hakuna Agano Jipya ambalo lilikuwa limeandikwa na kuthibitishwa na miujiza kwa wakati huo. Kwa namna gani nyingine ambayo watu wangejuaje kwamba wanapokea injili ya kweli?

B. Mwonekano wa kuanza kwa Injili, mitume waliahidiwa ubatizo katika Roho Mtakatifu ili kwamba waweze kuifanya kazi kwa uhakika bila kukosea iliyoanzishwa na Yesu Kristo (Matendo 1:4–5). Zifuatazo ni hoja zinazohusiana na ahadi hii:

(1) Roho Mtakatifu angezungumza kupitia mitume: Mtapewa nini cha kusema; *"... kwa maana si ninyi msemao, bali ni Roho Mtakatifu"* (Marko 13:11).

(2) Roho Mtakatifu angewafundisha na kuwapatia kumbukumbu ya kile Yesu alichokuwa amefundisha: *"Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia"* (Yohana 14:26).

(3) Roho Mtakatifu alikuwa akimshuhudia Kristo: *"...yeye atanishuhudia"* (Yohana 15:26).

(4) Roho Mtakatifu kazi yake ilikuwa ni kuwaongoza katika kweli yote. *"Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote..."* (Yohana 16:13).

(5) Roho Mtakatifu angewapatia nguvu: *"Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya. Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu"* (Luka 24:48-49). Nguvu hii ambayo kwayo wangefunikwa ingeshughulikia utangazaji wa ujumbe wa kweli, kama ilivyoonyeshwa katika mafungu ya juu; nguvu hii pia ingewawezesha kufanya miujiza ili kuthibitisha ukweli wa ujumbe waliouhubiri. Ishara ambazo zingekuwa zinaambatana na ujumbe wanaohubiri ziliahidiwa wakati thenashara walipoamriwa kwenda ulimwenguni na kuhubiri Injili: *"Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa*

*kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya"* (Marko 16:17-18). Ilikuwa ni kwa makusudi gani ishara kuambatana na neno? Jibu hili hapa: *"Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo.]"* (Marko 16:20). Sikiliza Paulo akisema tena kusudi hilo: *"...Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia; Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda mwenyewe"* (Waebrania 2:3-4).

Kutoka katika nukuu hapo juu nimethibitisha vitu viwili:

Kwanza, ilikuwa ni lazima kwamba Roho Mtakatifu aje kwa mitume ili kwamba injili itangazwe kwa uhakika bila makosa; Kumbukumbu ya mwanadamu isingeweza kuaminiwa pamoja na ujumbe wa ufunuo kwa sababu kumbukumbu yake ni dhaifu.

Pili, ilikuwa ni lazima kwamba ishara

ziambatane nao hadi mwisho ili ujumbe uweze kuthibitika.

C. Katika Matendo 2:1-4 tunasoma kuja kwa Roho Mtakatifu kwa mitume, utimizwaji wa ahadi.

(1) Waliahidiwa kwamba Roho Mtakatifu angewaongoza katika kuhubiri. Katika Matendo 2:4 tunasoma kuwa Roho Mtakatifu aliwapatia ya kusema.

(2) Bwana pia aliahidi kwamba ishara zingeambatana nao.

Katika Matendo 2:43 tunasoma: *"... ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume"* Moja ya ishara ilikuwa ni kuzungumza kwa *"lugha mpya"* (Marko 16:17). Katika siku hii, siku ya Pentekoste, mitume walizungumza kwa *"lugha nyingine"* (Matendo 2:4). Kulikuwa na Wayahudi kule kutoka katika kila taifa chini ya mbingu (Matendo 2:5), *"...kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe"* (Matendo 2:6).Wakashangaa na kusema, *"Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?"* (Matendo 2:8). Wakasema pia,, *"...tunawasikia hawa wakisema*

*kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu"* (Matendo 2:11). Tunaona kwamba kuzungumza huku kwa lugha hazikuwa sauti nyingi zisizoeleweka, bali kulikuwa ni kuzungumza katika lugha ambayo ingeweza kuelewaka kwa watu ambao waliishi nchi mbalimbali ambapo walizungumza lugha hizo. Wale wanaodai kuzungumza katika "lugha zisizoeleweka" leo wangeweza kuzungumza lugha ambazo hawajawahi kufundishwa badala ya kutamka maneno yasiyokuwa na maana. Hebu ambaye hajawahi kujifunza Kihispania, Kifaransa au Kilatini azungumze katika lugha hizi. Ndio, na azizungumze na kumwacha msemaji mwejeji asikilize na kuthibitisha uwezo wao wa kuelewa kinachozungumzwa.

Miaka michache iliyopita, nilipokuwa nazungumza na mwanamke mmoja juu ya mada hii, nilivuta barua kutoka mfukoni mwangu na nikampatia, nikasema, "Barua hii inaweza ikakusaidia" Alisoma sehemu ya kwanza ambayo ilikuwa kwa Kiingereza, halafu akauliza, "Sehemu ya pili ya barua hii ni nini?" Nikamjibu,

"Ni lugha isiyofahamika." Akashangaa na kusema, "Unaweza ukasoma hii? Unaweza ukatafsiri?" Nikamtafsiria. Akaendelea, "tunaweza kunena kwa lugha, lakini hakuna anayeweza kusoma, kuandika, au kuelewa katika lugha." Halafu nikafafanua: "Hii ni lugha ya Kihispania cha zamani, lakini kwako ni kama lugha isiyofahamika, lugha ambayo hujawahi kujifunza. Watu katika siku ya Pentekoste walisikia katika lugha yao wenyewe kutoka sehemu waliyozaliwa. Hawakusikia lugha ambayo haifahamiki kabisa na mtu yeyote katika muda wowote au mahali popote. Walisikiliza katika lugha ambayo iliweza kuandikwa vile vile ilivyoweza kuzungumzwa." Kunena kwa lugha ilikuwa ni mojawapo ya ishara zilizowafuata. Waliponya wagonjwa, wakatoa mapepo, na wakafanya maajabu mengi.

D. Kuja kwa Roho Mtakatifu juu ya Mataifa (Matendo 10:44-48) (Kornelio na rafiki zake) kulikuwa kwa kusudi tofauti. Ulikuwa ni ubatizo katika Roho Mtakatifu, maana Petro alitambua hivyo (Matendo 11:15-16).

(1) Lengo la ubatizo huu linaonekana wazi katika matumizi yake yaliyoonekana baadaye. Akiwa Yerusalemu, Petro alihusisha tukio hili na kuondoa mashaka ambayo Wayahudi walikuwa nayo juu ya kuwabatiza Mataifa (Matendo 11:1-18); kwa hiyo hili ndilo lililokuwa lengo lake: mpango wa nje kwao. Kwa kuwa hili ndilo lilikuwa lengo, lilipooneshwa mara moja, kulikuwa hakuna haja ya kurudiwa; hii ni sababu kwa nini halikurudia tena.

(2) Ubatizo huu katika Roho haukumwokoa Kornelio na rafiki zake. Wao pia kama Wayahudi siku ya Pentekoste, walipaswa kusikia Injili na kuokolewa kwayo. Malaika alikuwa amekwisha mwambia Kornelio kwamba Petro *"... atakayekuambia maneno ambayo yatakuokoa, wewe na nyumba yako yote"* (Matendo 11:13-14). Kwa hiyo waliokolewa kwa maneno badala ya ubatizo wa Roho Mtakatifu.

**4. Mitume pekee ndio waliokuwa na uwezo wa kuwapa au kutoa kwa wengine karama ya miujiza ya Roho Mtakatifu**

Uwezo wa kugawa karama za miujiza

ya Roho Mtakatifu kwa Wakristo ulikuwa ni mahususi (maalum) kwa mitume tu. Hakuna mtu mwingine aliyepata heshima hii, na wale waliopokea karama hizi kutoka kwa mitume hawakuweza kugawa watu wengine. Ushahidi ufuataao:

A. Msamaria alipokea karama ya miujiza ya Roho kupitia mitume wawili: *"Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana; ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu; kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu"* (Matendo 8:14-17). Wasamaria hawa walikuwa wamebatizwa, kwa hiyo, walikuwa wamepokea kipawa cha Roho Mtakatifu kama ilivyoahidiwa katika Matendo 2:38, lakini hawakuwa wamepokea karama za kimiujiza. Mitume walimtuma Petro na Yohana ili kuweka mikono juu yao ili kwamba waweze

kupata nguvu.  Kwa nini Filipo - mtu ambaye alikuwa amefanya ishara nyingi miongoni mwao (Matendo 8:5-8) asiwapatie hizi nguvu?  Jibu ni dhahiri: Kwa kuwa hakuwa mtume, asingeweza kufanya hivyo.  Kama ndio, hivyo kwa nini mitume wawili walitumwa kwenda kuwapa?

B. Filipo alipokea uwezo huu wa kimiujiza kwa kuwekewa mikono na mitume. Imetajwa kwamba ishara nyingi ziliambatana na mahubiri ya Filipo huko Samaria (Matendo 8:5-8). Alipata wapi nguvu ya kufanya miujiza? Jibu:  Alikuwa miongoni mwa watu saba waliochaguliwa kufanya kazi katika kanisa la Yerusalemu; *"ambao wakawaweka mbele ya mitume, na walipokwisha kuomba wakaweka mikono yao juu yao"* (6) (Matendo 6:1-6). Ni wazi kwamba nguvu hii ilikuja kwa Filipo kwa kuwekewa mikono ya mitume.

C. Paulo alitoa nguvu hizi kwa watu kumi na wawili aliowabatiza.  Katika Matendo 19:1-7 tunasoma juu ya watu kumi na wawili waliobatizwa na Paulo. Kwa hiyo, walipokea karama

ya Roho Mtakatifu (Matendo 2:38), lakini hawakupokea karama ya miujiza ya Roho Mtakatifu. Hii ingekuja kwao kupitia tu kuwekewa mikono ya kitume. Hivyo, *"...Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri"* (Matendo19:6).

**5. Ukomo wa nguvu za kimiujiza**

A. Tumeona hapo juu kwamba karama za kimiujiza zingeweza kutolewa na mitume pekee; na sio mtu mwingine yeyote. Kwa hiyo, mtume wa mwisho alipokufa, nguvu ya kutoa (au kugawa) karama ya miujiza ilikoma, na mtu wa mwisho aliyewekewa mikono na mtume alipokufa, kazi ya miujiza iliyofanywa na watu kanisani ilikoma milele.

B. Paulo anatwambia katika Waefeso 4:8-13 ni kwa muda gani karama hizi zitaendelea: *"hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo."* (13) Karama hizi zingeendelea mpaka maarifa ya Mwana wa Mungu

yatakapofunuliwa kikamilifu; mpaka Maandiko yatakapokuwa yamemalizika na kuthibitika. Katika ukamilifu wa ufunuo wa Mungu kulikuwa hakuna haja ya uvuvio, wala miujiza kuthibitisha ujumbe.

C. Paulo mara baada ya mjadala wake kuhusu karama za roho (1 Wakorintho 12) anaeleza ukomaji wa karama hizo: *"...ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika. Kwa maana tunafahamu kwa sehemu; na tunafanya unabii kwa sehemu; lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika"* (1 Wakorintho 13:8-10). Ni dhahiri kwamba karama hizi za roho hazikukusudiwa kuwepo siku zote: Unabii utabatilika; kunena kwa lugha za kimiujiza zitakoma, maarifa ya kimiujiza yatabatilika. Lini? Jibu: *"lakini ijapo ile iliyo kamili..."* (1 Wakorintho 13:10)(Fungu la 10). Walijua na kutoa unabii wa neno la Mungu kwa sehemu - ufunuo Wake ulifunuliwa kwao kwa sehemu hadi pale wote utakapokuwa umetolewa - lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika (ilitoweka). Vitabu kamili


vya Maandiko Matakatifu vilikamilika kwa kitabu cha Ufunuo; kwa hiyo karama za miujiza zikakoma.

D. Karama za miujiza za Roho zilikoma baada ya kukamilika kazi ambayo kwayo zilikuwa zimetolewa; kazi hizo ni: ufunuo na uthibitishaji wa mapenzi kamili ya Mungu. Kudai nguvu za kimiujiza leo ni sawa na kusema Biblia haijakamilika. Kwa hiyo hakuna haja ya ishara kama hakuna mtu mwenye ufunuo mpya wa kuthibitisha. Na hakuna mtu mwenye ufunuo wa ziada, maana mitume waliongozwa katika kweli yote (Yohana 16:13) - sio tu sehemu ya ukweli - na ulikuwa umekamilishwa na kitabu cha Ufunuo. Hakuna mwanadamu atakayeongeza kitu bila kuwa katika laana ya hukumu. *"Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki"* (Ufunuo 22:18). Hakuna ufunuo zaidi wa kuthibitisha; kwa hiyo, hakuna ishara zaidi kwa ajili ya kuzithibitisha.

# UCHUNGUZI NA HITIMISHO

# 23

## SABABU YA ISHIRINI NA TATU



## SABABU YA ISHIRINI NA TATU

# Kwa sababu ya mafundisho yake ya kimaandiko na ushikaji wa meza ya Bwana

### 1. Kumbukumbu

KANISA la Kristo linaadhimisha meza ya Bwana kama kumbukumbu nzuri na rahisi. Ni tukio takatifu kwa ajili ya Kumbukumbu ya Kristo. Paulo anasema, *"Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu"* (1 Wakorintho 11:23-25). *"Kwa ukumbusho wangu"* imetajwa mara mbili katika mafungu haya na mara moja katika Luka 22:19-23. Ni kwa ukumbusho wa Kristo, sio tu ukumbusho wa kifo chake, bali pia

kuzaliwa, maisha, na mafundisho yake, kwamba tule mkate na kunywa kikombe.

Tunaangalia ua kutoka katika kaburi la mama kwa kumbukumbu ya rafiki wa kweli wa kidunia; tunaangalia picha ya baba iliyofifia kwa kumbukumbu ya ambaye alitulea tungali tukiwa wadogo, tunaangalia fundo la nywele za mtoto, kwa kumbukumbu yake ambaye alikuwa nasi kwa muda mfupi tu; Mnara wa askari au kumbukizi ya kiafrika Dar es Salaam, Tanzania, ni kumbukizi kwa Maaskari (wanajeshi wa Afrika) waliopambana katika mapambano ya Uingereza dhidi ya jeshi la Ujerumani katika Afrika Mashariki katika vita kuu ya kwanza ya dunia (1914-1918);

[“Askari Monument.” Wikipedia, Wikimedia Foundation, 23 July 2021, en.wikipedia.org/wiki/Askari_Monument.]

pia tunakusanyika kwenye

meza ya Bwana na kushiriki meza ya Bwana kwa kumbukumbu ya Yeye aliyesema, "Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu."

Maua matakatifu yaliyowekwa ndani ya vifuniko vya Biblia yanavunjika katika vipande vipande na kutoa unga kadri muda unavyozidi kwenda; picha zilizotunzwa kwa upendo mkubwa zinabadilika kadri miaka inavyozidi kwenda na kuwa karatasi chafu ambazo hazitambuliki; Tofali pia zinakuwa zinafutika kadri muda unavyokwenda, lakini meza ya Bwana, ni kumbukumbu ambayo haivunjikivunjiki; haibadilishwi au kufutika kadri muda unavyozidi kwenda. Hali ya hewa au muda haviwezi kuizuia alama hii ya kumbukumbu katika kumkumbuka Kristo. Hata hivyo, unaweza kumsahau Bwana na hiki ndicho kitu kilichoiondoa hiyo alama maeneo mengi.

Kimeiangusha chini katika maeneo mengi. Kristo aliamuru ifanyike kwa kumbukumbu yake. Lakini watu wamemsahau Kristo katika kitu kile ambacho aliwaamuru wakifanye kwa

kumbukumbu yake. Yeremia alisema, *“Je! Mwanamwali aweza kusahau mapambo yake, au bibi arusi mavazi yake? Lakini watu wangu wamenisahau mimi kwa muda wa siku zisizo na hesabu”* (Yeremia 2:32). “Wakristo leo hawasahau kula, lakini mmenisahau katika meza ya Bwana kwa siku zisizokuwa na hesabu.” Uchunguzi mdogo utathibitisha ukweli huu. Kwa mfano, mhubiri mmoja alisema kwamba “kwenye kusanyiko lake” hawajawahi kushiriki meza ya Bwana kwa miaka kumi na minne.

B. Ni kumbukumbu inayohubiri kifo cha Yesu: *“Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo”* (1 Wakorintho 11:26). Meza ya Bwana ni shahidi wa kimya kimya wa dhabihu kubwa ya nyakati zote. Popote pale itaakapokuwa inaadhimishwa, iwe Mashariki, Magharibi, Kaskazini au Kusini, itawakumbusha watu, kwamba Yesu alikufa kwa ajili yao. Kama ilivyo “mnara wa askari” kule Dar es Salaam linavyochukua ushahidi wa

kifo cha askari kwa ajili ya nchi yake, ndivyo meza ya Bwana inavyobeba ushahidi wa kifo cha Bwana kwa ajili ya mwanadamu. Ni ushahidi wa kufaa ulioje! Wale wanaoshindwa kushiriki meza ya Bwana, kama Mungu anavyofundisha, wananyamazisha ushahidi huu. Kufanya hivyi sio busara.

C. Ni kumbukumbu inayohubiri kuja kwa Yesu kwa mara ya pili: *"Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo"* (1 Wakorintho 11:26). Tukitazama kwa kuangalia mambo ya nyuma, inatangaza kifo cha Bwana. Tukitazama kwa kuangalia mambo ya usoni, ni kumbusho la kila juma kwamba Bwana anakuja tena. Inaonyesha nyuma kwenye kifo chake na mbele katika ujio wake; tunahitaji kufaidika na vyote viwili kipindi kilichopita na kijacho kwamba tuweze kuwa tayari siku anapokuja.

D. Ni kumbukumbu inayohubiri Agano Jipya: *"...Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu..."* (1 Wakorintho 11:25). Kikombe, ishara ya damu

ya Kristo, ni ishara na uthibitisho wa agano jipya kati ya Mungu na mwanadamu.

**2. Mara ngapi tushiriki meza ya Bwana?**

A. Je kunatakiwa kuwe na idadi yoyote na utaratibu katika kufuata sehemu hii ya ibada? Kama ndivyo, nani atakuwa anasimamia kanuni? Kanisa au Mungu? Inakubaliwa kwamba hakuna mwanadamu mwenye mamlaka ya kusimamia na kudhibiti ibada ya mwingine. Basi, kwa kuwa hii ni kweli, mamlaka haya ni ya Mungu na sio mwanadamu. Je, Mungu katika kutumia mamlaka yake, amefundisha kundi moja kufanya kila mwaka, kundi jingine kila baada ya miezi sita, jingine kila robo, na jingine kila juma? Hapana. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba mwanadamu ameacha nafasi yake, na sasa anaingilia mamlaka ya Mungu, na anajaribu kudhibiti ibada ya mwanadamu kwa Mungu. Katika kujaribu kukwepa hitimisho hili, watu wanasema kwamba Mungu hajatufundisha ni mara ngapi tunatakiwa kushiriki meza ya Bwana na kwamba uadhimishaji wa kila mwaka,

kila baada ya miezi sita, kila robo au kila mwezi unakubalika, lakini hii inawaweka katika njia panda nyingine. Maana kama Mungu alitufundisha kwamba hakuna muda maalumu wa kushiriki meza ya Bwana, basi mtu anayeishiriki mara moja tu katika maisha yake yote amemtii Mungu na yupo sahihi kimaandiko kama mtu yeyote yule. Kwa hiyo, Biblia ina mengi ya kusema kuhusiana nayo kuliko watu wengi wanavyofikiri.

B. Kanisa la Yerusalemu lilidumu kuendelea kuadhimisha kwa: *"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali"* (Matendo 2:42). Fungu hili linaonesha ni jambo lililokuwa lina fanyika kwa kawaida na kwa kurudiwa na sio desturi ya kutokea mara moja. Zaidi inaonesha kuwa idadi ya uadhimishaji wake ilikuwa inajulikana vizuri kwa Teofilo na kwamba haikuwa na maana kumwandikia maelezo.

C. Kanisa la Troa walikutana pamoja katika siku ya kwanza ya juma kwa lengo la kuumega mkate: *"Hata*

*siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane"* (Matendo 20:7). Kutoka katika fungu hili tunapata yafuatayo:

(1) Wao kumega mkate katika siku hiyo ni jambo linalokubalika. Kama ingekuwa kosa, Paulo angewahukumu.

(2) Walikutana pamoja siku hiyo, siku ya kwanza ya juma, kwa lengo la msingi la kumega mkate. Siku gani ya kwanza ya juma? Kila juma linayo siku ambayo ni ya kwanza. Kuna siku moja tu ya kwanza katika juma. Hakuna juma lenye siku za kwanza zaidi ya moja.

(3) Je, hii inamaanisha walishiriki Meza ya Bwana siku ya kwanza ya kila juma? Fungu halisemi *"kila juma"* wala halisemi Mungu aliamuru Wayahudi kuitunza kila Sabato. Mungu alisema, *"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase"* (Kutoka 20:8). Walikuwa wamepewa jukumu la kuitunza Sabato. Ilikuja mara moja kwa kila juma; kwa hiyo walilazimika kuitunza kila juma. Mitume wa awali walikutana "siku ya

kwanza ya juma" ili kumega mkate, na walifanya hivyo kwa idhini ya kitume. Ikiwa tutafuata mfano huu ulioidhinishwa, Je, tutakutana mara ngapi ili kumega mkate? Mara kwa mara kila inapokuja siku ya kwanza ya Juma, na hiyo ni mara moja kwa juma, kila juma.

(4) Inapaswa ikubalike kwamba kukutana pamoja katika siku ya kwanza ya juma na kumega kwao mkate, kulingana na fungu hili, kulitokea mara kwa mara. Walikutana pamoja katika siku ya kwanza ya juma na walimega mkate katika siku ya kwanza ya juma. Wale wanaotenganisha umegaji wa mkate katika siku ya kwanza ya juma na kukutana siku ya kwanza ya juma wanafanya kitu ambacho hawana mamlaka nacho. Kuwa na msimamo thabiti kunahitaji waache kumega mkate katika siku ya kwanza ya juma, pia waache kukutana pamoja katika siku ya kwanza ya juma.

(5) Wale wanaokana kwamba fungu hili linafundisha kuadhimisha meza ya Bwana kila siku ya kwanza ya juma, watueleze wamejifunzaje kwamba

inatakiwa kuadhimishwa kila mwaka, kila baada ya miezi sita, kila robo, au kila mwezi?

D. Kwa nini uadhimishe kifo cha Bwana kila mwaka, kila robo au kila mwezi, lakini unaadhimisha ufufuo wake kila juma? Wote wanakubali kwamba siku ya kwanza ya juma inaadhimishwa kwa sababu ni siku ambayo Bwana alifufuka kutoka kaburini. Sasa, waadhimishaji wa kifo cha Bwana wa kila mwaka, kila baada ya miezi sita, kila robo na kila mwezi - maana meza ya Bwana inaonyesha kifo chake - wanaweza kutuambia kwa nini wanaadhimisha kufufuka kwa Yesu kila juma lakini wanaadhimisha kifo chake kila mwaka, kila baada ya miezi sita, kila robo au kila mwezi tu?

E. Kanisa la Korintho lilishiriki meza ya Bwana walipokutana, ilikuwa ni siku ya kwanza ya kila juma. Kwa kanisa la Korintho, ambao walikuwa wameiharibu meza ya Bwana kwa njaa na ulevi, Paulo alisema, *"Basi mkutanikapo pamoja haiwezekani kula chakula cha Bwana"* (1 Wakorintho 11:20). Ni dhahiri kwamba walikuwa

wanajaribu kushiriki meza ya Bwana kila walipokuwa wanakusanyika. Sasa kama kulikuwa na taratibu za kukutana kwao pamoja, kulikuwa vilevile na utaratibu wa kula Chakula cha Bwana. Hii inaonesha kukutana kwao mara kwa mara. *"Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja"* (1 Wakorintho 16:2). Mtu atauliza, "Je, hii ina maana ya siku ya kwanza ya kila juma?" Kama sio, kwa nini mnapitisha kikapu cha kukusanya sadaka kila siku ya kwanza ya juma? Kama haya sio mamlaka yenu, mamlaka yenu ni yapi sasa? Ndio, ina maanisha siku ya kwanza ya kila juma. Macknight pia anafasili kirai hiki vivyo hivyo. Hebu tuone tulichonacho:

(1) Ilikuwa kawaida yao kushiriki meza ya Bwana wanapokutana pamoja (1 Wakorintho 11:20).

(2) Ilikuwa kawaida yao kukutana kila siku ya kwanza ya juma (1 Wakorintho 16:2).

(3) Kwa hiyo, ilikuwa kawaida yao kushiriki meza ya Bwana kila siku ya kwanza ya

juma.

### 3. Nani anayeshiriki katika ushiriki meza ya Bwana

A. Tunaweza kujua nani atakayeshiriki kwa kujua nani alifanya; ambao ni:

(1) Washiriki wa Kanisa lililokwepo Yerusalemu (Matendo 2:42).

(2) Washiriki wa Kanisa lililokwepo Troa (Matendo 20:7).

(3) Washiriki wa Kanisa lililokwepo Korintho. (1 Wakorintho 11:20-33).

B. Wale waliopo katika ufalme: *"Nami nawawekea ninyi ufalme, kama vile Baba yangu alivyoniwekea mimi; mpate kula na kunywa mezani pangu katika ufalme wangu; na kuketi katika viti vya enzi, huku mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli."* (Luka 22:29-30). Inatakiwa ifanywe katika ufalme; hivyo ni raia tu wa ufalme ndio wenye sifa ya kibali hicho.

C. Ni meza ya Bwana na chakula cha Bwana, kwa hiyo, ni wale tu walio wa Bwana ndio wenye kushiriki.

D. Hata hivyo, hakuna mtu au kundi la watu wenye haki ya kuamua nani

atakuwa na nani hatakuwa na haki ya ushirika: *"Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe"* (1 Wakorintho 11:28). Kujihoji mwenyewe kulikoelezwa katika fungu hili kunahukumu fundisho la "ushirika uliofungwa", (ambalo ni wakati kundi la kidini linakukataza wewe kushiriki meza ya Bwana kama wewe sio mshirika wa kundi lao). Kila mtu anatakiwa ajichunguze; sio mtu mwingine. Ni tendo la ibadi ya mtu binafsi, ni ushirika wa Mkristo na Kristo (1 Wakorintho 10:16); hivyo, ni mamlaka iliyopo kwa Kristo badala ya mwanadamu, kwa sababu ni meza ya Bwana (chakula cha Bwana).

**4. Maswali kadhaa**

A. Kushiriki mara kwa mara kila juma kutaharibu umuhimu wake? Hapana, hakuna msingi katika hili. Ni sawa na kuhudhuria kanisani, kila mwaka, kila baada ya miezi sita, kila robo, au kila mwezi, mapungufu yake hayana tofauti.

B. Kula na kunywa isivyostahili ni nini? (1 Wakorintho 11:27) "Isivyostahili"

ni kielezi, kinachoelezea kitenzi kwa hiyo kinarejea namna ambavyo kitendo kinafanyika, siyo thamani ya mtu. Tafsiri nyingine ya fungu hili inasema "kwa namna isivyostahili" au "katika njia haimpendezi Mungu au kuonesha sheshima na taadhima kwa Mungu."

C. Maana ya *"kikombe"* ni nini? (1 Wakorintho 11:25) Inamaanisha kitu ambacho wangeweza kunywa; maana waliambiwa kukinywea; kwa hiyo, inamaanisha kitu kilichomo ndani ya kikombe, na sio kikombe au chombo chenyewe.

D. Je, mkate ulibadilika na kuwa mwili "halisi" wa Bwana; na tunda la mzabibu lilibadilika na kuwa damu "halisi"? (1 Wakorintho 11:25) Wakatoliki wanafikiria hivyo. Ni fundisho lao la "transubstantiation ya Katoliki" (Maelezo: mkate na divai vinabadilika kuwa mwili na damu halisi wakati wa meza ya Bwana kuwa mwili na damu halisi ya Kristo, hata ingawa vinaonekana kawaida). Kuna pia "consubstantiation ya Walutheri (mf KKKT)" (Maelezo: ambapo mwili/ mkate na damu/divai

vinakuwa pamoja katika muungano (kimoja kwa chenzake). Wanasema kuwa badiliko hili linafanyika hata leo inapokuwa "limebarikiwa" na Padre au Mchungaji. Yesu alichukua mkate akasema, "huu ni mwili wangu." Yesu alikuwa anaishi katika mwili; mwili wake wa kidunia; kwa hiyo, kama mkate ulibadilika na kuwa mwili wake halisi, basi alikuwa na miili miwili halisi kwa wakati mmoja. Yesu pia alisema, *"...Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu..."* (Luka 22:20), lakini kikombe hakikubadilika na kuwa damu yake halisi, kwa maana ilikuwa bado inatembea mwilini mwake. Ikiwa inamaanisha mwili na damu "halisi", basi kwa nini neno "halisi" linaongezwa wanapovielezea? Kwa kuliongeza hili neno ni ushahidi kwamba ni ishara ya damu badala ya damu halisi. Kwa nini tusichukulie kwamba kikombe hiki ni agano jipya halisi? Kwa nini unabisha kwamba kikombe hiki ni damu halisi lakini sio agano jipya? Yote yapo katika fungu moja: *"...Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu..."* (Luka 22:20). Kristo pia alisema. *"Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi..."* (Yohana

15:5). Kwa nini msiseme kwamba Kristo alikuwa mzabibu halisi na wanafunzi ni matawi halisi?

# UCHUNGUZI NA HITIMISHO

# 24

## SABABU YA ISHIRINI NA NNE



## SABABU YA ISHIRINI NA NNE

# Kwa sababu lina muziki wa kimaandiko wakati wa ibada

### 1. Utangulizi

Makundi yote ya kidini yanakubali kwamba muziki una nafasi katika ibada ya Agano Jipya, lakini hawakubaliani iwapo unapaswa uwe wa sauti bila vyombo vya muziki au uwe wa vyombo vya muziki, au sauti ikiambatana na vyombo vya muziki; hata hivyo Agano Jipya, wataalamu wa vitabu vikuu, wanahistoria, na watoa maoni wameelezea kwa urahisi mafundisho na desturi za kanisa la Agano Jipya.

A. Mwandishi ametaja kwa kurudiarudia kanuni ongozi katika kanisa la Kristo ni: "Zungumza pale ambapo Biblia inazungumza na nyamaza pele ambapo Biblia imenyamaza." Kuzingatia kikamilifu kanuni hii ya msingi ni sababu ya kuondoa muziki wa vyombo katika ibada za makanisa ya Kristo.

**2. Muziki uliofundishwa katika Agano Jipya**

A. Hii ni kumbukumbu ya muziki uliotajwa katika Agano Jipya:

(1) *"Nao walipokwisha kuimba, wakatoka nje kwenda mlima wa Mizeituni"* (Mathayo 26:30).

(2) *"Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza"* (Matendo 16:25).

(3) *"... Kwa hiyo nitakushukuru kati ya Mataifa, Nami nitaliimbia jina lako"* (Warumi 15:9).

(4) *"...mtaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia"* (1 Wakorintho 14:15).

(5) *"mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu"* (Waefeso 5:19).

(6) *"Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu"* (Wakolosai 3:16).

(7) *"...Katikati ya kanisa nitakuimbia sifa"* (Waebrania 2:12).

(8) *"Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake"* (Waebrania 13:15).

(9) *"Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? Na aombe. Ana moyo wa kuchangamka? Na aimbe zaburi"* (Yakobo 5:13).

B. Kristo hakufundisha matumizi ya vyombo vya mziki katika ibada. Hoja hii inajibu swali kuhusu matumizi ya vyombo vya mziki. Kanisa la Kristo ni kundi la Agano Jipya, na Agano Jipya linatuambia mambo ambayo Bwana ameyaweka katika ibada. Tumeona kwamba Agano Jipya lipo kimya kuhusiana na muziki wa vyombo katika ibada. Ni dhahiri kwamba wale wanaovitumia katika ibada wanafanya

hivyo pasipo mamlaka ya Biblia. Hatutakiwi kuongeza katika kielelezo (mpangilio) cha Mungu.

C. Kuna aina mbili za amri: mahususi na za jumla. Kwa mfano, *"Ujifanyie safina ya mti wa mvinje..."* (Mwazo 6:14) ni amri mahususi. Mungu alibainisha mti na hiyo ikawa mwisho wa mada kuhusiana na aina ya mti. Mungu hakusema, "Usitumie aina yoyote ya mti;" lakini ukweli kwamba Mungu alibainisha matumizi ya mti wa mvinje kulizuia matumizi ya aina nyingine. Na kama Mungu angesema, "Ujifanyie safina ya mti," matumizi ya aina yoyote ya mti yangekidhi amri hii ya jumla. Pia, kama Agano Jipya lingesema, "Ujifanyie muziki," tungekuwa tunaendana na matakwa ama kwa kujifanyia muziki wa sauti au muziki wa vyombo, au vyote. Hata hivyo, Mungu hakusema hivyo. Alisema, "imbeni," na hili linazuia muziki wa vyombo na kuagiza kuimba nyimbo zisizo na ala (acapella). Ubainishaji na umahususi upo bayana hapa kama ilivyokuwa amri ya kujenga safina kwa kutumia mti wa mvinje. Amri mahususi ya kuimba

inatosha kwa wale ambao wako radhi kwenda kwa neno la Mungu na kufanya kile asemacho kwa sababu alikisema.

### 3. Hitimisho juu ya hoja kubwa na ndogo

Mjadala uliotangulia unatuandaa kwa ajili ya uchunguzi zaidi juu ya mada hii. Huku tukiwa tumeiandaa akili yetu, tunazingatia hoja zifuatazo:

#### 1. Hoja ya kwanza:

(1) Kila andiko linatolewa ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa ili apate kutenda kila tendo jema (2 Timotheo 3:16-17).

(2) Hakuna andiko linaloidhinisha muziki wa vyombo katika ibada leo (haliwezi kupatikana).

(3) Kwa hiyo, muziki wa vyombo katika ibada sio tendo jema.

#### 2. Hoja ya pili:

(1) Ni ukiukaji wa mapenzi ya Mungu kufanya vitu zaidi ya vile vilivyoandikwa (1 Wakorintho 4:6).

(2) Ibada ya muziki wa vyombo katika Agano Jipya haikuandikwa (andiko hili halipo).

(3) Kwa hiyo, wale wanaotumia vyombo vya muziki katika ibada leo wanakwenda kinyume na mapenzi ya Mungu.

**3. Hoja ya tatu:**

(1) *"Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo"* (Warumi 10:17).

(2) Neno la Mungu halituambii kutumia vyombo vya muziki katika ibada (andiko hili halipo).

(3) Kwa hiyo, muziki wa vyombo katika ibada sio tendo la imani.

**4. Hoja ya nne:**

(1) Mungu ametukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa (2 Petro 1:3).

(2) Kile ambacho Mungu ametupatia hakisemi kuhusu muziki wa vyombo katika ibada ya Agano Jipya (andiko hili halipo).

(3) Kwa hiyo, muziki wa vyombo katika ibada havihusiani na uzima na utauwa.

**4. *"Psallo"***

A. Baadhi ya watu wanauliza, "Je, neno

la Kiyunani '*psallo*' halijumuishi kupiga vyombo?" Baadhi ya watu wanatetea madai yao kwa kujikita katika neno hili lakini kama endapo watafikiri kidogo tu wataacha kuendelea kutetea hoja hii. Ikiwa neno la asili ambalo kwalo tunapata neno "imba" linamanisha na kujumuisha upigaji wa vifaa vya muziki, basi hatuwezi kuwa tunatii amri ya Mungu kuimba kama kila mmoja wetu hatapiga chombo cha muziki katika kusanyiko. Sasa nani yupo tayari kusema kwamba kupiga vyombo vya muziki kumejumuishwa katika neno la Kiyunani "*psallo*"? Ndio, nani atasema kwamba kila mtu ambaye anajaribu kumwabudu Mungu bila kupiga vifaa vya muziki anakiuka amri ya Mungu?

B. Fasili ya *psallo*. Katika kitabu cha *M. C. Kurfee, Instrumental Music in the Worship, hakimiliki na McQuiddy Printing Co., Nashville, Tennessee, uk.16*, kuna muhtasari wa fasili ya neno "*psallo*" kama ilivyotolewa katika 17 Leksikoni ya Kiyunani-Kiingereza, kama ifuatavyo: "

(1) Vuta nywele.

(2) Kuvuta nyuzi (kama nyuzi na upinde).

(3) Kuvuta kwa ghafula mstari wa seremala.

(4) Kugusa nyuzi za kifaa cha muziki, yaani, kutengeneza muziki wa ala.

(5) Kugusa hisia za moyo wa mwanadamu, yaani kuimba, kushangilia kwa sifa kutoka kwa mwanadamu kwenda kwa Mungu."

Kwa kuwa neno la Kiyunani "*psallo*" limebeba maana tano tofauti katika nyakati tofauti, maana gani tutakayoichukua na kusema ni maana ya Agano Jipya? Ni dhahiri kabisa kwamba maana ni "kuimba," kwa sababu sauti ya kushangilia ilifanywa na moyo wa mwanadamu: *"...mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu"* (Waefeso 5:19). Kwa hiyo, maana ya Agano Jipya sio kuvuta nywele; kuvuta nyuzi, kuvuta kwa ghafula mstari wa seremala; kugusa nyuzi za kifaa cha muziki; bali ni kupiga nyuzi (kugusa hisia) za moyo wa mwanadamu, maana hicho ndicho kifaa ambacho kwacho sauti inapaswa kufanywa moyoni.

**5. Matamko ya viongozi wa dini**

Viongozi mbalimbali wa kidini wameandika na kuzungumza kwa kauli moja juu ya swala la muziki. Hebu tuangalie baadhi yao:

A. John Calvin, amesimama kama mmoja wa waanzilishi wa Kanisa la Presbiteri: "Vifaa vya muziki katika kumshangilia na kumsifu Mungu hakuna tofauti na kuchoma ubani, kuwasha mishumaa, kurejesha vivuli vingine vya sheria. Kwa hiyo, Warumi, wameazima hili kwa upumbavu, pamoja na mambo mengine mengi kutoka kwa Wayahudi. ."— *Maoni ya John Calvin, Zaburi ya thelathini na tatu.*

B. Adam Clarke, Mtoa maoni mkubwa zaidi wa Kimethodisti: "Muziki kama sayansi, ninaupenda na kuutamani: lakini vifaa vya muziki katika nyumba ya Mungu ninavichukia na kuvidharau. Haya ni matumizi mabaya ya muziki; na hapa napinga waziwazi uharibifu huu katika ibada ya Mwandishi wa kikristo."— *Clarke's Commentary, Juz. IV., Uk. 686.*

C. John Wesley, mtu mashuhuri na mwanzilishi wa Kanisa la Methodisti

amenukuliwa na Adam Clarke akisema: "Sina kipingamizi na vifaa vya muziki katika makanisa yetu, ili mradi tu havisikiki wala kuonekana". *—Clarke's Commentary, Juz. IV., uk. 686.*

D. Martin Luther, mwanamatengenezo anayeheshimika, "aliita ala hii bendera ya Baal"*—McClintock & Strong's Encyclopedia, Music, Vol. VI., uk. 762.*

E. John Knox, mwanamatengenezo wa Kiskochi, alikiita chombo cha muziki kinachoitwa 'ala' (organ) "kist" (sanduku la kutunzia samani) la miluzi (kelele).*—McClintock & Strong's Encyclopedia, Music, Vol. VI., uk. 762.*

F. Charles H. Spurgeon, anatambulika kama mhubiri mkubwa sana wa Kibaptisti ambaye amewahi kuishi, alihubiri kwa miaka ishirini kwenye maelfu ya watu, kila juma katika Madhabahu Kuu ya Baptisti, London, Uingereza, hawakuwa na vifaa vya muziki katika ibada.*—M. C. Kurfees, Instrumental Music in the Worship, uk.196.*

G. Conybeare na Howson, wanazuoni

maarufu wa kanisa la Uingereza, katika maoni ya Waefeso 5:19, wanasema, "Jifanyie sauti za muziki katika mioyo yenu, kwa Bwana... nyimbo zenu, zisiwe kunywa katika karamu za kidunia (kipagani), bali zaburi na nyimbo (nyimbo za kiroho); na vinavyofuatana navyo sio muziki wa vyombo vyenye nyuzi, bali kushangilia moyoni"—*Life and Epistles of St. Paul, Juz. II, uk. 408.*

Viongozi wa kidini hapo juu, hakuna hata mmoja wao ambaye alikuwa mshirika wa kanisa la Kristo, wamenukuliwa sio kwa lengo la kuonesha matumizi ya vifaa vya muziki katika ibada sio sahihi - ukweli kwamba Kristo alithibitisha hivyo - bali ni kuonesha kwamba vimekataliwa na viongozi wengi wa kidini duniani. Ikiwa hakuna mtu aliyefundishwa kwamba vifaa vya muziki katika ibada sio sahihi, hakuwezi kubadili fundisho la Agano Jipya; lakini ni dhahiri kwamba wengine wamechukua msimamo ule ule, na kwamba hapa hatujasimama peke yetu kwa namna yoyote ile. Wanahistoria, wanasaikolopedia na viongozi wa dini

wanakubaliana kwamba sifa za muziki katika Agano Jipya ni sifa ya muziki katika makanisa ya Kristo.

**6. Jitihada za kuthibitisha vifaa vya muziki katika ibada**

Licha ya kwamba ibada ya muziki wa sauti bila vyombo kuwa ya kimaandiko, bado kuna mapingamizi dhidi yake, na jitihada zinafanyika kuthibitisha muziki wa vyombo. Baadhi ya jitihada hizi ni kama ifuatavyo:

A. Baadhi wanajaribu kuthibitisha muziki wa vyombo katika Agano Jipya kwa kusema kwamba ulikuwa na sehemu katika ibada ya Agano la Kale. Ikiwa kigezo hicho kinaidhinisha upigaji wa vyombo vya muziki katika ibada, kitaidhinisha pia utoaji wa sadaka ya wanyama na uchomaji wa ubani katika ibada. Ikiwa watu wanaleta vifaa vya muziki katika ibada leo kwa kusema kwamba vilitajwa katika Agano la Kale, kwa hili kuwa katika msimamo thabiti ni lazima kwamba walete pia sadaka za wanyama na kuchoma ubani katika ibada. Ikiwa mtu anaacha kutoa sadaka za wanyama na uchomaji wa

ubani katika ibada leo kwa misingi kwamba Yesu hakuviweka katika Agano Jipya, anapaswa pia aache upigaji wa vyombo vya muziki kwa sababu hizo hizo. (Kwamba leo tunaishi chini ya sheria ya Agano Jipya wala si katika mamlaka ya Agano la Kale, tazama Sura ya Kumi.)

B. Inasemwa pia kwamba ni sahihi kuwa na vifaa vya muziki katika ibada kwa sababu vinubi vimetajwa mbinguni. Kuhusisha mambo yaliyotajwa mbinguni katika ibada ya kanisani hapa duniani kunawapelekea watu katika matatizo makubwa kuliko walivyotarajia. Kwa mfano, fungu linalotaja vinubi pia linataja *"vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato"* (Ufunuo 5:8). Je, ni sahihi kuwa na manukato katika ibada eti kwa sababu yametajwa kuwepo mbinguni? Hapana! Lakini kuna mamlaka yale yale kwa manukato kuwepo katika ibada kama ilivyo kwa kinubi au kifaa kinginecho cha muziki, ambavyo vyote havitakiwi.Kama manukato haya yaliyotajwa mbingunii ni ya kiishara au halisi, hakika nitakubaliana nayo.

Na vinubi vilivyopoa katika jiji la mbinguni, viwe halisi au vya lugha ya picha, nitapendezwa navyo. Na kama Mungu aliweka kanisani ama kinubi au kuchoma ubani, au vyote, kwa upande wangu wala nisingepingana navyo, lakini hajaweka chochote kati ya hivyo kwenye kanisa lake.

C. Kundi jingine wanadai kwamba hakuna mamlaka kwa ajili ya matumizi ya vifaa vya muziki katika ibada, lakini wanasisitiza kwamba ni jambo la manufaa (kitu cha uchaguzi - *expedient*), sio suala la kujali, kitu tunachoweza kuwa nacho au kutokuwa nacho. Kama ni suala la kutojali, kwa nini wasiache kutumia wakati wa ibada pale ambapo wengine wanapinga kabisa? Kwa nini kusisitiza kutumia jambo ambalo linasababisha faraka kama ni la kuchagua na si la lazima? Wale ambao hawajali suala hili, sio kwamba ni watu wasiojali kwa sababu ya kitu chenye manufaa, bali ni watu wasiojali na matokeo yake wanakuwa watu wasiojali kanuni za msingi za kiungu za bila kuongeza au kuondoa.

D. Inadaiwa kuwa matumizi ya ala ni

halali kwa sababu zinasaidia kuimba. Haijalishi kama vifaa vinasadia kuimba au la, inategegemeana na lengo la kuimba. Kama tunafanya muziki kwa lengo la kuburudisha hadhara, kujionyesha, kuwashawishi wale ambao hawana shauku ya kuabudu katika roho na kweli, basi vifaa vinaweza kuwa msaada. Hata hivyo, hili sio lengo letu la kuimba. Lengo moja ni kufundisha na kuonyana (Wakolosai 3:16) Je, kupiga vyombo kutatusaidia kufundisha na kuonya? Hapana! Mara nyingi vina sauti kubwa kiasi kwamba huwezi kusikia maneno na kufanya tusiweze kufundishwa na kuonywa. Kwa hiyo, vinaingilia moja ya malengo ya kuimba, badala ya kusaidia kuimba.

E. Jaribio la kuhalalisha vifaa vya muziki linafanywa kwa kusema kwamba huwa tunatumia "*kifaa kitoacho noti kwa sauti ya chini na ndogo*" kifaa ambacho hutoa sauti tulivu sana ya noti ya kuanzishia wimbo ambayo viongozi wa wimbo tu wanaweza kusikia. Hoja hii ni dhaifu sana, na inaonesha ni vigumu kwa wao kupata uthibitisho dhidi ya mafundisho hayo, kwa sababu vifaa

vya muziki na "*kifaa kitoacho noti kwa sauti ya chini na ndogo*" sio kitu kimoja, na hata kama vingekuwa ni kitu kimoja, kusingethibitisha kwamba vinakubalika mbele za Mungu eti kwa sababu tunatumia "*kifaa kitoacho noti kwa sauti ya chini na ndogo*". Nukuu ifuatayo itatusaidia: "Chochote kile ambacho ni muhimu kufanya amri inahusishwa kwenye amri; kutoa sauti kunahusishwa katika amri ili kuimba.... Unapotumia "*kifaa kitoacho noti kwa sauti ya chini na ndogo*" kupata noti, hakuna linalofanyika bila ya kuimba wala lisilofanyika bila noti.  Kifaa hiki hakitumiki wakati wa kuimba. Lakini kifaa cha muziki kinapotumika pamoja na kuimba, kitu fulani kinafanyika ambacho hakiwezi kufanyika bila kukitumia, mfano aina nyingine ya muziki inafanyika kwa wakati mmoja pamoja nacho hufanywa kwa sauti ya binadamu. Ni kumsifu Mungu kwa kutumia aina mbili za muziki wakati Mungu mwenyewe amechagua na kuteua aina moja tu."—Nukuu kutoka *"Walking by Faith" katika Makala ya M. C. Kurfee, Review of John B. Cowden's Tract on Instrumental*

*Music in the Church, uk..28.*

F. Wakati fulani tunasikia, "Una muziki wa vyombo nyumbani kwako. Wanasema, ikiwa unaweza kuwa nao nyumbani, basi unaweza kuwa nao kwenye ibada." Hapana. Tuna vitu vingi sana nyumbani ambavyo havipo kwenye ibada. Tunasugua vyungu na masufuria tunapokuwa nyumbani, lakini hatufanyi hivyo tunapokutanika kwa ajili ya ibada. Tuna kula kuku na wali nyumbani, lakini tunakula mkate na kunywa kinywaji cha mzabibu tu tunapokuwa katika meza ya Bwana. Mungu aliamuru kutumia mkate na mzabibu kutumia, na hivyo kuzuia kutumia chakula chochote kile tunapokuwa katika meza ya Bwana, vivyo hivyo, Bwana ametuamuru kuimba, kufanya muziki wa sauti za mdomo, na hiyo inatuzuia kufanya aina nyingine yoyote ya muziki.

G. Wengine wamesema, "Biblia haisemi tusiwe navyo." Je, hiyo inathibitisha kwamba inakubalika kwa Mungu? Kama ndivyo, inathibitisha kwamba uchomaji wa ubani; kwa maana hakuna sehemu ilipoandikwa "Usichome

manukato katika ibada." Hii pia ingeweza kuthibitisha kwamba soda (Pepsi au CocaCola) au maandazi vinakubalika katika meza ya Bwana; kwa maana hakuna sehemu ilipoandikwa "Usinywe soda (Pepsi au CocaCola) katika meza ya Bwana" au "Usile maandazi katika meza ya Bwana." Kanuni potofu kama hiyo katika dini inajikita katika wazo la kuongozwa na kile ambacho Biblia haisemi badala ya kile inachosema. Kumpendeza Mungu, tunapaswa kuongozwa na kile alichokisema, kwa sababu ametuonya tusifanye zaidi ya vitu vilivyoandikwa (1 Wakorintho 4:6). Tunaweza kuzingatia onyo hili!

## UCHUNGUZI NA HITIMISHO

# 25

## SABABU YA ISHIRINI NA TANO



## SABABU YA ISHIRINI NA TANO

# Kwa sababu wokovu upo katika kanisa la Kristo

### 1. Utangulizi

Wahubiri wengi wa kimadhehebu wanasema kwamba mtu sio lazima awe mshirika wa kanisa ili aweze kuokolewa. Ikiwa wanamaanisha madhehebu, taasisi ambayo kwayo wao ni washiriki, wapo sahihi. Ikiwa wanamaanisha kanisa lililonunuliwa na damu, hawapo sahihi.

A. Ikiwa mtu anaweza kuokolewa akiwa nje ya dhehebu vile vile akiwa ndani yake, kwa nini awe ndani yake? Kwa nini unahubiri na kuwataka wengine wawe washiriki wa kanisa hilo, kama hakuna wokovu ndani yake? Wafanyakazi kama hao hawafanyi kwa lengo la kuwaokoa waliopotea, bali ni kwa lengo la kuwashawishi watu wabadili imani kwa kufuata kanuni za kidini za mafundisho ya kibinadamu, na kujenga taasisi ya kidini ya kibinadamu

ambayo kwayo hakuna wokovu.

B. Kanisa lolote ambalo halileti wokovu kwa mwanadamu sio kanisa la Kristo, kwa sababu kuwa na ushirika katika kanisa lake ni muhimu ili uweze kuokolewa. Hii ni sababu ya ishirini na tano iliyotolewa kwako ili uweze kuwa mshirika wa kanisa la Kristo.



**2. Ushirika katika kanisa la Kristo ni lazima ili kupata wokovu**

A. Wokovu upo ndani ya kanisa, kwa sababu ni taasisi iliyonunuliwa kwa damu: *"...kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe"* (Matendo 20:28).

Paulo alisema kwa washiriki wa Kanisa huko Korinto, *"...Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani..."* (1 Wakorintho 6:19-20). Gharama hiyo ilikuwa ni damu ya Kristo. Hebu tuangalie

baadhi ya hoja:

(1) Washiriki wa kanisa walinunuliwa kwa damu; kwa hiyo, wasio washiriki hawakununuliwa kwa damu. Nani anaweza kusema mtu anaweza kuokolewa pasipo damu?

(2) Kanisa ni kitu pekee kilichonunuliwa kwa damu (Matendo 20:28); kwa hiyo, wale ambao hawapo kanisani, hawajanunuliwa kwa damu.

(3) Kanisa lilinunuliwa kwa damu ya Kristo (Matendo 20:28); kwa hiyo, kama kanisa sio taasisi ya lazima, Mungu alitoa damu ya Kristo bure.. Kila mtu anayesema kwamba mtu anaweza kuokolewa nje ya kanisa anakuwa analeta mashitaka dhidi ya Mungu. Ni sawa na kumshitaki Mungu kwamba ni rafiki asiyekuwa na huruma aliyetumia damu ya Mwana wake kununua taasisi isiyokuwa na umuhimu. Hatuthubutu kwa maneno wala kwa matendo kuleta mashitaka ya namna hiyo dhidi ya "Baba wa huruma na Mungu wa faraja"!

B. Wokovu umo ndani ya kanisa, maana Paulo aliahidi kwamba Kristo ataliokoa

kanisa: *"Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili"* (Waefeso 5:23). Mwili ni kanisa (Wakolosai 1:18). Hivyo, Kristo ni Mwokozi wa mwili au kanisa. Kwa kuwa hii ni kweli, vipi kuhusu wasiokuwa washirika? Wanaishi duniani bila ahadi au tumaini.

C. Wokovu upo ndani ya kanisa, kwa sababu lipo ili mwanadamu aweze kupatanishwa na Mungu: *"Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba"* (Waefeso 2:16). Paulo anaubainisha mwili ni kanisa (Wakolosai 1:18). Angalia orodha za hoja na hitimisho:

(1) Inakubaliwa kwamba mtu lazima apatanishwe na Mungu ili aweze kuokolewa.

(2) Upatanisho kutoka kwa Mungu upo katika mwili au kanisa (Waefeso 2:16; Wakolosai 1:18).

(3) Kwa hiyo mtu ni lazima awe kanisani ili aweze kuokolewa.

D. Wokovu upo kanisani, kwa sababu hili ndilo kundi ambalo Kristo atajiletea mwenyewe: *"apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa"* (Waefeso 5:27). Kristo mwenyewe atajiletea kanisa hilo. Kama sisi ni washiriki wa kanisa, basi yote yapo sawa. Kama sivyo, tuliwezaje kutarajia kuwa mbele za Kristo? Jibu letu pekee ni mwangwi na kimya.

E. Mtu hawezi kuokolewa akiwa nje ya kanisa, kwa sababu Mungu anawaongeza humo wale wote waliookolewa: *"...Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa"* (Matendo 2:47). Katika toleo la King James (Kiingereza) tunapata maneno haya: "... Na Mungu akawaongeza kanisani, kila siku, ili kwamba waweze kuokolewa." Katika toleo la Swahili Union Version (SUV) tunapata maneno haya: "...Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."

Katika tukio hili watu elfu tatu waliongezwa kanisani. Katika hali yao

ya kupotea hawakuwa washirika, lakini katika hali yao ya kuokolewa walikuwa washirika. Kwa hiyo tunaona kwamba, kuokolewa kulikuwa ni kuongezwa kanisani. Wasingeweza kuokolewa bila kuwa washirika wa kanisa. Hii inaweka wazi kwamba matakwa ya wokovu na matakwa ya kuwa mshirika wa kanisa yanafanana. Hii ina maana kwamba wote waliopotea, sio washirika, na wote waliookolewa ni washirika. Hivyo, wokovu upo kanisani kwa sababu unajumuisha wale wote waliookolewa. Vipi kuhusu watoto wachanga na watu wenye ulemavu wa akili? Je, wapo kanisani? Hapana. Wapo salama, hawajaokolewa, kwa sababu hawajawahi kupotea katika dhambi.

F. Kama ni lazima kuwa mwana katika familia ya Mungu kusudi uokolewe, unatakiwa uwe mshirika wa kanisa la Mungu ili uweze kuokolewa. Hili ni kweli kwasababu Paulo anasema kwamba familia ya Mungu (nyumba yake) ni kanisa la Mungu. *"Lakini nikikawia, upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye*

*hai, nguzo na msingi wa kweli"* (1 Timotheo 3:15). Nyumba ya Mungu ni kanisa la Mungu, na nyumba ni familia. Tunasoma uongofu wa mlinzi wa gereza na nyumba yake (Matendo 16:29-34), lakini ilikuwa ni familia yake iliyoongolewa badala ya makazi. Pia tunasoma kuwa Kornelio *"mtu mtauwa, mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima"* (Matendo 10:2), lakini ilikuwa ni familia yake waliomcha Mungu badala ya makazi yake. Nyumba ya Mungu, familia ya Mungu, ni kanisa la Mungu. Mtu akiwa katika familia ya Mungu, yupo katika kanisa la Mungu. Ikiwa hayupo katika kanisa la Mungu, basi hayupo katika familia ya Mungu. Kama hayupo katika familia ya Mungu basi, basi sio mtoto wa Mungu, kwa sababu Mungu hana watoto nje ya familia yake. Wahubiri wanaofundisha kwamba mtu anaweza kuwa mtoto wa Mungu na bila kuwa mshirika wa kanisa la Mungu au familia wanafundisha kwamba Mungu ana watoto nje ya familia yake, na hivyo ana hatia ya uzinzi wa kiroho. Hii inashutumu jina

la Mungu!

G. Yesu, Mchungaji wa kondoo, alifundisha kwamba mtu lazima aingie kundini ili aweze kuokolewa: *"Mimi ndimi mlango; mtu akiingia kwa mimi, ataokoka..."* (Yohana 10:9).

(1) Wokovu upo ndani ya kundi (Yohana 10:9).

(2) Kundi ni kanisa (Matendo 20:28)

(3) Kwa hiyo, wokovu upo ndani ya kanisa.

H. Mtu hawezi kuokolewa akiwa nje ya kanisa, kwa sababu hawezi kuokolewa bila kuwa tawi katika mzabibu. Yesu, akizungumza na na wanafunzi wake alisema, *"Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi"* (Yohana 15:5). Kristo na wanafunzi wake wanatengeneza mmea wa kutukuka. Mtu hawezi kuokolewa pasipo mmea huu, kwa maana Yesu alisema katika fungu la kumi na tano, *"maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote"*

I. Haiwezekani kuokolewa ukiwa nje ya kanisa, kwa sababu haiwezekani kuokolewa bila kuhesabiwa haki: *"... na wale aliowaita, hao akawahesabia*

*haki..."* (Warumi 8:30). *"... ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja..."* (Wakolosai 3:15), na mwili ni kanisa (Wakolosai 1:18). Zingatia:

(1) Walioitwa wamehesabiwa haki.

(2) Walioitwa wapo katika mwili, ndani ya kanisa.

(3) Kwa hiyo, waliohesabiwa haki wapo kanisani. Hii inaweka wazi kwamba kama mtu hayupo kanisani, anakuwa hajahesabiwa haki.

J. Haiwezekani kuokolewa nje ya kanisa, kwa sababu haiwezekani kuokolewa bila kutuhamisha (kutuokoa) kutoka katika nguvu za giza: *"Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake"* (Wakolosai 1:13) Wale walio katika ufalme - na ufalme ni kanisa (Mathayo 16:18-19) - wamekwisha kuokolewa kutoka katika nguvu za giza. Kwa hiyo, wale ambao hawapo katika ufalme hawajaokolewa kutoka katika nguvu za giza. Watu walio nje ya ufalme au kanisa wanahitaji kufumbuliwa macho yao *"...na kuwageuza waiache giza na*

*kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi"* (Matendo 26:18).

K. Hebu tuangalie hema kama mfano. Kulikuwa na patakatifu na patakatifu pa patakatifu. Mfano unaweza kupelekwa mbali mno, lakini inaonekana Maandiko yanahakikisha maneno yetu kwamba patakatifu palikuwa ni mfano wa kanisa na patakatifu pa patakatifu palikuwa ni mfano wa mbingu. (Waebrania 8, Waebrania 9, Waebrania 10). Hoja ni hii hapa: Walilazimika kupitia patakatifu ili waweze kufika patakatifu. Kwa hiyo, Biblia inafundisha kwamba, mtu anatakiwa apitie katika kanisa ili aweze kufika mbinguni.

## 3. JE, KANISA NI TAASISI ISIYOJULIKANA?

Baadhi wanasema, "Ndiyo, unatakiwa uwe katika kanisa la Kristo ili uweze kuokolewa, lakini ni kanisa lisiloonekana, la siri, kitu ambacho hakuna mtu akijuaye." Hii sio kweli.

(1) Inatambulika kwamba watu elfu tatu waliuongezwa katika kanisa siku ya Pentekoste (Matendo 2:41,47). Hawakuongezwa hadi walipobatizwa (Matendo 2:41). Kwa hiyo, Mungu hatawaongeza watu ambao hawajabatizwa leo, kwa sababu yeye habagui watu (Matendo 10:34).

(2) Ipo dhahiri kwamba mateso makubwa yalilikumba kanisa *"...lililokuwa katika Yerusalemu; wote wakatawanyika..."* (Matendo 8:1).

(3) Kanisa hili linauwezo wakujulikana na linajulikana katika jamii nyingi, na ndio tunaona katika Agano Jipya barua zinatumwa katika jumuiya mbalimbali: Korintho, Galatia, Thesalonike, n.k. Kanisa lilikuwa na uwezokano wa kufahamika (kujulikana).

## 4. Maadili

Baadhi ya watu wanajenga hoja kwamba watu wenye maadili, raia wema wenye maisha safi, wanaweza kwenda mbinguni, bila kujali uhusiano wao na Ukristo.

## Kama hii ingekuwa kweli........

1. Mtu angeokolewa bila Kristo kuja duniani lakini alikuja kuokoa (Yohana 3:17).
2. Mtu angeweza kuokolewa bila Yesu kupigwa, lakini tunaokolewa kwa kupigwa kwake (1 Petro 2:24).
3. Mtu angeweza kuokolewa bila kifo cha Yesu, lakini alikufa kwa ajili ya dhambi zetu (1 Wakorintho 15:3).
4. Mtu angehesabiwa haki bila ufufuo wa Kristo, lakini alifufuka ili tuhesabiwe haki (Warumi 4:25).
5. Tungeweza kuokolewa pasipo damu, lakini tumepata ukombozi wetu kupitia damu yake. (Waefeso 1:7).
6. Watu wangempendeza Mungu bila imani, lakini bila imani haiwezekani kumpendeza Mungu (Waebrania 11:6).
7. Mtu angeweza kuokolewa bila kutubu, lakini wale ambao hawatubu watapotea (Luka 13:3).
8. Mtu angeweza kumkana Kristo na akaokolewa, lakini wale wanaomkana Kristo watakanwa mbele ya Baba (Mathayo 10:33).

## Kama hii ingekuwa kweli........

9. Mtu angeokolewa bila kubatizwa, lakini ubatizo unaokoa (1 Petro 3:20-21).
10. Watu wangeweza kuokolewa pasipo kuzaliwa upya, lakini watu lazima wabatizwe ili wauone ufalme wa Mungu (Yohana 3:5).
11. Tungeweza kuokolewa bila kutii injili, lakini Kristo atalipiza kisasi kwa wale ambao hawataitii injili (2 Wathesalonike 1:8).
12. Mtu angeweza kuokolewa bila kuongolewa, lakini lazima aongolewe ili aingie katika ufalme wa mbinguni (Mathayo 18:3).
13. Tungeweza kuokolewa bila kuujua ukweli, lakini lazima tuujue ukweli ili tuwe huru (Yohana 8:32).
14. Tungeweza kuokolewa bila kupenda ukweli, lakini wale wasiopenda ukweli watapotea (2 Wathesalonike 2:10).
15. Mtu angeweza kuokolewa pasipo Kristo, lakini pasipo Kristo hawezi kufanya chochote (Yohana 15:5).
16. Mtu angeweza kuokolewa pasipo jina la Kristo,  lakini hakuna wokovu katika

jina jingine (Matendo 4:12)

17. Mtu angeweza kuokolewa nje ya mwili, lakini Kristo ni Mwokozi wa mwili (Waefeso 5:23).
18. Kornelio angekuwa amekwisha okolewa, lakini hakuokolewa hadi alipotii (Matendo 11:14).

# UCHUNGUZI NA HITIMISHO

# Kiambatanisho na Nyongeza 1



# MATHAYO 16:18

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Strong's # | 2504 | 1161 | 4771 | 3004 | 3754 | 4771 |
| Transliteration | kagō | de | soi | legō | hoti | sy |
| Kigriki | κἀγὼ | δέ | σοι | λέγω , | ὅτι | σὺ |
| Kiswahili | | Nami | naku- | -ambia | | Wewe |
| Kingereza | I also | moreover | to you | say | That | you |
| | | | | | | |
| Strong's # | 1510 | 4074 | 2532 | 1909 | 3778 | 3588 |
| Transliteration | ei | Petros | kai | epi | tautē | tē |
| Kigriki | εἶ | Πέτρος , | καὶ | ἐπὶ | ταύτῃ | τῇ |
| Kiswahili | ndiwe | Petro | na | juu ya | huu | |
| Kingereza | are | Peter | and | on | this | the |
| | | | | | | |
| Strong's # | 4073 | 3618 | 1473 | 3588 | 1577 | 2532 |
| Transliteration | petra | oikodomēsō | mou | tēn | ekklēsian | kai |
| Kigriki | πέτρᾳ | οἰκοδομήσω | μου | τὴν | ἐκκλησίαν , | καὶ |
| Kiswahili | mwamba | nitajenga | langu | | kanisa | wala |
| Kingereza | rock | I will build | my | - | church | and |
| | | | | | | |
| Strong's # | 4439 | 86 | 3756 | 2729 | 846 | |
| Transliteration | pylai | hadou | ou | katischysousin | autēs | |
| Kigriki | πύλαι | ᾅδου* | οὐ | κατισχύσουσιν | αὐτῆς . | |
| Kiswahili | milango | ya kuzimu | hai- | -talishinda | | |
| Kingereza | [the] gates | of hades | not | will prevail against | it | |

# Kiambatanisho, vielelezo na chati







Inatumiwa kwa idhini ya; "World Video Bible School"{WVBS} yaani Shule ya Biblia kwa njia ya filamu ulimwengu. https://video.wvbs.org/




Inatumiwa kwa idhini ya; "World Video Bible School"{WVBS} yaani Shule ya Biblia kwa njia ya filamu ulimwengu. https://video.wvbs.org/


Je, tunakwend
wapi tunap
Ulimwengu
(Mahali pa kuishi)
Sheol au Ku
(Mahali pa w
Mauti
Paradis
Waliookolewa
Mlango mwembamba
Kumewekwa Shim
Mateso
Waliopotea
Mlango
mpana
Mauti
WALIOOKOLEWA: Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakioko
WALIOPOTEA: Wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu (2
MAUTI: Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa huku
MLANGO MPANA: Mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni weng
MLANGO MWEMBAMBA: Mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uziman
PARADISO: Utakuwa pamoja nami peponi. (Luka 23:43)
MATESO: Kuzimu alipokuwa katika mateso (Luka 16:23)
UFUFUO: Ufufuo wa wafu (1 Wakorintho 15:42-44)
SIKU YA HUKUMU: Na kama vile watu walivyowekewa kufa mara moja, na baada ya
MBINGUNI: Urithi uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu (1 Petro 1:4).
JEHANAMU: Mungu ana uwezo wa kuangamiza mwili na roho pia katika jehanamu
SHIMO KUBWA: Kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa (Luka 16:26)


la
okufa?
zimu
afu)
o
mo Kubwa
Kuzawadiwa
"Njoni"
Siku ya
Hukumu
Kuhukumiwa
"Ondokeni"
Ufufuo
Mbinguni
"Njoni"
Njoni, mliobarikiwa
...urithini ufalme
(Mathayo 25:34)
"Ondokeni"
Ondokeni ...katika
moto wa milele
(Mathayo 25:41)
Jehanamu
lewa (Mdo 2:47)
Wathesalonike 1:7-8)
umu (Waebrania 9:27)
ji waingiao kwa mlango huo (Mathayo 7:13)
i, nao waionao ni wachache (Mathayo 7:14)
kufa hukumu (Waebrania 9:27)
Mathayo 10:28).



AMRI
Agano la Kale
(Kutoka 20:3-17)
1. Usiwe na
mingine ila
2. Usijifanyie sa
ya kuchonga
3. Usilitaje bure jin
Bwana, Mungu wak
4. Ikumbuke siku ya
Sabato uitakase
5. Waheshimu baba
na mama yako
6. Usiue
7. Usizini
8. Usiibe
9. Usimshuhudie
jirani yako uongo
10. Usitamani nyumba
jirani yako
"Tazama, nimekuja
Aondoa la Kwanza, ili
Akiisha kuifuta ile hati iliyo
hukumu zake, iliyokuwa na
isiwepo tena, akaigo
Lilitolewa kwa taifa la Israeli (Wayahudi) PEKEE
Likawa sheria yenye nguvu kwa waisraeli baada tu ya kutoka Misri.
Amri kumi na sheria zilitolewa kupitia Musa
Amri kumi zilikoma kuwa sheria takribani mwaka 33 B.K
Amri kumi HAZIFANYI kazi leo. (Wakolosai 2:14)
Lilia


KUMI?
Agano Jipya
(2 Wakorintho 3:3)
1. Kuna Mungu mmoja tu
1 Wakorintho 8:6, Waefeso 4:5, Yohana 17:3
2. Jilinde nafsi zenu na sanamu
1 Yohana 5:21, Ufunuo 21:8
3. Usiape
Mathayo 5:34
4. Abudu siku ya kwanza ya Juma
1 Wakorintho 16:2, Mdo. 20:7
5. Waheshimu baba yako na mama yako.
Waefeso 6:1-2; Wakolosai 3:20
6. Usiue
Ufunuo 21:8; I Yohana 3:15
7. Usizini
1 Wakorintho 6:9,10; Waebrania 13:4
8. Usiibe
Waefeso 4:28; 1 Wakorintho 6:9,10
9. Usiseme uongo
Waefeso 4:25; Wakolosai 3:9
10. Usitamani
Wakolosai 3:5; 1 Wakorintho 6:10
nifanye mapenzi yako.”
kusudi alisimamishe la pili.
Waebrania 10:9
andikwa ya kutushitaki kwa
a uadui kwetu; akaiondoa
ngomea msalabani.
Wakolosai 2:14
“Yesu akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako.Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii.”
Mathayo 22:37-40
anza kuwa na nguvu takribani mwaka 33 B.K kwa watu wote wa ulimwengu huu.
©2009 WORLD VODEO BIBLE SCHOOL®



# Makanisa
# Mstari

Tangu Kipindi cha Agano Jipya hadi Le

Kanisa la Karne ya Kwanza

Kanisa la Agano Jipya
Lilianzishwa siku ya
Pentekoste: 33 B.K.
Matendo 2:38-47

A.D. 325

394 593 606 1000 1015 1054

Kanisa la Katoliki [Konstantine]

Kanisa la Katoliki la (Roma)

Kanisa la Orthodox la (Uyuna
(Madhehebu haya yapo hadi leo)

325 B.K.: Baraza la Nikea – Mwanzo wa Madhehebu ya Katoliki
394 B.K.: Misa/Ibada kwa Kilatini
593 B.K.: Fundisho ya Toharani
606 B.K.: Papa wa Kwanza Rasmi – "Mungu Duniani."
1000 B.K.: Fundisho la Mkate kuwa Mwili Halisi wa Yesu
1015 B.K.: Useja kwa Makasisi kuwa Amri
1054 B.K.: Matengano katika "Katoliki"

1192 B.K.: Fundisho la Kulipia Dham
1215 B.K.: Maungamo ya Dhanbi – "
1311 B.K.: Kunyunyiza Badala ya ter
1870 B.K.: Tangazo la Papa kuwa Ha

# **Kwa nini** kuna **makanisa mengi**

Achilia mbali tofauti za makanisa na madhehebu mae
tumechanganyikiwa na kuachwa mdomo wazi. Ni kanisa lip
kanisa lipi lilianzishwa na Kristo? Katika Matendo 2, tunas
kuidhinishwana Mungu. Makundi mengi ya kidini yamejitenga
makanisa na madhehebu mbalimbali tuyashuhudiayo leo. Ik
karne ya kwanza, kama linavyotajwa katika Matendo 2, ni la
kisha kuwa kanisa sawia na jinsi t

Imeandaliwa na: Michael Shank
na kutafsiriwa na Christopher Mwakabanje


Hivi Leo
wa Nyakati
o
1906 Kanisa la Kikristo
1830 Wanafunzi wa Kristo
1192
1311
1517
1526
1870
1215
ni)
1536 Ukalvini [John Calvin]
1560 Presbateriani [John Knox]
1534 Kanisa la Uingereza: Anglikana na Episkopo
1739 Umethodisti [John Wesley]
1968 Kanisa la Methodisti
bi
"Kizimba cha Maungamo"
ndo la Ubatizo la Kuzamisha
akosei
1880 Wanaharakati Walokole [Sarah W. Lankford]
1521
Wanabaptisti
[Waliojitenga "wakazamishwa"
na Kujitenga na Ukatoliki]
1609 Kanisa la Baptisti [John Smyth]
[Makundi kadhaa yanayojimega kutoka Baptisti yanaendelea leo hii]
1865 Jeshi la Wokovu [William Booth]
1907 Mapatano ya Kibaptisti Kaskazini [Charles Evans Hughes]
1845 Mapatano ya Wabaptisti Kusini [William Bullein Johnson]
1820 - 1860 Waadventisti/ Wasabato [William Miller]
1536 Wamenonaiti [Menno Simons]
1690 Amish [Jacob Amman]
1526 Kanisa la Lutherani [Martin Luther]
hivi?
lfu elfu, yakikinzana kiitikadi na matendo duniani leo,
pi liko "sahihi?" Ni kanisa lipi limeidhinishwa na Mungu? Ni
soma habari za kanisa moja lililoasisiwa na Yesu Kristo na
a toka katika kanisa la karne ya kwanza, yakimeguka na kuwa
kiwa tunatafuta kuwa kanisa moja alilolianzisha Yesu Kristo
azima tuweke pembeni miongozo, mafundisho na mapokeo,
tunavyosoma katika Agano Jipya.
© 2014 World Video Bible School


VIPINDI
Mwanzo 1:1,26
KIPINDI CHA MABABA
Adamu
Kipindi cha mababa kilianzia katika bustani ya Edeni na kuendelea kuwe
na kipindi cha Musa.
Mungu alizungumza na mababa
Waeb
EDENI
KUTOKA
Dola ya Ashuru
Dola ya Babeli
Dola ya Uajemi
Dola ya Uyunani
GHARIKA
WAEBRANIA
KIPINDI CHA
Musa
Kipindi cha Musa kilianzia mlim
kuwepo sambamba na kipindi
Mungu alizungumza kupitia
Kuvuka Bahari ya Shamu
Kutoka 20
AMRI KUMI
SHERIA
Mlima Sinai
Hesabu 13:27
HEMA
HEKAL
© 2009 World Video Bible School



VYA BIBLIA
Je, ni lini kipindi cha Ukristo kitakoma?
“Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake.”
Mathayo 24:36
Kalvari
Waebrania 9:15-17
epo sambamba
rania 1:1
la ya
umi
KIPINDI CHA UKRISTO
Kristo
Kanisa la Kristo ndiyo ufalme
Mungu anazungumza kupitia Neno
Waebrania 4:12
KORNELIO
Mdo 10:1-48
Huduma ya Kristo
Mathayo 5:17
MUSA
PETRO SIKU YA PENTEKOSTE
na Sinai na kuendelea
cha Mababa
a Musa
Waebrania 9:18-20
UFALME ULIOGA WANYIKA
Biblia:
“Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.”
Luka 21:33
Mathayo 24:35
Mdo 2
Mataifa yote
Danieli 7:14
Wagalatia 3:28
LU
KRISTO

CHUMA NA UDONGO

## Rumi

(146 K.K. – 476 B.K.)

"miguu yake ni ya chuma; na nyayo za miguu yake nusu ya chuma na nusu ya udongo ... na ufalme wanne utakuwa na nguvu mfano wa chuma; ...bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu."
(Danieli 2:33, 40, 42, 43)



**Ufalme wa Mungu** Ulianzishwa (takribani 33 B.K.)

"Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele; wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele." (Danieli 2:44).

Agano Jipya linafunua kwamba Yesu na Yohana Mbatizaji walihubiri kuhusu kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu kwa kusema "umekaribia" (Mathayo 3:2; 4:17, 23). Kutokana na kwamba kanisa na ufalme ni kitu kimoja (Mathayo 16:18-19; Marko 9:1; Mdo 1:3; 2:38, 47; 8:12; Wakolosai 1:13), na kanisa lilianzishwa katika karne ya kwanza katika siku za utawala wa dola ya Kirumi, maana yake ni kwamba ufalme wa Mungu ulianzishwa katika karne ya kwanza kutokana na huduma ya duniani ya Yesu. Kanisa/ufalme linaundwa na watu kutoka mataifa yote (Isaya 2:1-2) na hivyo kuziangamiza "falme hizi zote" (Danieli 2:44) na linazungumziwa katika Agano Jipya kwamba lilianzishwa kwenye karne ya kwanza B.K. (Wakolosai 1:13, 2 Wathesalonike 1:5; Ufunuo 1:9). Ufalme huu bado upo leo, na wenye dhambi wote waliotubu wanaweza kuchagua kufanyika sehemu yake kwa kuzamishwa ndani ya Kristo. Yesu, akiwa kichwa cha kanisa lake na Mfalme wa wafalme wote (Wakolosai 1:18; 1 Timotheo 6:15), sasa anatawala katika ufalme wake – watu wake (Mdo. 2:36; Luka 17:21).

# Kitabu cha Danieli na Ufalme wa Mungu


(Kanisa)


| | DOLA ZA ZAMANI ZA MESOPOTOMIA NA MEDITERENIA | UNABII WA DANIELI NA TAFSIRI |
|---|---|---|
| DHAHABU | **Babeli** (625 K.K. – 539 K.K.) | "Na sanamu hii kichwa chake kilikuwa cha dhahabu safi ... na Mungu wa mbinguni amekupa ufalme ... Wewe (Nebukadreza wa Babeli) u kichwa kile cha dhahabu." (Danieli 2:32, 37, 38, pia 1:1) |
| FEDHA | **Umedi–Uajemi** (539 K.K. – 331 K.K.) | "Kifua chake na mikono yake ni ya fedha ... na baada ya zamani zako (Nebukadreza) utainuka ufalme mwingine mdogo kuliko wewe." (Danieli 2:32, 39, pia 8:20) |
| SHABA | **Uyunani** (331 K.K. – 63 K.K.) | "tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba ... na ufalme mwingine wa tatu wa shaba, utaitawala dunia yote." (Danieli 2:32, 39, pia 8:21) |







Imetayarishwa na Rob Baker



o
Ukweli
Timotheo 3:15
Wakristo
Mawe Yaliyo Hai
1 Petro 2:5
Yesu
Ndiye Mlango
Yohana 10:9
Ubatizo (Marko 16:16)
Kukiri (Warumi 10:9-10)
Tubu (Luka 13:3)
Amini (Yohana 8:24)
Sikia (Yohana 6:45)
World Video Bible School © 2007




metayarishwa na Rob Baker




World Video Bible School © 2007




1. Siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu. (Matendo 2:41)
2. Ilikuwa siku za mwisho. (Matendo 2:17-21)
3. Ilikuwa Yerusalemu. (Luka 24:46-49, Matendo 1:12, 2:1-5)
4. Ilikuwa katika siku za wafalme.
5. Ilikuwa katika siku ya baadhi ya wafuasi

(Matendo 1:15, 2:9)

6. Nguvu ikaja. (Matendo 2:1-4)
7. Mwanzo ukawa Roho Mtakatifu alipowashukia (Matendo 11:15). Roho Mtakatifu alishuka siku ya Pentekoste.
8. Maandiko yaoneshayo pande zote kabla ya kuja kwake na baada ya kuja kwake siku ya Pentekoste.

